# FAHAMU ZA KISIASA ZA HIZB UT-TAHRIR

## UTANGULIZI

Siasa ni kusimamia mambo ya Ummah kindani na kiinje na hutekelezwa na serikali na Ummah, hivyo basi serikali hutekelezwa usimamizi huu kivitendo, na Ummah ndio ambao kwao wanaihesabu serikali.

Na usimamizi wa mambo ya Ummah kindani na kiinje kwa upande wa serikali huwa kwa utabikishaji wa mfumo ndani, na hii ni siasa ya kindani.

Amma usimamizi wa mambo ya Ummah kiinje kwa upande wa serikali huwa ni mahusiano yake na madola na mataifa na watu wengine, na kueneza mfumo ulimwenguni, na hii ndio siasa ya kiinje.

Na kufahamu siasa ya kiinje ni suala muhimu la kuhifadhi muundo wa serikali na Ummah na suala msingi la kuwezesha kubeba ujumbe katika ulimwengu, na ni jambo lisilo na budi ili kuyapangilia mahusiano ya Ummah na Ummah nyenginezo juu ya mwelekeo wa sawa.

Na kwa kuwa Ummah wa Kiislamu umekalifishwa kuupeleka ujumbe wa Kiislamu kwa watu, basi imekuwa ni lazima juu ya Waislamu waufahamu ulimwengu ufahamu wa kuelewa hali zake, na kujua matatizo yake na kujua kwa misukumo ya serikali zake na watu wake, na wenye kufuatilizia shughuli za kisiasa ambazo hujiri katika ulimwengu, na ni wenye kudadisi mikakati ya kisiasa za serikali katika mbinu ya utekelezaji wake, na namna ya mahusiano yao wao kwa kwao, na miondoko ya kisiasa ambayo huichukua nchi, na kwa hivyo imekuwa ni lazima juu ya Waislamu kutambua msimamo wa kihakika katika ulimwengu wa Kiislamu juu ya

kufahamu msimamo wa kimatifa wa kiulimwengu, ili waweze wao kufafanua mbinu ya utekelezaji wa kuisimamisha serikali yao na kueneza ujumbe wao katika ulimwengu.
Isipokuwa ni muhimu ieleweke kuwa msimamo ya nchi huwa haibakii katika hali moja, hivyo basi hubadilika kwa mujibu wa mbadiliko wa hali ya kimataifa.
Na kuwa msimamo wa kila taifa miongoni mwa mataifa huwa haijilazimishi katika hali moja kiupande wa kiulimwengu bali huingiwa na mabadiliko wa hali tofauti tofauti kama nguvu na udhaifu, na katika upande wa utofauti wa mahusiano yaliopo kati yake nchi nyenginezo, na ikhtilafu wa mahusiano hayo. Hivyo basi haiwezekani kupeana misingi mipana ilio thabiti ya msimamo wa nchi yoyote miongoni mwa nchi zilizosimama kati ulimwengu bali yawezekana kutoa msingi mpana kuhusu msimamo wa kimataifa katika fulani, pamoja na picha ya uwezekano wa kubadilika msimamo huo, na kupeana fikra Fulani kuhusu msimamo wa nchi yoyote katika dhurufu Fulani, pamoja na kuelewa kuna uwezekano wa kubadilika msimamo huo, hivyo basi haitoshelezi kwa mwana siasa kufuatilizia siasa zilizoko katika ulimwengu na aziunganishe kwa ufahamu wake wa kale wa kisiasa, ili iweze kumbainikia na kufahamu siasa ufahamu wa sawa na aweze kupata maarifa fulani iwapo msimamo wa kiulimwengu upo vile vile kama ulivyokuwa au umebadilika na ili aweze kujua msimamo wa kila nchi na maarifa fulani iwapo msimamo huo bado upo katika hali ile ile au imeingia na mabadiliko.
Na mabadiliko wa msimamo wa kimataifa hufuata mabadiliko ya msimamo wa baadhi ya madola kutoka hali moja hadi hali nyengine, imma kwa nguvu zake, na

imma kwa udhaifu wake na imma kwa nguvu za mahusiano yake kwa madola mengine, au kwa udhaifu wa mahusiano hayo, na wakati huop itapatikanwa mabadailko katika mizani ya kiulimwengu, kwa kupatikanwa mbadiliko katika mizani ya nguvu iliosimama katika ulimwengu, hivyo basi kufahamu msimamo wa kila dola miongoni mwa madola ambazo zina taathira katika msimamo wa kimataifa imekuwa ni msingi wa kufahamu msimamo wa kiulimwengu. Na mpaka hapa umuhimu imelengwa juu ya kuzingira kwa maaluma kuhusu kila dola kwa sababu ndio nguzo ya kwanza ya kufahamu siasa. Na wala sio kujua msimamowa kila dola inaohusiana na masuala yake katika msimamo wa kiulimwengu, bali ni mahusiano katika kia kitu kilicho na mahusiano na siasa zake za kindani na za kigeni. Na mpaka hapa ni lazima kujua fikra ambayo juu yake imesimama siasa za madola zilizosimama katika ulimwengu, na ambayo ina umuhimu inaozungumzwa katika msimamo ambao inaowawajibisha Ummah wa Kiislamu kuchukua ndani yake. Vile vile ni lazima ijulikanwe mipango na mbinu ambazo inazozitumia na iunganishe maarifa ya mipango na mbinu kwa kufuatilizia kwa daima, na kujua kiwango cha mabadiliko wake. Na kujua misukumo ambayo iliopelekea kubadilika kwake, au sababu ambazo zilizopelekea madola haya kubadilisha mipango na mbinu, pamoja na kujua vyema mambo ambayo huathiri dola hizi au zinazopelekea kubadilisha mipango yake na mbinu zake.

## SIASA NI FIKRA NA TWARIKA

Ama fikra ambayo juu yake hujengwa siasa za serikali huwa ni fikra ambazo hujengwa juu ya msingi wae mahusiano yake na mataifa na watu wengine. Hivyo basi serikali isiokuwa na mfumo basi fikra kwake huwa tofauti na kuna uwezekano wa kubadilika, na dola aina hizi huingiwa suala la utafiti mikakati na mbinu za kisiasa, na wala haingiwi na utafiti wa fikra za kisiasa.

Ama dola ambayo ina ifumo ilishakana nao bai firka zake huwa thabiti hazibadiliki, nao ni kueneza mfumo ulishikamana nao katika ulimwengu kwa Twarika thabiti isiobadilika, hatia ikitofautika mbinu na kubadilika, na huingiwa utafiti wa fikra za kisiasa juu yake.

Ni wajibu zitizamwe dola zilizosimama katika ulimwengu zitizamwe juu ya msingi huu, kwa kuzingatia kuwa kila moja wapo miongoni mwake ina fikra msingi ya mahusiano yake na mataifa na watu wengine, ilithabiti au isio thabiti, na ina Twarika maalum ya kutekeleza fikra hii, thabiti au isio kuwa thabiti, a juu ya mwangaza wa fikra yake na Twarika yake huchorwa mipango na kufuatwa malengo yake. Isipokuwa dola zilizosimama katika ulimwengu leo huwa zinajitafutilia zenyewe mbinu, na kufuata mbinu itakaohakikisha lengo, hata kama itagongana na Twarika, na zinakwenda juu ya qaida ya (lengo huhalalisha mbinu)

Na namna iwavyo hakika dola zote huweka mikakati ya kisiasa na kubadilisha kulingania na haja, na kufuatwa kwa mbinu hubadilika na kutafautika kulingania na hali. Na dola katika matendo yake ya kisiasa huchunga masilahi ya Ummah, na huweka mahusiano yake na dola nyengine kwa mujibu wa masilahi, isipokuwa hutafautiana katika hilo kwa tofauti kubwa. Hivyo basi

dola ambayo haibebi mfumo maalum hufanya masilahi ndio pekee kinachoathiri katika mahusiano yake ya kiulimwengu huufanya mfumo kuwa kiungo cha kisaidizi katika njia hii, hivyo basi ni lazima dola ijulikanwe kwa upande wa fikra mabazo zinabeba, jee ni dola inaobeba mfumo au haibebi mfumo wowote? Wakati huo itajulikawa viungo ambavyo vinaathiri katika mahusiano yake ya kiulimwengu. Na kwa kuwa mfumo ndio ambao unaoathiri katika mahusiano ya kiulimwengu na katika msimamo ya kiulimwengu, hivyo basi imekuwa ni wajibu kujua mifumo ambayo inaotawala ulimwengu leo, na ijulikanwe upeo wa taathira wa kila mmoja miongoni mwao katika siasa za kiulimwengu leo, na upeo wa uwezekano wa kuathiri kwake katika siasa za kiulimwengu katika siku za usoni, na wakati huo itajulikanwa kwa uwazi kifumo hii na upeo wa kuathiri kwake katika mahusiano za kiulimwengu siku za sasa na za usoni.

Na tukiuangalia ulimwengu leo tutakuta unatwaliwa na mifumo matatu pekee, nayo ni : - Uislamu, ukomunisti, uraslimali, na kila mfumo unaobewa na mamilioni ya wanadamu, isipokuwa Uislamu hauna serikali kwa sasa, na ni kwa sababu hiyo hatuoni kuwepo kwake katika mahusiano ya kiulimwengu, na wala katika msimamo wao kiulimwengu, na wala katika msimamo wa kiulimwengu ambao utawala ulimwengu leo. Ama yale tyanaotendwa na madola ya ulimwengu la kuzuia kwa kurudi dola la Kiislamu katika waqla wa maisha, baada ya kuwa ni wenye kuonekanwa na vijana wa Ummah wa Kiislamu, hivyo basi hauna mahusiano na msimamo wa kiulimwengu, na wala hauathiri katika mahusiano ya kiulimwengu huhitaji kuwepo kwa dola litakoubeba

mfumo wa Uislamu na kuupeleka siasa zake za kindani na za kigeni juu ya msingi wake.
Ama yale yanao oneknwa kutokamana na mwelekeo wa siasa za kiulimwengu na khususan Amerika, la kujaribu kuyawekea maeneo ya Kiislamu kwa lengo la kuyakoloni mfano wa (mashruu makubwa ya mashariki ya kati) katika mwaka 2003 miladi, bila shaka hili ni katika natija ya fikra hatari inaozidi kwa dola hizo ila kutarajia kukaribia kusimamia kwa serikali ya Waislamu, na wala sio eti Uislamu unaathri katika siasa za kiulimwengu taathira inaojulikanwa kama vile lau kama Uislamu una dola iliosimama kihakika.
Ama mifumo mengine miwili, kwani kila mmoja wapo una dola kadhaa, na kwa sababu hiyo ikawa ina athri katika mahusiano ya kiulimwengu, na katika msimamo wa kiulimwengu, na katika siasa za kiulimwengu, na haswa wakati umoja wa usovieti ulipokuwa umesimam kabla ya kuvunjika kwake, n amiongoni mwa atahri zake ni kuwa ulimwengu katika kambi mbili ikawa kuna kambi ya mshariki na kambi ya magharibi. Isipokuwa kuanguka kwa kambi ya kimashiriki na kuvunjika kwa muunganio wa Warsaw, ikimalizika siasa ya maqiatbi katika ulimwengu, na ukomunisti haukuwa unatabikishwa katika dola angalau kwa muundo isipokuwa katika uchina na Korea kaskazini, na kwa hilo yakakoma mapambano ya kiulimwengu na yakawa ni ya kimaeneo baada ya hapo. Kwani kwa kuanguka kwa muungano wa usovieti fikra yake haikuwa ni yenye kuathiri katika siasa za kimataifa na hili linarudia fikra ambayo iliokuwa juu yake imesimama siasa za kigeni, nao ni kueneza ukomunisti siasa zao za kigeni hazikusimama juu ya fikra hii. Hivyo basi siasa za uchina haziusimama

juu ya msingi wa kueneza ukomunisti katika ulimwengu na hili larudia waqia ya watu wa itbari katika uijirani ya Asia, na katika maisha yao hawakuwa na haja ya kuwa na itibari ya kiulimwengu. Na kwa sababu ya waqia huu ya watu wa kujitayarisha nafsi yake na nguvu zake ili ipate kuathiri katika siasa za kiulimwengu, na bado vitendo vyote vya uchina vimeelekezwa katika kuleta itibari ya kimaeneo katika jirani yao.
Ama kambi ya kirasilimali, hakika kwao fikra ambazo juu yake siasa zimesimama ni kueneza mfumo wa kirasilimali, nao ni kutengamanisha dini na maisha katika ulimwengu mzima, pamoja na uweingi na tofauti wa dola ambazo zinazoubeba mfumo wa kirasilimali lakini zote zinaeneza fikra kiongozi yao ya kirasilimali katika ulimwengu, na kuufanya mwelekeo wa mtazamo wa kimaisha ndio ambao unaotawala katuika ulimwengu.
Ama Twarika ambayo hufuatwa na kambi ya kirasilimali ili itekeleza fikra yake hiyo ni ukoloni, yaani kulazimisha utawala wa kisiasa na wa kijeshi na kithaqafa na wa kiuchumi juu ya watu walioshindwa ili kuwanyanyasa, na Twarika hiyo nao ni ukoloni ni thabiti wala haibadiliki vyovyote zitakazo badilika tawala, namna zitavyo tofautiana kanuni zao. Na ukoloni sio kama vile anavyosema Lenin "Ni daraja ya juu zaidi ya urasilimali" bali ukoloni ni sehemu ya mwelekeo wa mtazamo katika urasilimali, nao ni Twarika ambayo kwao huenezwa urasilimali katika mataifa na watu. Hivyo basi siasa ya kigeni ya kambi ya kirasilimali ni thabiti katika fikra yake na njia yake, na wala hayabadilishwi na ikhtilafu za madala na mashindano yao. Hivyo basi uiengereza ni mfano wa Amerika na mfano wa Ufaransa na ni mfano wa Italia na mfano wa diola yoyote miongoni mwa

madola ya kirasilimali, msingi wa siasa zake ni kueneza mfumo wake na mwelekeo wa mtazamo wake katika maisha kwa kupitia kukoloni mataifa na watu.
Na ni wajibu ieleweke kuwa katika kufahamu Twarika ya kambi ya wamagharibi kuwa Twarika hii, hata kama ni thabiti katika asili yake (ukoloni) isipokuwa mbinu ya kulifikia (ukoloni) na mtazamo wake yameingiwa na maendeleo fulani katika kambi ya mmagharibi, katika upande wa kushikana kwake kama Twarika kwa urasilimali kama fikra, pamoja na wakati, na katika jumla ya kuendelea kwake na yale yalioingia ndani mwakekatika mabadiliko katika mbinu na tofauti katika mtazamo wa kukoloni. Ama kubadilika kwa mbinu yake, ni katika kile kilichoitwa ukoloni wa kale ni kumakinisha kijeshi koloni, kisha ikawa ni ukoloni mambo leo nao unategemea mambo mengine. Kwa hivyo Amerika ikawa inategemea upande wa kiuchumi kama mikopo na yale yalioitwa mikakati ya maendeleo na mfano wa wajuzi na mengineo, na upande wa ukandamizaji wa kisiasa na kulazimishwa. Baadaye Amerika ikarudia upande wa mbinu hizi hadi mbinu ya utawala wa kijeshi juu ya mataifa na watu ili kuzifanya chini ya itibari yake na matakwa yake. Na ikawa inakimbilia kuweka kambi za kijeshi katika koloni zake ili kulinda itibari yake humo. Na uiengereza ikawa inategemea mbinu ya kuweka watu watakao kuwa vibaraka wake, na watu wa ujasusi wa kienegerza na watawala wa nchi katika vibaraka wake, na mikataba miovu ya kibiashara na akadhoofika kutegemea mikopo kwa sababu ya udhaifu wa hali kimali. Vile ikadhoofika kutegemea kambi za kijeshi kwa sababu ya kudhoofika itibari yake kimataifa, hata hivyo bado inazuia kuwepo kwa kambi za kijeshi na kambi katika

koloni zake kama ilivyo katika Kopras (Cyprus) au karibu na koloni hizi, hivyo basi kubadilika katika mbinu ni kiungo muhimu cha ukoloni.

Ama tofauti ya mtazamo wa ukoloni, katika upande wa kushikamana kwake (kama Twarika) na urasilimali (kama fikra), hayo hurudia katia ya nguvu ya mshikamani huu, yaani ukoloni ni twarika pekee ya kueneza urasilimali, na yale yanaomaanishwa ni kuwa umuhimu wa kwanza ni kwa kueneza urasilimali, na baina ya udhaifu wa mshikamano huu, yaani umuhimu wa kwanza ni ukoloni wenyewe na umuhimu wa pili ni kueneza urasilimali, ni kan kwamba ukoloni umekurubia kuwa ndio lengo, na nguvu wa ushikamanao au udhaifu wake inategemea biladi ambao inaolengwa kutawaliwa na madola ya kirasilimali, jee ni yenye hadahra inataka kuivamia na kuingiza hadahra ya kirasilimali iliofisidifu. Ili kuwa sahali kuitawala nakupora utajiri wake au ni tupu isio na hadhara na inahitajo uvamizi, bali wataikoloni ili wapore utajiri wake na kutawala pekee? Na hili labainika katika ukweli wa mvutano wa dola za kimagharibi katika kukoloni kwaAfrika ulikuwa umechukua upande wa kuliibia, na ikakaribia kuwa kueneza kwa fikra ya kirasilimali kukosekanwa. Kwani vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Uganda na Rwanda viliendelea kwa miaka na waathiriwa wake wakawa ni mamia kwa maelfu ya wanadmu, na pia matukio ya Zaire (demokrasia Congo) na hakukuridhika humo ila uroho wa kimada na mvutano wa itibari baina ya Uropa na Amerika. Na wala haikuwa uingereza na wale waliokuwa pamoja nao wauropa na Amerika wakiangalia kitu chengine katika Afrika isipokuwa manufaa ya kimada, hivyo basi ukoloni katika Afrika ulikuwa umekuruba kuwa ndio lengo

kuliko kuwa twarika. Ama katika ulimwengu wa Kiislamu, katika mashariki ya kati na kaskazini mwa Afrika au Asia yakati na kusini ya mashariki yake, kwni dola za kikoloni zikiongozwa na Amerika zinakimbilia huko pamoja na kutawala kisiasa na kijeshi na kiuchumi katika ulimwengu wa Kiislamu pia kwa ajili ya maslahi yakimada pia zinakimbiia kueneza urasilimali kwa njia nyingi, kwa mfano juhdi zao wa warsha uhuru wa mwanamke) na kummakinish amwanamke nayale yaliokuja katika mpango wa kiamerika ya mashariki ya kati, na kulazimisha itibari ya kuthaqafa na ikawa inajuliknwa kama kurudi kujenga thaqafa na mazungumzo kati ya dini na makutano ya hadhara na kumakinishwa mabadiliko au marekebisho na mifumo ya kiilemu, ili kuondosha mafungamano ya Waislamu na hadahra yao na thaqafa yao. Na hivi ndivyo twarika katika urasilimali inapiga hatua pamoja na wakati, pamoja n ahayo ukoloni ni nguzo msingi katika urasilimali, iwe ndio twarika ya kueneza urasilimali au twarika iliokaribu na lengo.

## MIKAKATI NA MBINU ZA KISIASA

Mikakati ya kisiasa na mbinu ambayo hutuekelezwa nayo mikakati hiyo hubadilika kulingania na masalahi japo mikakati hubadilika kwa uchache kuliko mbinu, na tofauti kati ya mikakati na mbinu ni kama inavyoonekanwa katika kufuatilia siasa za kimataifa ni kuwa nmikakati ya kisiasa ni jumla, huwekwa ili kufikia lengo miongoni mwa malengo yanayohitajika kueneza mfumo au twarika yakuueneza, ama mbinu ni siasa maalum katika sehemu miongoni mwa sehemu ambazo zinsaidia kutekelez amikakati na kumakinishwa kwake.

Kwa mfano mpango a kiamerika kuhusu Iraqi ilikuwa ni kuikoloni kwa maazimio au bila ya maazimio ya kiulimwengu, baadaye kuweka serikali itakao halalisha ukolini kisheria kupitia umoja wa mataifa, baada ya kuwa imepuuzwa mwanzoni wa kukoloniwa, na Sheria nyengine ni za (ndani) kupitia serikali hiyo kwa niaba ya watu wa Iraq kutia sahihi mkataba utakao ruhusu kubakia kwa jeshi la ukoloni ili lipewe sifa ya kisheria, kwa kuwepo kwake kupitia makubaliano ya wananchi kutaka kwa na maazimio ya kiulimwengu. Na hili litawarudisha nyuma mataifa mengine na baraza la amani kuingilia masuala ya Iraq, na litafanya Amerika ndio mpelekeji wa masuala yote ya Iraq na kwa hili litahalalisha ukoloni kwa sababu kilichomfanya kubakia kwake na kuwepo kwake ni serikali ya kisheria (iliochaguliwa). Na Iraq itapewa katiba mpya chini ya usimamizi wa ukoloni, na hapo mgawanyiko utapewa umuhimu na nchi kugawanywa kwa hujj na majimbo na itawashwa mioto ya kimadhehebu, na waislamu watashughulishwa na kumtoa mkoloni, na kwa sababu hiyo Amerika ilitumia kila iwezavyo katika mbinu na namna ili kuikoloni Iraq kwa mujibu wa mpango uliowekwa, na baadaye kuhlalisha ukoloni huu kwa kuipatia uhalali kwa sura ya kisheria za kimataifa na za nchi.

Na upande wa pili mpango wa ufaransa ulikuwa ni kuleta mazungumzo katia ya madola makubwa chini ya uongozi wake ili kupambana na mpango wa kiamerika na ukakamilika mpango huo kwa kuweka pingamizi kupitia baraz ala Uislamu na kutoa maazimio wazi na kuunyima hifadhi mpango wa kiamerika wa kutumia baraza ili kuivamia Iraq, hivyo basi Amerika ikashindwa kabisa kucheza na karata ya baraza la usalama, na ikaweza

kukashifika kiulimwengu kuwa ni dola iliokiuka knuni, hivyo basi Amerika ikadhihirka kuwa inakwenda kinguvu kidhalimu na inakiuka kanuni, badali ya kudhihirika kuwa ni mlinzi wa kanuni za kiulimwengu kama ilivyo kuwa inadhihirika hapo zamani. Na ufaransa ikaweza kuamsha hisia za ujerumani na kuziathiri, kiasi cha kumuudhi Amerika katika kitendo chao, na Urusi pia ikasimama upande wa Ufaransa katika kumpinga Amerika kutumia baraza la amani ili imsaidia katika mipando yake, na hivi ndivyo ulivyofaulu mpango wa Ufaransa, sio katika uvamizi wa Amerika lakini katika kufedhehi malengo ya Amerika katika uvamizi huu.

Ama mpango wa kiengereza ilikuwa ni wa kimatata muovu, ilimsaidia Amerika kimacho ili anye apate chochote katika ghanima, na kujitokeza pamoja naye juu ya jukwa la kiulimwengu iwapo upande wa Amerika ndio mzito, na kumgonga visu katika mgongo kila anapweza kudunga. Kwa hivyo uingereza ilimuandama Amerika kwa sababu upande wake ulikuwa na uzito katika msimamo wa kiulimwengu, lakini kwa upande mwengine ilimrudisha kuchukua azimio kutoka baraza la usa;lama haswa kuifanyia uadui Iraqna tangu hapo awali ilikuwa inajua kutowezekana kutoka maazimio kutokamana na msimamo wa Ufaransa na Urusi na Ujerumani, hivyo basi ikadhihirika kwa hilo aibu ya Amerika kuwa inataka kuifanyia uadui Iraq kwa maazimio au bila maazimio. Na Uingereza ikasisitiza hilo katika mkutano uliohudhuriwa na Blair na Chirac na Shroeder katika 20/09/03 miladi, ili kutumia uerevu wa kisiasa wa kiengereza katika kumakinishwa na kukitisha msimamo wa dola mbili dhidi ya msimamo wa kiamerika, kwa kudharau kwa baadhi za rai zilizotolewa na muingereza au mfano wake, na

litawafanya kujificha na kujitokeza kwa muingereza wazi kwa hilo mbele ya muamerika. Na uingereza ikaendelea na siasa hiyo hiyo hata baada ya kukoloni Iraq, na muamerika kuupeleka mpango wake kwa umoja wa mataifa ili kuhalalisha kisheria ukoloni.

Na mfano wa mpango wa Amerika ilioweka ili kuzuia muungano wa Uropa kuwa wammoja na kuwa tishio kwa Amerika na iliosimama juu ya misingi ya jira tatu nayo: -

Ya kwanza: - kupanua muunganio wa uropa kwa madola ya mashairki ya Uropa, na madola haya ni vibaraka wa Amerika, na vichwa vya silaha yake, ili kuingiza tathria za Amerika katika muungano. Na hili lilidhihirika pindi dola hizi zilipounga mkono maoni ya Amerikakatika kuivamia Iraq, na ndicho kilichomfanya Ramsfield kuikejeli Uropa kwakuiita ya kale na mpya. Na Chirac raisi wa Ufaransa alikasirishwa na kitendo hicho cha madola hayo, na akajaribu kuwatishia kuwa kuchagua kwao kuwa upande wa Amerika itakuwa ni kizuizi kwao mwisho kukubaliwa katika muungano pamoja na hayo walikubaliwa kuunganakatika mkutano wa muungano wa Uropa ulioweka kwa ajili ya kukubali wanachama wapya na wala Ufaransa haikuweza kuwazuia kujiunga.

Ya pili: - kuwepo kw amuungano wa Atlantic (Nato) pamoja na kuvunjika kwa upinzani WARSAW, kisha kupanua muungano ki-istratijia ili iingilekatika matatizo ya kiamani katika Uropa badali ya kuihami kiinje kama ilivyo kuwa asili ya shughuli zake. Na pindi Uropa ilipohisi hatari ya muungano dhidi yake kwa kuongozwa na Amerika kivitendo, Ufaransa na Ujerumani na Ubelgiji na Luxemborg zikalingania kuundwa kwa nguvu maalum ya uropa, Amerika ikapinga hilo na bado inasababisha

Uropa shida hata kabla ya kuona nguvu maalum za kiuropa zikijitokeza.
Ya tatu: - Amerika kufaidika kwa msimamo wa Uingereza kwani uingereza kwa urefu wake wajadi haitaki muungano wa Uropa kuwa ni nguvu moja na baadaye Uingereza iyayuke humo na kuwa dola sawa kama Luxemborg, kwani bado uinabeba ndani ya ubwenyenye wa kibepari ambayo umilikaji wake hazijatoweka juani, na ndio maana twaiona kuwa nikizuizi cha kuleta muungano, na wala haikuvunjika ila pale ilipoona waqia, na ikajiunga ili kudhooofisha, na mpaka leo bnado haijaungana katika sarafu moja za kiuropa (Euro). Na fikra za kibepari zinaifanya Kutafuta dori juu ya jukwaa la kimataifa kwa njia yoyote ile itakaoipata.
Na kwa upande wa pili mpango wa Ufaransa ulikuwa ni kupitia nguvu muungano wa Uropa na kuufanya mwavuli unaofaa kupambana na mwavuli wa Amerika, na kukimbilia kulianzisha kwa jeshi la Uropa kando na muungano wa kaskazini Atlantic (Nato), na ilioweza kuvutia katika upande wake Ujerumani kuhusu hilo, na Ufaransa ikacheza mchezo wa kiuerevu mno kwa kuweka mkataba na Ujerumani, kwa kiasi ambacho iliifanya Uingereza kuungana nao ili isikose fungu katika ghanima iwapo zitafaulu juhudi za Ufaransa na Ujerumani. Na hivi ndivyo Ufaransa ilivyo faulu hivi karibuni pamoja na Uingereza na Ujerumani katika kuanzisha kiini cha hili jeshi, pamoja na misukumo mkali kutoka kwa Amerika juu ya Uingereza na Ujerumani kuzuia kulibuni. Vile vile zilifaulu mikakati ya madola tatu katika kuweka siasa zenye upeo wa mbali ya muungano katika muungano na dola zinazo weza kuathirika kama Italia na Uhispania.

Na hivi ndivyo twkauta namna ambavyo Ufaransa ilivyofaulu katika kuweka njia, hata kama muanzoni mwake ilikuwa ni kuupatia nguvu muungano wa Uropa na kubuni kiini cha kijeshi huru katika uropa kw akukubaliana na Ujerumani na Uingereza. Na lau kama dola hizi sio kushikana kwao na urasilimali ambayo hufanya (masilahi maalum) maadili ya kila dola ndio kipao mbele, basi wangeliweza kuleta muungano wa uropa ulio na nguvu mbele ya Amerika, pamoja na hayo kule kufaulu tu kwa Ufaransa katika kuweka mpango juu ya dola zilizo na nguvu katika uropa (Ujerumani na Uingereza) huchukuliwa kuwa ni kitendo cha athari mbele ya Amerika na katu haitoweza kukipuuza.
Na mfano wa mpango ambao Amerika ulioweka ili kakanyagiza Urusi na kuifanya kuwa ni dola isio na itibari hata ya kieneo pia, na inatekeleza hayo kwa kuitoa katika sehemu za itibari zake katika Balkan na mashariki ya Uropa na Asia ya kati na pia kufunga vijalishaji vyake vya silaha za nuclear ambazo ni kiungo muhimu katika viungo vya nguvu zake kuongozea hadi kumtangulia katika anga, hivyo basi ikatumia mbinu kadhaa kufikia hayo, ikiwemo kulipiga jeshi la Yugoslavia (Serbia na jabali jeusi) kule kuliko na mahusiano (kijamii ya kale) pamoja na Urusi, kupitia mzozo wa Kosovo, vile cile ikaweka mahusiano ya kiuchumi na ya kijeshi pamoja na za mashariki ya uropa ili kupenyesha itibari zake humo, kisha ikwa kuwaunganisha wengi wao katika muungano wa kaskazini wa Atlantic (Nato) na vile vile ilipata fursa ya kutumia vita dhidi ya ugaidi na ikaweka kambi zake za kijeshi katika dola za Asia ya kati na hili baada ya kuwa imeweza kuwavutia baadhi ya watawala wa dola kupitia misaada ya kiuchumi, na ikakoloni Afghanistan na

ikakimbilia kuendeleza mfumo wa kinga ya makombora ya Urusi yanaopita katika bara yalio na uwezo wa kubeba vichwa vya nuclear. Vile vile iliweza kutumia suala la ufukara katika Georgia na kuwaweka vibaraka wake katika kilele cha haram (piramidi) na ndicho kilichofanya eneo kuanguka nyongo kati ya Urusi na muungano wa Nato katika Uturuki, na ilikuwa imeikinaisha Urusi kuachana na vituo vyake vya ana mara na kushiriki katika Kituo cha anga katika kiulimwengu "ISS" na hili ni kumwekea mipaka katika mashindano ya kuvamia anga. Na hivi ndivyo inavyoendelea Amerika katika mipango yake ya kumzingira Urusi ili ibakie dola lisilo na itibari ya kimaeneo baada ya kukata itibari yake kiulimwengu kwa kuanguka kwa muungano wa Usovieti.

Na hali Kadhalika kwa Uchina, kwa sababu Amerika inaona uwajibu wa kuipigisha magoti Uchina, na kuifanya ni dola kawaida haswa kwa kuwa haimiliki sifa za dola kuu, lakini imekuwa ani dola kuu ya kimaeneo tangu nusu ya tisaini kwa nguvu inazomiliki na ina kura turufu katika baraza la usalama na ina malengo na matarajio ya kiaeneo, na hili ndilo ambalo lisilomridhisha Amerika. Hivyo basi Uchina katika jicho la Amerika ni soko kubwa la kibiashara na ni lazima iafaidike nalo, na binadamu wengi ambao ni wajibu wachungwe, ili wasije wakawa ni hatari watakao tishia masilahi ya kiamerika katika eneo la mashariki ya Asia, hivyo basi ilikuwa juu ya Amerika kuweka mikakati baada ya kumalizika kwa vita vya baridi ili kuikanyagia Uchina, na kuifungia katika sehemu dhiki, iwapo haitoweza kuikata kikamuilifu kiameneo, hivyo basi umuhimu wake ilikuwa ni kusawazisha mahusiano na Vietnem na ili aifanye kuwa ni jiwe kizingiti mbele ya Uchina wakati yatakapo tengenezeka

mahusiano ya Amerika ya Vietnam. Vile vile inaribu kuifanya kisiwa cha korea kuwa ndio kituo kilichoendelea cha hatari ubavuni mwa Uchina, kwa kuzidi kuikandamiza Korea kaskazini kwa hijja ya jira ya shri na wakati huo huo inaendela kubakisha kambi zake za kijeshi huko karibu na mipaka ya Uchina na mlangoni mwake. Vile vile inajaribu kuifanya Hind (India) mfano wa uchina na pia inafanya bidii ya kuleta muungano wa istratijia na muungano wa kijeshi la kieneo katika Asia ya kati na mashariki ya kati, vile vile imeweka kambi za kijeshi katikati ya Asia katika mipaka ya magharibi ya Uchina kwa upande mwengine wa Himalaya.

Hivyo basi mikakati na mbinu ya kisiasa huwekwa kwa ajili ya kitendo cha papo hapo, lakini pamoja na hayo serikali haichukui muda kubadilisha mbinu zilizoko, na Kutafuta mbinu nyengine iwapo itadhihirka kuwa mbinu zile hazitoweza kuwafikisha katika mlaengo, na vile vile inaoweza kubadilisha mikakati iwapo haitofaa, au iwapo kubakia kwake itaipatia serikali taabu na wala kuwepo kwake haina masilahi, lakini pindi serikali badali yake na pindi inapo badilisha mbinu huwekwa mahala pake mbinu nyengine, na wala haiwachi kuweka mkpango na mbinu isipokuwa iwapo itashuka na kuporomoka hadhi yake katika msimamo wa kiulimwengu, kama hali ilivyo kuwa madola ambayo yalipoteza itibari zake za kisiasa tangu zamani, kwa mfano Japan na Italia na Uholanzi na Ubelgiji na Uhispania na Ureno.

Na mfano wa kubadilisha mikakati ni yale yaliofanywa na Amerika katika mikakati yake ambayo iliweka kuhusu Ujerumani, kwani mipango yake ilikuwa ni kulituma jeshi la kijerumani, na kuisimamisha jamuhuri ya kijerumani ya magharib, na baadaye mpango wake ukawa ni

kudhoofisha Ujerumani ya magharibi na kuleta muungano baina yake na Ujerumani mashariki, na kuiwekea Ujerumani mipaka ya silaha, kisha katika mwaka 1990 miladi ikaiunganisha ili kuleta dola la kiuropa iliona nguvu itakao shindana na Ufaransa na Uingereza, na ili ishindane nazo katika uongozi wa muungano wa Uropa, na kwa hilo ikadhoofika uwezekano wa kuunganisha uropa kama nguvu moja.

Vile vile mpango ambao Amerika iliouweka wa Uchina baada ya kuona kuisaidia na kuifanya kuwa ni mchezaji wa kiulimwengu, na kutengeneza mahusiano pamoja naye, na vile vile kutengeza mahusiano ya Uchina na Japan na ili nifanye kuwa ni nguzo miongoni mwa nguzo za nidhamu za kimataifa, na hilo kupitia kuidhoofisha msimamo wa muungano wa kisovieti wa kiulimwengu wakati huo, na ili kuzidisha mwanya baina washirika waiwili wa kikomunisti maadui Amerika ikarudi baada ya hayo, baada ya kumaliza vita baridi ba kubadilisha mpango wake, na ikaonelea kuwa suala sasa lahitajia kuweka mpango wa kumkanyagia uchina na kumfunga ndani ya kuta zake kubwa, na ikafanya haraka kuweka mpango ili isije kuwa ni hatari kwa masilahi yake katika mashariki ya Asia, haswa kuwa uchina inamiliki viungo vitakavyo muezesha kufikia hilo.

Na mfano wa kubaalisha mbinu ni kama alivyofanya Amerika katika nchi za ulimwengu wa Kiislamu, kwani baada ya kuwa ilikuwa inategemea mapinduzi ya kijeshi ili wafikisha vibaraka wake katika utwala na misaada ya kiuchumi kama madeni na yale yaliokuwa yanaitwa mipango ya maendeleo kama wajuzi na mengineo, na kwa yale yalioitwa vitutio na vitishio au fimbo na karoti, saa hii imekuwa inategemea masuluhisho ya kijeshi na

vitisho, na imerudi katika kutegemea ushirikiano na makmbi ya kijeshi baada ya kuwa imeachana nayo, na ndiyo yaliorudisha mabangoni zama za ukooni wa kijeshi ubeberu wa kiamgharibi.
Na Uingereza imeshabadilisha mbinu zake kuachana namikataba na kambi za kijeshi na kutegemea viongozi vibaraka na mikataba ya kiuchumi na mikataba ya silaha, na inavyoonekana ni kuwa inajribu kambi za kijeshi kama mbinu mpya ya kale.
Haya ni maelezo ya mikakati na mbinu za kisiasa, hivyo basi ni wajibu juu ya Waislamu wajue kihakika kuwa kambi ya kimagharibi haibadilishi fikra yake ya kisiasa wala Twarika yake na kuweka mikakati mingine na kufuata mbinu mpya ili aweze kueneza mfumo wake. Na iwapo itavunjwa mbinu zake na kuharibiwa mipango yake yataharibika malengo yake ambayo kwao amekweka mipango mbnu hizo, hivyo basi mapambano ya kisiasa ni lazima yaelekezwe kwa mipango na mbinu katika kuikasifu na kupambana nayo katika wakati ambao ataelekea kupambana na fikra ya kisiasa, na Twarika yake, kwa hivyo ni lazima juu ya Waislamu wajue mipango iliowekwa ya kila nchi na kutambua mbinu zake.

## <u>MSIMAMO WA KIMATAIFA</u>

Ufahamu wa msimamo wa kiulimwengu unatofautiana na ufahamu wa siasa yakila nchi, na hili ni kwa ufahamu wa siasa za nchi zilizoona athari inahusiana na uufahamu wa fikra na Twarika ambazo husimama juu yake na siasa ya nchi hiyo kama tulivyo elezea hapo mwanzo. Ama msimamo wa kimataifa, ambao ndiyo hekalu la mahusiano ya kiulimwengu uliona athari yaani hali ambayo inavyokuwa juu yake nchi ya kwanza na nchi

ambazo zinazo shindana nayo, msimamo hu hauhusiani na fikra wala Twarika mashindan na mahusiano ya kiulimwengu, na mashindano ya daima kati ya nchi ilioko katika nafasi ya kwanza, na katika kuathiri siasa za kiulimwengu, hivyo basi hamna budi kufahamu msimamo wa kiulimwengu.

Ispokuwa inapasa ieleweke kuwa msimamo wa kiulimwengu haubaki katika hali moja, bali hugeuka na kubadilika katika ulimwengu kulingania na hali zake na matukio yake, laikini pamoja na hayo inawezekana kuichora picha yake wazi na inawezekana kupeana msingi mipana kuhusiana nayo au kuelezea vidokezo vyake ni maelezo wa waqia ambao umeshudhudia kitambo au ni ule unaonekanawa sasa, au unaotarajiwa kutokea, lakini pamoja na hayo huzingatiwa kuwa ni jambo thabiti, hivyo basi ni wajibu juu ya mwanasiasa kuwa na maelezio kuhusu msimamo wa kiulimwengu na kuhusu siasa za kiulimwengu, na ayafungamanishe kwa yale anaoyaona ili aweze kuwa na bayana na mambo na kuitolea hukmu juu yake.

Na kufahamu msimamo wa kiulimwengu, inawalazimu Waislamu kuwa na maarifa ya dola nambari moja katika ulimwengu na nafasi za nchi nyengine kuhusiana nayo, na kuhusiana na siasa za kiulimwengu, na inawalazimu kujua dola zinazofuata na dola ambazo zipo katika sayari na dola huru.

Ama dola zinazofuata ni dola ambazo zimefungika na dola nyengine katika siasa zake za kigeni na katika masuala mengine ya kindani, kwa mfano Misri pamoja na Amerika, na Kazakhstan (sasa) pamoja na Urusi. Ama dola ambazo zipo katika sayari ni dola ambazo zimefungika siasa zake za kigeni na dola nyengine lakini

mfungamano wa kiamslahi na wala mafungamano wa kufuata, kwa mfano Japani pamoja na Amerika na Australia pamoja Amerika na Uingereza, na Canada pamoja na Amerika na Uingereza na Ufaansa. Na Uturuki (sasa) pamoja na Uingereza na Amerika. Ama dola huru ni dola ambayo utekelezaji wa siasa zake za kigeni na za kindani hufanya vile inavyotaka kulingania na maslahi yake mfano Ufaransa na Uchina na Urusi.

Na pia hali ambazo haziingii chini ya siasa za kiulimwengu, bali ni matukio yaliotokea kutokamana na kuondoka kwa dola ya kikoloni kayika nchi. Hivyo basi hali hizi na mifano yake hazifanyi utafaiti katika siasa za kiulimwengu, na wala hazitolewe kuhusiana nazo misingi mipana, bali kila hali husomwa kwa waqia wake na kupewa hukmu yake. Kwa mfano Iraq baada ya muingereza kutoka humo na kutokea kwa mapinduzi 14 Julai 1958 mjiladi na kubatilishwa kwa mikataba yote na mafungamano, nchi ikawa ni huru kiulimwengu, mfano wake ni mfano wa Ufaransa wa Uingereza na nchi yoyote ile huru, lakini kwa kuwa mtawala wake wakati huo alikuwa ni kibaraka cha Amerika, ndiposa iraq katika waqia wake ikawa ni nchi inaofuta Amerika. Japo katika upande wa kiulimwengu ni huru, lakini pindi yalipotokeza mapinduzi 17 Julai 1968 na akaja mtawala kibaraka cha muingereza na nchi ikawa inafuata Uingereza.

Na hali Kadhalika hivyo basi pindi nchi huru inapokuwa mtawala wake ni kibaraka au anaiendesha serikali ni kibaraka basi nchi inakuwa inafuata nchi ambayo huzingatiwa kiongozi wake ni kibaraka wake.

Na hivi ndivyo nchi zote ambazo zilizokoloniwa hukumbwa na hali hizi, na hutoka katika mikono moja

hadi mikono mengine kwa kubadilishwa viongozi. Na mfano wa nchi hizi kwa upande wa kiulimwengu kidhahiri ni huru. Lakini kiuhakika inafuata, lakini hali hizi moja moja na hutokamana na kukomboa koloni kutoka kwa mkoloni, na majaribio ya dola za kikoloni kurudia katika koloni, au majaribio ya dola nyengine kutoka kuchukua nafasi ya mkooni katika nchi ambayo mkoloni mmoja ametoka, yaani katika koloni.
Lile ambalo ni lazima kulifahamu ni nafasi ya nchi yakwanza katika ulimwengu, kutokamana na umuhimu katika kufahamu siasa za kiulimwengu na katika kufahamu msimao wa kiulimwengu. Kwani katika amani dola ya kwanza huzingatiwa katika msimamo wa kiulimwengu ndio yeye kauli kiulimwengu, na itajilinganisha katika hilo baada ya hapo nchi ya pili na nchi yoyote nyengine kwa upande wa uwezo wake wa kuathiri kiulimwengu kisiasa.
Na kuathiri nchi nyengine huwa kwa nchi ambayo ina uzito katika kuathiri nchi ya kwanza, na kuathiri huku hutofautiana kwa tofauti ya nchi katika nguvu/uwezo wa kujitegemea, na nguvu za kiulimwengu. Hivyo basi kwa kadri ya nguvu za nchi na upeo wa uzito wake kiulimwengu, itakuwa ni kiasi kile ambacho inao katika kuathiri nchi ya kwanza, pia kuathiri siasa za kiulimwengu kwa upande wa kimataifa.
Na mfano wazi zaidi leo wa kuathiri nchi ya kwanza na baadaye kuathiri siasa za kiulimwengu ni mfano wa Uingereza siku hizi (2004 miladi) kwani kuathiri kwake katika siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa imetokamana na itibari yake yakuendela katika koloni zake za kale. Na vile vile Ufaransa na Urusi na Ujerumani, kwani zilishirikiana pamoja baada ya vya Amerika,

Uingereza dhidi ya Iraq na kuleta aina ya athari kwa dola ya kwanza na vile vile kuathiri siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa.
Ama nchi ambzao haziathiri dola ya kwanza na vile vile zisiszo na atahri huru katika siasa za kiulimwengu zikiwemo: - nchi zinazofuata, hizi haziwezi kuw na atahri juu ya nchi inaofuata. Na vile vile nchi ambayo ipo katika sayari, kwani kuathiri kwake inategemea kutoka kwa nchi kubwa ambayo inazunguka katikasayari yake.
Ama nchi zilizosalia zisizo futata na zile ambazo zisizo katika sayari nazo ni nchi huru kama Uswizi na Uhispania na Uholanzi na Italia na Uswidi, kwa mfano huwez akuathiri katika siasa za kiulimwengu katika upande wa kimataifa, iwapo zitalinda masilahi ya nchi ya kwanza au kutishia, na mfano wa hayo, Italia na Uhispania kulinda masilahi muhimu miongioni mwa masilahi ya Amerika, nahili ni kwa njia ya usaidizi wao kwa Amerika katikak uikoloni Iraq mwaka 2003 miladi.
Na kwa sababu hiyo ni wajibu juu ya nchi yoyote inataka kuathiri katika siasaza kiulimwengu na kuuburuta kwa mujibu wamasilahi yake kufua moja katika njia mbili: ima kutishia masilahi ya kihakika ya nchi ya kwanza katika msimamo wa kimataifa utishio wa kivitendo, au kulinda masilahi ya nchi yakwanza kwa njia ya kutaridhilia kwa ajili ya masilahi yake.
Na njia ya kutishia ya kihakika iliona athiri ndio njia iliona matunda bila shaka, na ndio ambayo inaofaa kwa nchi sahihi ambayo inaolenga kuadhamini kuathiri na kusikiwa sauti yake katika msimamo wa kimataifa. Ama njia ya pili ambayo hulengwa katika kuifuata kwake ya kulina masilahi hiyo ni njia ya dhulma na wala haiaminiki, kwani huenda ikafikisha katika lengo na

huenda ikapelekea katika maangamivu, hivyo basi ni kucheza kamari na muundo wa Ummah na ni kamari ya kijinga na hatima ya dola, kwa sababu kulinda masilahi ya nchi kuu kwa upande wa nchi yoyote, haitanyima kuridhia maslahi hayo pamoja na nchi yoyote ilio chini yake kwa hadhi na uwezo.

Kwani katika mwaka 2003 miladi Amerika ilifanya maridhiano na marafiki wake wa kale katika nchi za Uropa ya magharibi, baada ya kuisifu kuwa ni uropa ya kale, na ikaanza Kutafuta katika nchi za mashariki ya Uropa ili kuweka badali yao katika kumsuhubu yeye katika suala la Iraq, na ilimuaga dhidi ya Uingereza pale ilipojaribu kumzuia kusonga mbele katika kuivamia Iraq pasina kurudia umoja wa mataifa oili ichukuwe Sheria ya kimataifa kwao, na akasema Ramsfield waziri wa ulinzi wa kiamerika (Amerika inaweza kwenda Iraq bila ya Uingereza)

Na katikakutishia masilahi na kuleta athari ya kivitendo ni lazima nchi iwe na uwezo wa kujihami na sababu za usimamizi kamili wa kindani. Na njia sahihi ya hilo iwe inasonga mbele na kunyanyuka, yaani ni lazima iwe na mfumo, na inabeba ujumbe ulimwengu, na ianze kwa majirani wake, na ili iweze kujihami na kuingiliwa na mambo ya kindani na wala isitosheke na kuihami mipaka yake bali iapnua kwa mfumo wake na itibari yake ili iweze kushindana na dola ya kwanza katika msimamo wa kimataifa.

Na ili iweze nchi yoyote kuitingisha nchi ya kwanza katika kiti chake rasmi, basi ni juu yake igeuze upepo wa kisiasa katika upande wake na ivutie nchi nyengine katika siasa zake na fikra zake, kama ilivyofanya Yjerumani kabla ya vita vya pili vya dunia, na wakati nchi yoyote

itakapoweza kufanya hilo basi msimamo w akimataifa utakuwa unayumbayumba nafasi ya nchi ya kwanza , na mara nyingi haliwezi kupatikanwa hilo isipokuwa vitakapotokeza vita na msimamo utabalika, view ni vya kiulimwengu jumla au vifungike kivipande, au iwapo hatari ya vita ipo dhidi ya dola ya kwanza n suala linalotarajiwa, na inahitajia katika vita hivi nchi zitakazo shiriki katika kambi yake.
Na suala la nchi ya kwanza katika ulimwengu sio jipya kwani lipo tangu zamani. Kwani Misri katika historia ya kale ilikuwa ni dola ya kwanza na Ashur katika Iraq ilikuwa inashindana nayo katika nafasi hiyo. Na dola ya Warumi ilikuwa ni dola ya kuanza na dola ya kifursi ilikuwa inashindana nayo juu ya nafasi hiyo. Na dola ya Kiislamu tangu zama za makhalifa wema hadi vita vya kimsalaba ilikuwa ni dola ya kwanza na wala haikuwa na kushindana naye katika nafasi hiyo. Na Ufaransa ilikuwa ni dola ya kwanza na Uingereza ilikuwa inashindana nafasi hiyo. Na dola yakiuthmai kwa sifa yake ya dola ya Khilafa ya Kiislamu, ilikuwa ni dola ya kwanza kwa muda unaokaribia karne tau, na wala haikuwa na mshindani wa nafasi hiyo hadi katika nusu ya karne ya kumi na nane miladi. Na kabla ya vita vya dunia vya kwanza Ujerumani ilikuwa ni dola ya kwanza, na YUingereza na Ufaransa zilikuwa zinashindana nafasi hiyo. Na baada ya vita vya dunia vya kwanza Uingereza ilikuwa ni dola ya kwanza na Ufaransa ilikuwa inashindania nayo katika nafasi hiyo, hatimaye ikakaribia kuichukuwa afasi hiyo na vikasimama vita vya pili vya dunia, na Amerika ikashiriki katika vita, na vita vikamalizika na Amerika ikawa ndio dola ya kwanza katika kuchora siasa za kimataifa msimamo wa kimataifa,

kwani ilikuwa inauwezo zaidei katika madola katika kuzifanya siasa za kimataifa katika upande wake, na ikaendelea kutwala msimamo wa kimataifa, halitokei wala kutekelezwa ila mtukio ya kisiasa iliokuwa inataka. Na pamoja na hayo muungano wa usovieti wakati huo na Uingereza na Ufaransa zinajaribu kushindana nayo na ilikuwa inashiriki kuathiri katika siasa za kiulimwengu kwa kiasi fulani kwa mujibu wa nguvu za dola hizi, na haswa muungano wa usovieti kwa sura ya nguvu, kisha Uingereza kwa sura dhaifu.

Ama muungano wa usovieti ilifaulu kusimamia ubavuni mwa Amerika ililegea na kurudi nyuma, na ikaendelea kushuka chini na chini zaidi, hadi ikafika hivi ilivyo leo. Na maelezo kuhusiana na hayo ni kuwa Uingereza baada vita vy apili vya dunia, ilikuwa inaaznza kunyanyuka kutokamana na kipigo cha vita, na ikawa inajaribu kutingisha Amerika katika nafasi yake ya kwanza na ikawa inafanya mipango ya kisiasa ili kuiathiri Amerika, hivyo basi haikushiriki katika vita vya Korea isipkuwa ushurikiano wa mambo na ilikuw ainaopelekea habari za Amerika za kivita hadi Uchina, na Uchina ndio ambayo iliokuwa kihakika inaopigana na Korea, na Uingereza kwa mbinu zake za kisiri chafu ikaweza kuathiri nafasi ya Amerika kimataifa katika vita vya Korea, na ikatingisha nafasi yake. Na katika mkutano wa Geneva ambao uliowekwa kwa ajili ya India Uchina iliosimama upande wa mashariki, na ukamalizika kwa maazimio yalio na masilahi kwa upande wa mashariki. Pipa ilikuwa inampelekea Urusi habari za Amerika za kiujasusi na za kijeshi, na miongoni mwake ni ile iliompelekea ursi kuhusu ndege (U2) na kupelekea kuangushwa kwake. Kisha msimamo wa Macmillan katika mkutano wa Paris

kusimamia upande wa Khrushevedhidi ya Eisenhower na kujaribu kumdhalilisha Eisenhower kwa sifa yake ya raisi wa Amerika, na kupelekea kutofaulu kwa mkutano na kudhoofisha nafasi ya Amerika. Na hivi ndivyo ilivyokuwa inafanya mambo mengi ili kuipiga Amerika na majaribio ya kuathiri nafasi ya nchi ya kwanza. Lakini Amerika ilitambua yote hayo. Baadaye katika mkutano wa Khrushchev na Kennedy katika Vienne, na tangu tarehe hiyio Uingereza ikawacha kuihujumu Amerika na kuchukua msimamo wa kujihami na hapo Urusi (muungano wa Usovieti) na Amerika zikaanza pamoja kuiondosha Uingereza katika dunia.

Muungano wa usiovieti ilikuwa inawasha moto wa vita baridi dhidi ya kamb ya kimagharibi, na haswa Amerika kwa kiasi kikubwa, kwani ilikuwa inajaribu kuchukuwa hatamu za uongozi kutoa kwa kambi ya kimagharibi, na ilikuwa inafanya vitendo ili kumuondosha Amerika katika nafasi ya dola ya kwanza ili yeye awe ndio dola ya kwanza katika dunia, na iliweza k ufaulu kwa vitendo ngome yake kuu, nao ni umoja wa mataifa, katika kuitatua matatizo ya kimataifa na kuifanya iweke mikutano nje ya umoja wa mataifa, na huku inamshajiisha Uingereza kutingisha Amerika kwa ajili ya kudhoofisha nafasiya nchi ya kwanza, na kuzidi kupanua mwanya wa utesi kwa ajjili ya kudhoofisha nafasi ya dola kwanza, na ikapanua mwanya wa utesi baina ya Ufaransa na Amerika, na ikachangia mno kati vitendo vya kimataifa. Pamoja na hayo ikatangulia katika nyanja ya anga hatimaye ikamshinda Amerika, na ikaendelea katika silaha za nuclear na katika makombora zinazopita bara, na ikaweka kambi yake ya kijeshi katika Cuba ili kumtishia Amerika, na ikakashifu mbinu nyingi za

Amerika katika Congo na Misri na Algeria na kwengineko. Isipokuwa yote hayo, japo iliathirika Amerika kiasi kikubwa lakini haikuweza kumuondosha katika nafasi ya nchi ya kwanza, bali ilikuwa ni ushindi wa kivipande katika masuala fulani ya kisiasaz akimataifa, japo muungano wa usovieti haikuwacha kuihujumu Amerika kwa mbinu za vita baridi, hadi ukafanywa mkutano wa Khurshchev na Kennedy mwaka 1961 miladi, walikutana katika mwezi wa Juni mwaka huo katika Vienna mji mkuu wa Austria, na wakakubaliana waugawanye ulimwengu baina yao. Na baada ya tarehe hiyo Uingereza na Ufaransa zote hizo zikaanguka katika siasa za kiulimwengu, na muungano wa Usovieti na Amerika zikawa ndizo pekee katika kuchora siasa hizi. Na hayakufaulu majaribio yote ambayo iliofanya Uingereza ili iwe na rai katika siasa za kiulimwengu, na Ufaransa vile vile pia haikufaulu hata katika masiku ya De Gall kupiga angalau hatua moja katika kuleta uwezekano wowote upande wake katika kuchangia katika siasa za kiulimwengu, na hali ikaendelea hivyo hadi mwaka 1989 miladi, wakati ukuta wa Berlin ulipoangushwa, na ikavunjika muungano wa Sovieti baada ya miaka miwili kwa sura rasmi na vikamalizika vita baridi, na Urusi ikarithi rasmi mahala pa muungano wa usovieti katika mwanzo wa miongo ya tisiani katika karne iliopita, lakini iliangushwa katika nafasi ya pili katika siasa za kiulimwengu, na ikachipuka hali mpya ya kimataifa na Amerika ikawa kwa mara ya kwanza pasina mshirika wa kimataifa, na ulimwengu ukaingia katika hali ya kimataifa ambayo haijwahi, Amerika ikajaribu katika mwisho wa zama za Bush baba kuchora siasa za kiulimwengu kipekee, na akaiita kwa

jina la nidhamu hii haikuandikiwa kufaulu, na mwito huo ukabakia ni yenye utata, vile vile hali ya kimataifa kubakia ni yenye uwingi, hadi alipokuja Clinton katika kiti cha utwala katika mwaka 1992, miladi a akaweka nidhamu mpya ya kimataifa ambayo haitegemea upweke, bali inategemea utwazi na idara ya Clinton ikaanza kuweka misingi ya nidhamu hii mpya, ambayo miongoni mwa nguzo yake muhimu ilikuwa ni kuweka siasa za ushirikiano pamoja na madola mengine makubwa ambazo zilionekanwa katika kuitatua matatizo ya Balkan katika Bosnia na Herzegovina na Kosovo, vile vile kufaulu katika kuharibu silaha za nuclear katika Ukraine na Byelorussia kwa maelewano na Urusi, na pia kuweka kwa sahihi mkataba wa uwiano baina ya Amerika na madola ambayo yalikuwa ni hapo awali ni sehemu ya nidhamu ya mashariki, na wakashiriki kuweka sahihi mkataba huu wa uwiano Uingereza na Ujerumani, na Amerika katika kipindi hiki iliweza pia kupitia siasa ya ushirikiano, kupanua muungano wa Atlantic kaskazini (Nato) kwa kushirikiana pamoja na dola za magharibi ya Uropa, na zikafaidika dola z amuungano wa Uropa kwa upanuzi huu, na upanuzi huu ukatimia kw hisabu ya Urusi, na kwa hisabu na itibari yake.

Na kikatofautika kipindi hiki kwa kuzidi nguvu za Ujerumani, na udhaifu ukaingia katika muungano wa kisovieti, na kuangushwa kwa ukuta wa Berlin, na kuondoshwa kwa msaada wa Ujerumani ya mashariki, liakaandama kuunganishwa kwa Ujerumani mashariki pamoja na Ujerumani ya magharibi kwa haraka sana, na ikawa ni nguvu kubwa kabisa kiuchumi katika Uropa, na ili ibadilike kuwa ni nguvu za kisiasa za kivitendo na yenye athari itakaokaribia Amerika na Uropa, mwishowe

mazungumzo yakawa ni Ujerumani kuingia katika klabu ya nchi zenye uwanachama wa daima katika baraza la usalama ni suala la kuzungimziwa na Amerika na Uropa a kiulimwengu.

Na hali hii mpya ya kisiasa iliandamana na hali mpya ya kiuchumi, pale ilipoamilishwa siasa za soko kwa kiasi kikubwa, na hili likadhihirika katika siasa ya utandawazi ambayo ilijilazimisha yenyewe juu ya dunia, hivyo basi mashirika yakaungana na kuwa makubwa, na ikajitokeza kama mchezaji mkuu wa kiuchumi huko inalazimisha siasa zake juu ya madola, na mashirika ya nchi nyingi yakawa ndio mazungumzo ya wanauchumi na maafikiano ya Gatt yakabuniwa katika mwaka 1995 miladi hadi kuwa ni chama cha biashara cha kimataifa kitakachokilinda siasa za utandaazi kwa sitara ya kanuni, vile vile iliamilishwa sanduku la fedha la kiulimwengu (IMF) na benki ya kiuliwemngu (World Bank) hapo haya matatu nayo ni chama cha biashara cha ulimwengu (WTO) na sanduku la fedha (IMF) na benki ya kiulimwengu (World Bank) yakawa yanatumiwa na madola makuu kama chombo cha kuingia na kulazimisha siasa za dola za kiuchumi na walikiri wote hayo akiwemo Lawrence Eagleburger aliyekuwa waziri wa kigeni wa Amerika na Michael Kamdiso aliyekuwa rasi wa sanduku la fedha la kiulimwengu walikiri kuwa walitumia IMF katika kuiangusha nidhamu ya Suherto kupitia kulazimisha siasa ya upataji wa fedha, na kumnyima mikopo iwapo hatakubali siasa hiyo, hivyo basi akalazimika kukubali matakwa, na akafanya upataji wa fedha na kwao akaangushwa.

Vile vile iuliamilishwa dori ya G7 nayo ni madola saba ya kiviwanda na ikijumlishwa Urusi, na hivi ndivyo

zilitawala madola haya manane nazo ;: Amerika na Japa, Ujerumani na Uingereza na Ufaransa na Italia na Canada na Urusi, madola haya yalitawala siasa za kiulimwengu za kiuchumi na za kifedha, na tukiongezea nchi ya uchina juu ya kiuchumi ulio nayo na kwa nguvu za nuclear inayomiliki, na uzito wa wakaazi wa kiti cha kudumu katika baraza la usalama, iwapo tutaongeza uchina wa nguvu hizi, inazozimilki basi twaweza kusema ni zaidi, hakika madola makubwa katika dunia leo ni hizi nchi tisa, lakini utofauti wa nguvu wa hizi zinatufanya tuondoshe mbili miongioni mwake nazo ni Italia na Canada kwani hazimiliki nguvu zozote za kisiasa au za Anasema Hoper Vidrin aliekuwa waziri wa kigeni wa ufaransa katika kitabu chake "ahani za Ufaransa katika zama za utendawazi" Hakika nguvu hii ya kipekee (Amerika) ambayo intawala kila nyanja ya kiuchumi na teknolojia na kijeshi na kifedha na kilugha na kithaqafa ipo katika hali ambayo haijafikiwa katika historia" kulingania na maelezo yake.

Baadaye Vidrin anaweka sifa haswa za nchi zenye nguvu na itibari kwa kusema "Amerika inashikilia nafasi ya kwanza katika ulimwengu pasina mpinzani, na zinakuja baada yake katika nafasi ya pili nchi saba zenye itibari ya kiulimwengu nazo" Ufaransa na Uingereza na Ujerumani na Ursui na Uchina na Japan na India kwa sharti ya kuwa watapanua maoni yao ambayo bado ni ya kimaeneo" na anasema "Vipima vya sifa hizi ni nyingi ikiwemo pato la wakasi, kiwango cha teknolojia na silaha za nuclear kisha kiwango na aina ya silaha, na mfungamano na vyama na miundo ya kimataifa kama baraza la usalama na mjumuiko wa 8 au muungano wa kiuropa, kisha

umaarufu wa lugha na taathira ya kithaqafa iliyorithi kutoka kale"

Lakini kilicho wazi zaidi katika rai hii ya Vidrin ni kuwa baada nchi kubwa Amerika ambayo hajakaribiwa na dola yoyote katika mwanzo wa karne ya ishirini na moja, zinakuja nchi tatu kubwa kihakika nazo ni Urusi na Uingereza na Ufaransa, kisha baada ya hizi tatu inakuja Ujerumani, na nchi hizi nne zina malengo yake kimataifa katika sehemu nyingi za dunia. Kisha Uchina nayo ni nchi kubwa katika mipaka ya mizungugio yake ya kimaeneo, na kama sio kukandamiza kwa juhudi zake za kimataifa basi ingeshindana na zote au baadhi ya nchi nne zilizotangulia. Ama Japan ni dola kubwa baada ya Amerika kiuchumi. Hivyo basi mpangilio wa nguvu za nchi ni kama ifuatavyo: Amerika, Urusi, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uchina, Japan kwa kufuatana na yamkinika kuitwa nchi hizi saba nchi kuu, ama India na Canada na Italia hazistahiki kuitwa nchi kuu, pamoja na kwa ndizo zinazofuata hizi saba, na pamoja nazo zinakuwa nchi kumi za mwanzo katika ulimwengu.

Na kumalizika karne ya ishirini na kuanza elfu ya tatu ya miladi, idara ya George Bush mtoto iligeuza misingi ya nmchezo, ndiposa ikawacha siasa za ushirikiano ambayo ilianzishwa na Clinton, na ikaanza kulazimisha nchi kubwa siasa zake kwa njia ya kulazimisha na ikajiondosha katika mikataba kadhaa ya kimataifa mfano makubaliano ya Kyotona mahakama ya jinai ya kimataifa na makubaliano ya Salt ya kupunguza uenezaji wa silaha za kibalistiki, na mengineo na ikachafua mahusiano kati yake na nchi kuu zaidi na zaidi kwa kutokwa kwa tukio la 11/Septemba/2001 milai, kwa kulipuliwa kwa makao makuu ya biashara ya kiulimwengu katika New York na

jengo la Pentagon katika Washington, na hilo likapatia misukumo mpya wa mwelekeo wa upweke na kutokamana na mlipuko hayo ikapata kisingizio cha kupigana kke kilichoiitwa ugaidi, na ikakoloni Afghanistan na Iraq chini ya kisingizio hichi, na ikadhihirika kiburi cha siasa za idara ya kiamerika na ikabeba siasa imma pamoja na sisi au dhidi yetu na siasa hizi mpya iliwa wauropa na wengineo wa kikundi kitendo kwa hasira, na kuituhumu na ufinyo nma ukosefu wa busarta, na wakawataka wamerika kurudi katika mashauriano na ushirikiano, lakini wamerika wakakataa kurudia misingi ya ushirikiano na mashauriano ambayo iliofuatwa na Clinton, na wakawaweza wanaojiita wahifadhi wapya chini ya uongozi wa Dick Chenny makamu wa raisi, na Ramsfield waziri wa ulinzi wa Wolfwetz naibu wake, na Richard Nearl raisi wa baraza la siasa za ulinzi na Douglas Faith na John Bolton na Condoleza Rice na wengine, hawa waliweza kuathiri uamuzi wa Bush, na walutumia kila uwezo wao na itibari zao na mashirika yanaowasaidia, ili kuitunukia siasa hiyo.
Na katika yaliochipuka zaidi katika siasa hizi ni kutoirudilia umoja wa mataifa na Sheria zake katika kufanya uamuzi, na masilahi ya kiamerika yakapewa umbele, na iwapo masilahi yao yatagongana na Sheria za kimataifa basi Sheria za kimataifa zitapuuzwa, na iwapo hazitagongana basio zitaamilishwa, na ikaamiliana hivyo na baraza la usalama, iwapo itafaulu katika kuitolesha maazimio kutoka kwa baraza la usalama basui ni sawa na iwapo sivyo basi itaipuza na kuachana nayo.
Na Uropa ikiwakilishwa na Uingereza ikajaribu kuisisitiza idara ya Amerika kurudia Sheria za kimataifa, na akayatangulia majaribio hayo waziri wa mambo ya kigeni

Collin Powell na raisi Bush akavutiwa nayo, lakini kikundi cha wahifadhi wapya waliyabwaga majaribio hayo, na Amerika ikaendelea kupuuza siasa za ushirikiano, vile vile ikapuuza kuipatia dori ya kivitendo chama cha kimataifa.
Pamoja na ahyo idara ya Bush mtoto haikuweza kuangusha dola kubwa, kama Uingereza na Urusi na Ufaransa na Ujerumani kucheza dori ya katika siasa za kimataifa bali siasa ilioanzashwa na iara ya Bush mtoto umetilia nguvu msimamo wa nchi hizi na wala haikudhoofisha kwa sababu ilikimbilia kuungana nazo ili kujihamii mbele ya hujuma ya mbaya juu ya Amerika, na kuungana mwimo wa Ufaransa, Ujerumani, Urusi na miimo hii ikasaidiana na Uingereza kwa siri, na nchi hizi na Ujerumani zikaweza kupambana na kusimamia wima katika msimamo yao kama nchi kuu kivitendo kiasi fulani katika siasa za kimataifa.

## DESTURI YA KIMATAIFA NA KANUNI YA KIMATAIFA

Ilikuwa kushindania kituo cha serikali ya kwanza katika zama zilopita hakudhihirishi matendo ya kisiasa yaliofungamana na kanuni ya kimataifa. Kwasaba ya kutokuweko kwake,bali kulikuwa hudhihirika matendo ya kijeshi kwa vita,mapigano na kupunguza vipande vya serikali tangu mwanzo wa tarekh.Hali ikaendelea hivyo hadi katikati mwa karne ya kumi na nane ilipopanuka kanuni ya kimataifa au kwa usahihi zaidi ikapatikana kwa muundo wa kanuni na kuweka sharia.Tangu wakati huo vikaanza vitendo vya kisiasa vikichukuwa sehemu

muhimu katika mahusiano ya kimataifa,katika kutatua matatizo ya kimataifa. Vikawa vitendo vya kisiasa vyachukuwa mahali pa vitendo vya kijeshi katika kutatuwa matatizo,kusitisha kudhibitikwa serikali ya kwanza na kushindania kituo chake.Tangu hapo ikazidi kuhukumu kanuni ya kimataifa katika mahusiano ya kimataifa na kuzidi kufanya vitendo vya kisiasa ni chombo cha kutatuwa matatizo imma peke yake au kiupande wa vita na mapigano.Likamakinika hilo kwa kiwazi baada ya 1919 M,ilipobuniwa umoja wa mataifa,ikazidi kuhukumiana kwa kanuni ya kimataifa na desturi ya kimataifa.Vitendo vya kisiasa inavyotekeleza serikali kwa sura jumla,serikali zinazoshindana na serikali na serikali ya kwanzana serikali ya kwanza yenyewe haswa.Hakika wanategezea kile kinachoitwa desturi ya kimataifa au kanuni ya kimataifa.Basi hapana budi kutupia jicho la haraka desturi ya kimataifa na kanuni ya kimataifa,ili kudiriki uhakika wa siasa na namna ya kutekeleza vitendo vya kisiasa upande wa kimataifa.

Amma desturi ya kimataifa nayo ipo tangu zama za kuwepo serikali,tawalana miundo,nayo ni mkusanyiko wa misingi iliojitokeza kwa ajili ya mhusiano baina ya mahusiano wa wanadamu katika hali ya kivita na hali ya usalama.Ikawa kwa ajili kufuatwa na mkusanyiko kuna muda mrefu,desturi za kimataifa kisha ikamakinika mkusanyiko huu wa misingi mbele ya serikali,zikawa serikali zajichukulia ni zenye kushikamana na desturi hizi mshikamano wa kujitolea,ikawa imefanana na kanuni.Kushikamana huku ni kushikamana kwa kimaana wala si kushikamana kwa kimada.Ikawa mkusanyiko wa wanadamu wafuata kwa kujitolea na kwa kuogopa rai jumla na asie fuata amejiingiza katika hatarikya rai jumla

na kuaibishwa kwa hilo.Huzingatiwa katika aina hii,yaani sampuli ya desturi ya kimataifa,masikizano ya waarabu kabla ya uislamu ya kuzuiya mapigano katika mwezi mitukufu.Kwa hilo ni kwamba maqureshi walisimamisha kumpinga Mtume (s.a.w) pindi kiliposimama kikosi cha Abdillah bin Jahshi na kumuuwa Amru bin al-Hadhramy,akateka watu wawili wa kiqureshi na kuchukuwa msafara wa biashara,wakasimama maqureshi kupinga hilo.Wakanadi kila mahali kwamba Muhammad na maswahaba zake wamehalalisha,wakamwaga damu,wakachukuwa mali na kuteka watu wawili,basi ikaandaa rai jumla kwake kwakuwa amehali fudesturi za kimataira.

Hivi ndiyo ilivyokuwa baina ya mikusanyika ya wanadamu misingi iliozoeleka wakiifuata katika vita na usalama,wakiwemo mitume au wanaoitwa mabalozi na zikiwemo ngawira za vita na mengineo.Isipokuwa desturi hizi kuna zile ambazo ni jumla wakifata jumla ya mikusanyiko ya wanadamu mfano mabalozi ya wajumbe, nyengine ni haswa kwa mkusanyiko maalum.Ikawa desturi hii yaendelea kulingana na haja za serikali,tawala na miundo yaani kulingana na haja ya mikusanyiko ya binadamu katika mahusiano yao na wengine kama mikusanyiko. Ikawa desturi hizi za kimataifa wakihukumiana nazo watu rai jumla na kuaibishwa anaye halifu.Yakawa yafuata kwa kujitolea na kwa hiari kwa kuathirika kimaana na jengine na hakukuweko na nguvu ya kimada ikitabikishwa.Basi kwa kutegemezwa katika desturi hizi vikawa vya simama vitendo vya kisiasa kutoka kwa makundi ya wanadamu.

Amma kinachoitwa kanuni ya kimataifa hakika hii imetokea na kupatikana dhidi ya serikali ya kiislamu

iliokuwa ikiwakilishwa na serikali ya Kiuthmani.Hilo ni kwamba serikali ya Kiuthmani kwa sifa yake kuwa ni serikali ya kiisalamu, ikasimama kupiga vita Ulaya,ikawatangazia jihad Wanasara wa Ulaya na kuanza kufungua miji yao mji baada ya mji,ikashika ile inayoitwa Yunani,Romania, Albania,Yugoslavia,Hangari na Austria mpaka ikakomeamipaka ya Vienna.Ikatia hofu jumla ya Wanasara huko Ulaya,ikapatikana desturi jumla kwa Wanasara kwamba jeshi la waislamu halishindwi na kwamba waislamu wanapopigana hawajali mauti.Kwa itikadi yao kwamba wako na pepo wakiuwawa na kuitakidi kwao kadarna ajal.Waliona Wanasara ushujaa wa waislamu na ukali wa hamasa yao kilichowafanya wanakimbia wakiwaona,kilicho wasahilishia waislamu kufunguwa miji na kuifanya inyenyekee utwala wa kiislamu.Wakawa Wanasara wa Ulaya zama hizi ni tawala na falume,zikawa ni serikali zilizo tawanyika,kila serikali imegawanyika katika tawala ikitawaliwa kila moja wapo na bwana wa utawala akigawanya ufalme katika uongozi.Kilicho mfanya mfalme hawezi kulazimisha tawala hizi kupigana,wala hawezi kuzielezea mbele ya wapiganaji kwa kila kinachoitwa mambo ya nje.Hilo likasahilishia waislamu mapigano na ukombozi.Ikaendoelea hali ya serikali za Ulaya hivi hivi hadi zama za kati,yaani mwisho wa karni ya kumi ns sita.Katika karni ya kumi na sita,yaani zama za kati zikaanza serikali za Ulaya zakusanyika kuunda jamii moja inayoweza kusimama mbelel ya serikali ya kiislamu,likawa kanisa ndilo lenyekuwadhibiti na dini ya Kinasara ndio yenye kuwaunganisha.Kwahiyo zikawa zajaribu kuunda jamii ya kinasara kutoka kwa mkusanyiko wa serikali,wakaanza kuweka mahusiano

baina yao kukapatikana kutokana na hayo misingi waliokubaliana kupanga mahusiano na baadhi yao.Ikawa hilo ni mwanzo kupatikana lililo itwa baada yake kuwa ni kanuni ya kimataifa.Basi msingi uliopatikana kanuni ya kimataifa ni serikali za kinasara za Ulaya zilikusanyika kwa msingi wa fungamano la kinasara kwa ajili ya kusimama mbele ya serikali ya kiislamu.Basi hilo lakapelekea kupatikana kinachoitwa jamii ya serikali za kinasara,zawafikiana juu ya misingi baina yao nyengine ni usawa baina ya watu wa serikali hizi katika haki,nyengine ni kwamba serikali hizi ziko na mifumo ile ile na mifano ya pamoja na nyengine ni kwamba serikali hizi jumla zasalimu amri kwa Papa wa kikatholiki na utawala wa juu wa kiroho pamoja na kutofautiana madhehebu yao.Basi ikawa misingi hii ndio chanzo cha kanuni za kimataifa.Isipokuwa mkusanyiko wa serikali za kinasara mwanzoni haukuathiri,kwakuwa misingi walioafikiana haikuweza kuwaunganisha, kwakuwa nidhamu ya kifalume iliendelea kuwa kizuizi cha nguvu ya serikali na kuwamakinisha kujenga mahusiano.Ikawa kanisa kusaliti serikali imezifanya kuwa ni wafuasi katika wafuasi wa kanisa na zenye kunyakuwa ubwana wake na ukombozi wake.Kwahiyo ikapatikana mvutano ili washinde watawala wa falume,ukamalizika kwa kushindwa serikali na kuondoka nidhamu ya kifalume. Wakati huo huo ikatokezea mvutano baina ya serikali na kanisa uliopelekea kuondoshwa utawala wa kanisa katika mambo ya kindani nan je ya serikali.Baada ya kuwa kanisa ndio yenye kutawala,lakini ikaendelea serikali ya kinasara na kila kilichoko katika amri kwamba ilipanga mahusiano na serikali na kanisa kwa namna itakayo itahakikisha kujikomboa serikali.Hili lilipelekea

kupatikana serikali zenye nguvu Ulaya,lakini pamoja na hayo haikuweza kusimama mbele ya serikali ya kiislamu,ikaendelea hivyo mpaka katikati ya karni ya kumi na saba,yaani mwaka wa 1648 M.Katika mwaka huu ziliweka serikali za kinasara za Ulaya kongamano nalo ni Westphalia,katika kongamano hili kukawekwa misingi thabiti ya kupanga mahusiano baina ya serikali za kinasara za Ulaya na kupangwa jamii ya serikali za kinasara itakayopambana na serikali ya kiislamu.Basi liliweka kongamano misingi zinazofuatwa kwa kile kinachoitwa kanuni za kimataifa,lakini hazikuwa kanuni za kamataifa jumla bali zilikuwa ni kanuni za kimataifa za serikali za kinasara za Ulaya na si nyenginezo.Ikakatazwa serikali ya kiislamu kuingia katika jamii ya serikali au kuambatanishwa na kanuni za kimataifa.Tangu wakati huo kulipatikanwa kile kinachoitwa jamaa ya kimataifa,ikawa imebuniwa na serikali za kinasara za Ulaya,jumla bila ya kutafautisha,bila ya kutafautisha baina serikali za kifalume na serikali za jamhuri au baina ya serikali za kikatoliki na serikali za kiprotestanti.Ikawa imefungika katika serikali za magharibi mwa Ulaya mara ya kwanza,zikajiunga serikali nyengine za kinasara za Ulaya Kisha zikaenea serikali za kinasara zisizo kuwa za Ulaya lakini ikabakia ni haramu kwa serikali ya kiislamu hadi karni ya pili ya karni ya kumi na tisa,ilipokuwa serikali ya kiislamu katika hali ya udhaifu,ikaitwa mtu mgonjwa,hapo ikataka serikali ya kiuthmani kuingia katika jamii ya kimataifa ikakataliwa ombi lake,ikakazania sana,basi ikawekewa sharuti kali,miongoni mwazo ni kutohukumu na uislamu katika mahusiano yake ya kimataifa,kuingiza kanuni za kiulaya,ikakubali serikali ya kiuthmani kwa shuruti hizi na ikazinyenyekea.Baada ya

kukubaliwa kwake kujiondoa kuwa serikali ya kiislamu katika mahusiano ya kimataifa ikakubaliwa ombi lake,ikaingizwa katika jamii ya kimataifa mwaka wa 1857kisha baada ya hapo zikaingia jamii ya kimataifa serikali nyengine zisizokuwa za kinasara ka Japan.Kwahiyo huzingatiwa kongamano la Westphalia lililofanywa mwaka wa 1648 ndilo lililopanga misingi ya kufuata ya kanuni za kimataifa.Juu ya misingi yake hii vikapatikana vitendo vya kisiasa kwa sura tofauti na kupatikana vitendo vya kimataifa kipamoja.

Ikawa kubwa katika misingi hii ni fikra mbili hatari: Kwanza:**Fikra ya usawa wa kimataifa.**Pili:**Fikra ya makongamano ya kimataifa.**Amma fikra ya usawa wa kimataifa,nazo hupitisha kwamba ikijaribu mojawapo ya serikali kuzidi hisabu ya serikali nyengine,basi hakika serikali nyengine zitaungana kumzuia asizidi, kuhifadhi usawa wa kimataifa ambayo ni udhamini unaozuiya vita na kuenea uislamu.Amma fikra ya makongamani ya kimataifa,hakika kongamano labuniwa na serikali za Ulaya,hufungwa kutatuwa matatizo yao na mambo yao kulingana na maslahi ya Ulaya kisha ikaendelea fikra hii hadi makongamano ya kimataifa makubwa yanayofungwa kuangalia mambo ya ulinwengu kulingana na maslahi ya serikali hizi kubwa.Fikra hizi mbili zilikuwa ndio msingi wa yale yanayokumba ulimwengu katika ugumu unayo kutana nayo wanapoenua utawala wa serikali za kikoloni na serikali kubwa.

Mara ya mwanzo zilipotumika fikra hizi mbili ilikuwa ni masiku ya Napoleon,mwanzoni mwa karni ya kumi na tisa.Basi pindi yaliposimama mapinduzi ya kifaransa,kuenea fikra zilizo simama juu ya uhuru na

usawa na kutambua haki za watu binafsi na haki za raia yaliweza kubadilisha ramani ya Ulaya na kubuniwa serikali mpya na kumaliza serikaliza za zamani.Hapo zilikusanyika serikali za Ulaya kwa hoja ya usawa kushirikiana dhidi ya Ufaransa. Baada ya kushindwa Napoleon zikakusanyika serikali hizi katika kongamano la Viena mwaka wa 1815 M na kuangalia kurudisha usawa na kupanga mambo ya jamii ya serikali za kinasara,ukarudishwa ufalme Prussia na Austria,kusimamishwa muungano wa majimbo baina ya Sweden na Norway.Ikaunganisha Ubelgiji na Uholanzi iwe serikali moja itakayozuiya kupanuka kwa Ufaransa,ikawekwa katikati daima.Ili kutekeleza maamuzi ya kongamano hili zikaweka serikali zilizoshiriki katika kongamano muungano baina yao nao ni muungano baina ya wafalume na Urusi,Urusi na Austria kwa makubaliano ya mfalme wa Uingereza kisha ikajiunga Ufaransa,yaani muungano baina ya serikali kubwa ili kudhibiti serikali nyengine.Mwaka wa 1818 M uliwekwa mkataba wa Ex-Lashapell baina ya Urusi,Uingereza,Prussia,Austriana Ufaransa waliowafikiana serikali hizi kuingilia kisilaha ili kuzuiya harakati yoyote ya kimapenduzi ya inayotishia matokeo walio fikia kongamano wa Viena.Haya yalifanya serikali tano kubwa zenyewe kuwa na muundo utakao hifadhi usalama na kundi la serikali,yaani katika jamii ya kimataifa ya kinasara.Ukapanuka utawala wake ukakusanya baadhi ya miji ya kiislamu baada ya kudhoofika serikali ya kiuthmani.Zimetekeleza serikali hizi maingiliano kadhaa kwa hoja ya kuhifadhi amani,zikaingilia Napoli mwaka wa 1821 M,zikaingilia Isbania1827 M,Uremo mwaka wa 1826 M na Misri mwaka

wa 1840 M.Zimejaribu serikali hizi kubwa kuingilia Marekani,zikajaribu kusaidia Isbania kurudishiwa koloni zake Marekani lakini Marekani alikuwa imekuwa imekuwa serikali yenye nguvu ikiipigia hesabu ikazuia hilo,akatowa raisi wa Marekani James Monroe taarifa yake mashuhuri inayojulikana kama taarifa ya Monroe nayo ni mwaka wa 1823 M.Alisema: "Hakika Marekani hairuhusu serikali yoyote ya Ulaya kuingilia mambo ya bara la Marekani na kunyakuwa sehemu yake" zikawacha serikali hizi kuingilia.

Hii ndio asili ya kanuni ya kimataifa nayo ndio yalioleta visingizio vya kuingilia, kufanya serikali kubwa kuhukumiana na serikali ndogo,nacho ndicho kilicho tegemezewa matendo ya kisiasa wanayoyatekeleza serikali kukidhi maslahi yao au kushindana na serikali ya kwanza.Isipokuwa kanuni hizi za kimataifa zimetokezewa na mabadiliko,lakini yote ni mabadiliko katika maslahi ya seriali kubwa na kwa ajili ya kupanga tama zao au kwa lugha nyengine ni kugawanyiana manufaa ya kilimwengu baina yao kwa namna isiopelekea katika vita na mvutano wa kisilaha.Hakika karni ya kumi na tisa Miladi zilikuwa zama za ukoloni, zikamimika serikali ulimwenguni zikikoloni nchi dhaifu.Ikawa yapatikana kwa ajili ya ukoloni huu ambao haukufikia kiwango cha vita vikubwa.Lakini ilikobaika kwa Uingereza,Ufaransa,Urusi kwamba Ujeruma na nguvu zake kubwa ikawa yatatishia na wakaona kwamba itachukuwa petroli ya nchi ya kiislamu Iraq, ikatishia Uingereza na petrol ya Iran na Bara Arabu.Zikaafikiana serikali hizi tatu dhidi ya Ujerumani,zikaitangazia vita,ikaingia serikali kiuthmani vita hivi upande wa Ujerumani dhidi ya washirika wake.Ikawa ushindi niwa

washirika,isipokuwa Urusi ilitoka katika ushirika huu,ikabakia Ufaransa,Uingereza na Marekani.Amma Marekani ilirudia kujiondoa kwake,ukakia uwanja baina ya Uingereza na Ufaransa.Zikasimama serikali hizi mbili ili kupanga ukoloni baina yao na kuzuiya kupatikana kuwepo mivutano ya kisilaha kwa kubuni Umoja wa mataifa.Hilo ni kwa ajili ya kupanga mambo ya serikali na kuzuiya vita baina yao.Isipokuwa umoja wa mataifa ulipatikana katika hali geni na mgongano,hakika ilikuwa inayumbayumba,kwakuwa siasa ya serikali kubwa haikubadilika.Ikawa hamu ya kila moja wapo katika kongamano la suluhisho ni kuhakikisha usawa ya nguvu tofauti,kuhami maslahi yao,kugawanya milki za Ujerumani na serikali ya kiuthmani,hazikukubali serikali za kikoloni kuguswa ubwana wake kwa lolote na zikahifadhi koloni zake,zikazidisha namna nyengine ya ukoloni ulioitwa kwa jina la (serikali chini ya uwakilishi).Ikawa katika athari ya haya ni kuteleza ikatelea umoja wa mataifa katika jaribio lake la kuunganisha serikali na kumakinisha usalama.Imejaribu kuweka mikataba ya kimataifa ili kudhamini amani, yaani kudhamini kutovutana na koloni.Ikawekwa chini usimamizi wa jumuiya Protokal Geneva 1924 M,malengo yake ni kuweka sawa mizozano kwa njia ya amani na ikalazimisha kurudia kuhukumu kinguvu.Ikawekwa mikataba ya Locarno 1925 M, ikapitisha ubadilishanaji wa dhamana na ushirikiano wa misaada.Ukawekwa mkataba wa Briand-Kellogg 1928 M,ukakataza kushikamana na vita na mkataba wa Geneva 1928 M ukawa haswa ni kuhukumu kwa nguvu.Lakini mikataba hii yote haikuweza kuzuiya kuanguka kwa umoja wa mataifa katika umuhimu wake,ikatokezea mbele ya masikio yake

na macho yake vita kadhaa miongoni mwazo ni vita vya China na Japan mwaka wa 1933 M,vita vya Utaliano na Habash mwaka wa 1936 M,vita vya Ujerumani na Austria mwaka wa 1939 M,vita vyake dhidi ya Czechoslovakia mwaka wa 1938 M kisha Poland mwaka wa 1939 M mpaka ilipotokea vita vya ulimwengu vya pili mwaka wa 1939 M.

Haya ndio mabadiliko yaliotokea katika mahusiano ya kimataifa,yakabadilika makonga mano kuwa ni vyama vya kimataifa vilivyosimama kuhifadhi usalama wa kimataifa lakini maendeleo haya hayakubadilisha kitu,zikabakia serikali kubwa zazozania ngawira mpaka ilipotokezea vita vya pili vya.Baada ya vita vya pili vya dunia zikaona serikali kubwa zianzishe chama cha kimataifa ni mbinu bora ya kupanga mahusiano baina yao na kuifanya kuwa ndio chama cha serikali zilizoingia vitani,kisha wakakipanua na kukifanya chama cha kilimwengu kinachorusiwa kuingia serikali jumla za ulimwenguni.Zikapanga mahusiano ya kimataifa kwa mikataba ya chama hichi.Kwahiyo yatakuwa mahusiano ya kimataifa yamebadilika kutoka kongamano la serikali kubwa kudhibiti ulimwengu,kugawanya ngawira baina yao na kuzuiya isitokezee serikali kubwa isiokuwa wao itakayobadilika kuwa chama cha kimataifa kitakachopanga mahusiano baina yao,kudhimi udhibiti wa serikali kubwa kisha kuwa chama cha kimataifa kitakachokuwa kama serikali ya kilimwengu,itakayopanga mambo ya serikali za kilimwengu na kuzidhibiti.

Hakika msimamo wa kimataifa baada ya kongamano la Viena 1815 M ulikuwa ukionekana katika serikali nne kubwa Prussia,Urusi,Austria na Uingereza. Ilipojaribu

Ufaransa kutingisha serikali hizi kutoka vituoni mwao,kubadilisha ramani ya ulimwengu,ikabadilika msimamo wa kimataifa,ikawa serikali ya kwanza,zikaungana serikali nyengine kubwa dhidi yake na kumaliza tama yake kisha zikashirikiana naye kudhibiti ulimwengu.Ukawa msimamo wa kimataifa ikionekana katika serikali hizi tano.Ikaanza Uingereza kudhihiri kidogo kidogo mpaka ikawa serikali ya kwanza.Ilipojaribu Ujerumani kuzozana na serikali ya kwanza na kunyakuwa mafuta ya biladi za kiislamu,ikawafikiana Uingereza, Ufaransa na Urusi juu yake,wakapambana nayo,ikamaliza tamaa yake na ikawa ndio koloni pekee katika sehemu nyingi za ulimwengu.Ikawa kushiriki kwa Uingereza ni kushiriki kwa simba,ikaridhisha Ufaransa na taka za chakula na kuipa baadhi ya koloni.Ukawa msimamo wa kimataifa waonekana na Uingereza na Ufaransa wakiwa na Utaliano isipokuwa Uingwrwza ilibakia kuwa ndio serikali ya kwanza kisha ikapatikana umoja wa kimataifa,ikwawa lengo la kihakika la kupatikana kwake ni kuhifadhi kituo cha serikali ya kwanza,kuzuia serikali nyengine kuzozana nayo na kuzuia serikali yoyote isiwe serikali kubwa hata kama itabuniwa kwa huja ya kuhifadhi usalama wa ulimwengu.Ilipojaribu Ujerumani mara nyengine kuzozana na serikali ya kwanza na kuwa serikali kubwa, ikawafikiana Uingereza na Ufaransa mara ya kwanza kisha Uingereza,Ufaransa, Urusi na Marekani wakazindua vita vya ulimwengu vya pili mpaka wakaimaliza.

Isipokuwa matokeo ya vita hivi mara hii vilikuwa dhidi ya Uingereza,imetoka katika vita vya kuvunja mbavu.Serikali iliotoka mshindi ni Marekani.Kwahiyo

ikabadilika nguvu ya serikali kutoka mkono wa Muingereza hadi mkono wa Marekani,ikawa Marekani ndio serikali ya kwanza,ukawa msimomo wa kimataifa waonekana kwamba Marekani ndio serikali ya kwanza,kwamba muungano wa kisovietindio inayozozana nayo na kwamba Uingereza na Ufaransa ni serikali mbili zilizo daraja ya pili yaani serikali mbili za pili katika msimamo wa kimataifa.

Isipokuwa imetokezea katika msimamo wa kimataifa baada ya vita vya ulimwengu vya pili sababu mpya nayo ni kugawanya ulimwengu wa kimataifa kambi mbili,hili ndilo lililozidisha nguvu ya mvutano wa kimataifa,kukawekwa msimamo wa kimataifa na haukuwa kwa namna iliopo kabla yake.Ndio msimamo wa kimataifa ulikuwa kabla ya vita vya ulimwengu vya kwanza uko kimakundi lakini hakukuweko na kambi.Ikawa kabla ya vita vya ulimwengu vya pili umegawanyika mirengo wa kidemokrasia na mrengo wa kidikteta wa unazi na ufashisti,lakini haukuwa mgawanyiko kwa sura ya kikambi za kimfumo.Kwakuwa unazi na ufashisti si mifumo wala haienuki kufikia mfumo.Kwahiyo hapakuwepo kabla ya vita vya kilimwengu vya pili kambi kwa maana ya mfumo.Amma baada ya vita vya ulimwengu vya pili ulimwengu umekuwa ukigawanyika kimataifa kambi mbili nazo ni kambi ya kimagharibi na kambi ya kimashariki,huchukuliwa Marekani ni serikali ya kwanza katika kambi ya kimagharibi na huchukuliwa Urusi nio (muungano wa kisovieti) ndio serikali ya kwanza katika kambi ya kimashariki.Hakika hata kama kambi mbili zavutana kwa msingi wa kimfumo na kuzozania maslahi yanayogongana baina yao,isipokuwa zimesimama juu ya

msingi wa kimataifa,kwakuwa mfumo peke yake haukuwa ndio kituo cha mgawanyiko wa kambi mbili bali kuna na maslahi ya kitaifa pia, ila maslahi haya ya kimataifa yalikuwa yenda katika kambi ya kimashariki kulingana na mfumo wa kikoministi na kulingana hali zinazolazinu kuenea kwake.Huenda kambi ya kimagharibi kulingana na siasa ya kueneza mfumo kulingana na maslahi ya kitaifa na kizalemdo kwa msingi wa kirasilimali unaofanya manufaa ndio kipimo cha vitendo jumla katika maisha.Kwahiyo twapata katika kambi ya kimagharibi serikali zisizo kuwa na mfumo wake lakini maslahi yake yamefikana na maslahi yao na hayakuwepo haya katika kambi ya kimashariki.Kwa hili serikali zote za kambi ya kimashariki ni za koministi na katika kanbi hiyo hiyo,wala hakuna serikali zisizokuwa za kikoministi kwakuwa kituo chake ni mfumo,pindi ilipokuwa kambi ya kimagharibi imevunjika.Kwahiyo ilikuwa yawezekana kutokezea mwanya katika kambi ya kimagharibi,yawezekana kutolewa serikali humo hadi kambi ya kimashariki na yawezekana kuwa katika kambi ya kimagharibi kambi nyengine isiokuwa kambi mbili ikisimama peke yake ilio na athari zake katika misimamo ya kimataifa katika hali mbili usalama na vita.

Anayeangalia kwa makini kambi ya kimagharibi atapata kuna mgawanyiko wa kindani uliotokamana na kupanda Marekani kituo cha serikali ya kwanza.Baada ya kuwa kituo hichi ni cha Uingereza na baada ya kuwa Marekani imejiondoa katika msimamo wa kimataifa.Mgawanyiko huu uko wazi haukufichika,nao ndio uliokuwa ukiahirisha kusimama chama cha kilimwengu.Serikali ya kwanza haikufata katika siasa ya kimataifa mwendo wa mkubwa wa kambi,kama ilivyokuwa hali ya Uingereza

ilipokuwa serikali ya kwanza,bali yenda mwendo wa msingi wa kambi na kulazimisha mwongozo huu wanajeshi kikamilifu.Kwahiyo zilikuwa serikali za kambi ziko karibu kinguvu kuliko serikali ya kwanza kama Uingereza kwa mfano yenye chuki zaidi na kuasi sana kuliko serikali ndogo na siri ya hayo yarudia siasa ya Marekani yenyewe.Hakika baada ya kushinda kwake katika vita vya pili vya ulimwengu akaazimia mvutano wa ubwana kwa serikali zote,kama alivyo azimia kulazimisha ubwana wake ulimwenguni,ikaghurika na ilipofikia na nguvu zake na wingi wa mali yake mpaka ikajiona kwamba ni lazima ishike ulimwengu mzima na kwamba mataifa na serikali msaada wake na kutaka ridha yake.Kwahiyo ikapambana na Ulaya kwa vitendo vya kisiasa,miradi ya kimali kisha baada yake kwa mapinduzi ya kijeshi katika koloni zake,haswa Uingereza.Imekuwa serikali ya kwanza na serikali yenye koloni nyingi kisha Ufaransa kisha Uholand.Nayo badala ya kuvamia koloni,imevamia serikali za kikoloni zenyewe kwa mradi wa Marshal,kutoa misada na madeni.Mpaka itakapo jimakinisha huelekea katika koloni,ikaanza kuishika na kuidhibiti kidogo kidogo mpaka itakapochukuwa koloni zake zote lakini kwa mbinu inayotafautiana na mbinu alioshambulia serikali zilizobakia za Ulaya.

Kwahiyo ikaenea tafauti baina ya serikali za kambi ya kimagharibi na tafauti hii si mpya bali ni tofauti ya zamani.Imeanza tofauti hii katika kambi ya kimagharibi kabla ya vita vya pili va ulimwengu,isipokuwa tofauti katika kambi moja bali ni tofauti ya kiuchumi baina ya serikali kisha ikabadilika kuwa katika kambi moja. Yarudia tofauti hii katika matatizo ya kiuchumi na haswa tatizo la petrol. Kwakuwa makubaliano yanayoambatana

nayo ni baina ya Uingereza na Marekani na haja ya Uingereza msaada wa Marekani ndicho kilichopelekea tofauti baina ya serikali hizi mbili na mwishowe baina ya serikali za kambi ya kimagharibi.Hiyo ni kwamba Uingereza baada ya kujimakinisha msimamo baada ya vita vya kwanza vya ulimwengu,ikawa Ufaransa ndio inayozozanana nayo na kuwa mzozano huu uko wazi,ikawa yafanya kazi kudhoofisha Ufaransa kwa kuipa nguvu Ujerumani upande mwengine na kuhimiza harakati za kizalendo na kitaifa katika koloni kiupande mwengine.Ikaleta shida kwa Ufaransa na kuishuhulisha na kujikinga na hatari ya Ujerumani.

Isipokuwa ilitokezea katika msimamo wa kimataifa hapo jambo la Utaliano, ikadhihirika kwa Ujerumani nguvu zinazotishia msimamo wa Uingereza pamoja na Ufaransa na kudhihika mpaka Roma na Berlin.Ikawa ni lazima Uingereza kuitoa Marekani kutoka upweke na kumtia tama na petroli ya mashariki,ikawa makubaliano ni petroli.Isipokuwa Marekani baada ya kuanza uchimbaji wa petrol yakapata mashirika ya kimarekani thamani ya petrol ya mashariki,si kulingana na faida ya kiuchumi peke yake bali kulingana na muundo wa Marekani yenyewe. Kwahiyo ikaanza kunyakuwa visima vya mafuta na upendeleo wa petrol kutoka mashirika ya Uingereza,ikaanza kuizidi kukawa na mashindano baina ya mashirika ya Uingereza na Marekani.Kwa kutoka mashirika ya Marekani huko mashariki.katoka Marekani kutoka upweke wake kisha vikatokea vita vya pili vya ulimwengu,basi ikasongea Marekani mpaka daraja ya serikali ya kwanza,ikashuka Uingereza na Uholanzi.Amma Uholanzi hakika kwa udhaifu wake ilimalizika mambo yake.Amma Uingereza hakika hii

ilipata hasara ya baadhi ya nguvu zake mashariki,ikapata hasara baadhi ya nguvu zake kwa kuingia bahari ya kati na kupata hasara baadhi ya nguvu zake katika baadhi ya serikali ndogo.Kilichofanya msimamo wake wa kimataifa kushuka kwa kiwangocha chini,ikaendelea Marekani kuifata katika kusafisha nguvu zake ulimwenguni kote.Amma Ufarasa hakika baada ya kuondoka koloni zake mashariki ya mbali na Afrika yilidhoofika mambo yake,juu ya majaribio yake de Gaulle ya kuinyanyua na kurudisha nguvu zake za kimataifa,isipokuwa haikumakinika kuirudisha katika malisho yake ya kimataifa kama ilivyokuwa mwanzo,hata kama bado yahesabiwa ni serikali kubwa.

Kufikia hapa yote yabainika kwamba kugawanyika kambi ya kimagharibi na kuvunjika kwake baada ya vita vya pili vya dunia na wakati wa vita baridi kumedhoofisha serikali zake zote isipokuwa Marekani,hakika kwa kusafisha serikali hizi,kwa kuchukuwa koloni zake na kwa nguvu walizo nazo ilibakia kuwa ni serikali ya kwanza na kujengeka kituo chake.Lakini Uingereza ilibakia kipindi cha zama ikitekeleza mikakati ya kisiasa na matendo ya kijeshi mengineo. Ili kuathiri kituo cha washirika wake Marekani,kutetemesha kutoka kituo chake cha serikali ya kwanza kisha kutosheka baadaye na majaribio ya kuhifadhi maslahi yake pasi na kuathiri kituo cha washirika wa Marekani,baada ya kumbainikia kiasi cha udhaifu wake na ilipofikia upungufu wa nguvu zake,hasa katika kuelekea serikali kubwa kwa uweza wake wa kijeshi na kiuchumi kama Marekani.Kwahiyo ikawa kambi ya kimagharibi kwa kuizingatia peke yake imevunjika,inayozozana imekumbwa na mpasuko,na

tafauti serikali zake zote,zashindania manufaa na zafanyiana vitimbi zanyewe.
Amma kambi ya kimashariki hakika ilisimama juu ya msingi wa kimfumo peke yake hadi mwanzo wa miaka ya sitini karni iliopita,ilikuwa ikiongozwa na Urusi (muungano wa kisovieti) mongozo wa kifikra na kijeshe,ikawa mahali pa mwalimu anayehusia kiupande na mahali pa mlinzi na kiongozi upande mwengine.Kwahiyo hapakuwepo baina ya serikali zake anayeshindana Urusi (muungano wa kisovieti) juu ya muongozo wa kifikra na kisiasa,bali hapakuwa anayethubutu serikali yoyote miongoni ya serikli zake kuingilia siasa ya kisovieti, ikitokezea basi ilikuwa ikimalizwa kwa huku kuingilia kwa nguvu za kijeshi ikilazimu.Siasa ya kambi ya kimasharika imesimama tangu masiku ya Stalin kindani juu ya msingi wa kutia nguvu nguzo za serikali,kurejesha nguvu za kijeshi kivita ili kutetea na kuvamia wakati mmoja,ikawa siasa ya nje yasimama juu msingi wa kutowezekana makubaliano ya amani kati ya urasilimali na ukoministi. Kwahiyo akawa anaona kwamba ni lazima kudumisha kuufanya urasilimali kuwa ni mtesi wa kisiasa.Kwa hakika ni mtesi wa kifikra.Pindi vilipotokezea vita vya pili vya kilimwengu,ikasaidina Urusi,(muungano wa kisovieti) pamoja na Uingereza, Ufaransa na Marekani vitani,wakaishi kipindi upande hadi upande.Lakini hali ya kidharura iliovuliwa haikuendelea na maringo baada ya kumalizika,vikarudi vita baridi baina ya Urusi(muungano wa kisovieti) na serikali za kimagharibi pamoja na kubakia mshikamano wa kisiasa.Mshikamano huu wa kisiasa ulikuwa katika baraza la umoja wa mataifa,katika mikutano ya kimataifa,ufadhili wa

kidiplomasia kuongezea na uwakilishi na haikumaanisha kubadilisha siasa ya kikoministi ya kimsingi,bali ilikuwa ni mbinu kati ya sampuli ya mbinu za kisiasa.Amma siasa ya kikoministi mbele ya kambi ya kimagharibi,asli yake ni fikra iliosimama juu yake muungano wa kisovieti,hilo ni kwamba mfumo wa koministi walazimu kile kinachoonesha kwamba urasilimali na ukoministi haiwezi kuishi kwa amani upande na upande,lazima mmoja ushinde mwengine na jumla ya vitabu vya kikoministi vyataja kuhalalisha kuepukana na mizozo baina ya mifumo miwili.Rai hii ni katika rai wanazoona kila mmoja kati ya Lenin na Stalin wala hakuna alie tafautiana na mwengine kirai,wakoministi wote waliwafikiana juu ya fikra hii na hawakuepukana na mwana siasa yoyote wa koministi,awe ni kiongozi au asiyekuwa kiongozi au asiyekuwa kiongo,aende mwendo wa siasa ya makubaliano ya amani baina ya urasilimali na ukoministi.Kwakuwa ilizingatiwa kwamba imetoka nje ya fikra ya kikoministi katika siasa ya nje.

Hii ndio hali walivyokuwa nayo kambi mbili upande wa kimfumo,upande wa kisiasa na upande wa kiserikali,isipokuwa tangu waka wa 1961 M kumetokezea mabadiliko katika kambi mbili upande wa kiserikali yaliopelekea katika mabadiliko ya hali yao ya kihakika na kupelekea katika mabadiliko ya misimamo ya kimataifa.Hilo ni kwamba kambi mbili tangu nusu ya pili ya mkataba wa sita yaani tangu mwaka wa 1956 M akaanza kila mmoja harakati na kugaagaa ikaendelea kukuwa mpaka ikapelekea kuanguka kambi mbili muanguko kamili na ikawa kambi mbili ni serikali mbili:Marekani na muungano wa kisovieti pasi na kupigia

serikali hizi mbili serikali za kambi zao zilizo bakia hesabu yoyote.
Amma kulingana na kambi ya kikoministi hakika serikali ya kikominista ilisimama juu ya msingi usiokuwa wa kitaifa,juu ya msingi wa kimfumo,yaani ilisimama juu ya msingi wa kuwa serikali ya kikoministi ulimwengu mzima na kwa ulimwengu mzima.Msingi huu uliilazimu mambo mawili: moja wapo ni kuendelea katika hali ya kujiandaa kwa kudumu kindani,kijiandaa vikali nguvu za kiuchumi na nguvy ya kijeshikwa ajili ya kueneza ukoministi.Haya yalazimu mikazo mikali kwa raia kwa sura ya kudumu upande wa kisiasa na upande wa kiuchumi.Kwa hiyo ikaendelea serikali ya kikoministi kuwa ujanamizi mzito kwa raia a Urusi,ikabakia Urusi kunyimwa upande wa kiuchumi vifaa mpaka baadhi ya mambo ya kidharura,hayo yote ni katika njia ya kueneza ukoministi ulimwenguni. Amma jambo la pili lililolazimu serikali ya kikoministi nalo ni kusimama katika hali ya utesi ulioenea na serikali jumla za kimagharibi,kwa sifa ya kuwa ni serikali za kirasilimali za kibepari,kuwasha vita baridi nao kwa sura ya kudumu na kujiandaa kuingia katika vya kujihami kila wakati.Hili ndilo lililofanya ulimwengu kuwa kambi mbili zilizo na uadui kwa sura ya wazi na namna itakayo wapelekea katika vita kila wakati.Isipokuwa ufisadi wa kikoministi umezidi haukumakinisha watu wake kuendelea masafa ya nadharia yake hadi mwisho wake.Kwahiyo mnamo mwisho wa miaka ya hamsini karni iliopita,ilikuja kilikuja chuo kipya cha hukmu,ikaanza ukoministi kufasiri tafsiri mpya inayowafikiana na maslahi ya Urusi na ikokaribu zaidi ya kitaifa kuliko ya kikoministi.Kulingana na siasa ya kindani faraja kwa watu upande wa kisiasa na upande

wa kiuchumi. Wakahafifishia watu mikazo,wakawa wanaruhusu kidogo kidogo bidhaa za matumizi.Kulingana na siasa ya nje wakaanza kujaribu kujikurubisha kwa Marekani,kuleta mahusiano makubwa nayo,ikawa kwapita baina ya Urusi (muungano wa kisovieti)na Marekani mawasiliano ya haraka ili wakubaliane kusi vita baina yao kisha zikaanza kupanuka sehemu za mawasiliano mpaka zikajimlisha maswala jumla ya serikali yanayoweza kuwa na tafauti baina yao. Yalipoiva mawasiliano haya,kukawa na mkutana hatari baina ya Khrushechev na Kennedy mwezi wa sita 1961 M,yakapita makubaliano jumla juu ya maswala jumla ya serikali.Kwahiyo ikajiondoa Urusi (muungano wa kisovieti) kutoka fikra muhimu upande wa serikali nayo ni fikra ya uadui wa kudumu baina ya ukoministi na urasilimali.Ikajiunga na siasa ya makubaliano kwa maana yake ya kirasilimali.

Amma kambi ya kirasilimali hakika Marekani ilijua kwamba Uingereza yenda kinyume naye na kubadilisha kuzozana nayo juu ya ngawira.Ikaona hali ya vita baridivilivyoko baina ya kambi ya kimashariki na kambi ya kimagharibi ni hali inayoangamiza nguvu zake,nayo ni hali isiokuwa ya kivita itakayobadilika kuwa maandalizi ya kijeshi kutokana na kukuwa kwa kiuchumi wala si usalama uliobadilika kuwa kukuwa kwa uchumi kuliko tokana na maandalizi ya kijeshi,bali ni hali baina ya usalama na vita.Nayo hutumia kiwango kikubwa katika mali ya serikali katika njia ya kujiandaa kijeshi kwa kitu cha kuchanganyikwa yaani kwa vita visivyojulikana kwamba vitatokezea.Katika upande huo ikaona Uingereza yenyewe ndio yenye kuwasha moto wa vita hivi baridi na kuviendeleza kwakuwa makusudio yake katika hayo ni

kubakia Marekani kubakia katika hali yakumalizika pamoja na mali yake na uweza wake,idhoofike kidogo kidogo pindi atakapo keuka usawa wa kimataifa.Ikaona Marekani kwamba maslahi yake ni kujikurubisha na Urusi(ukoministi)dhidi ya Uingereza (urasilimali).Kwa namna ambayo ufisadi wa kirasilimali yamejazana pia,kwakuwa manufaa yako katika ngazi ya juu ya thamani kwa warasilimali,kwa namna ambayo hawana thamani thabiti kwao,bali yapapia maslahi ya kimada.Kwahiyo ikawa Marekani pia yajaribu kubana sehemu ya mgawanyiko baina yake na Urusi (muungano wa kisovieti), ikaanza kujaribu kuingia naye katika mikataba.Hiyo ni tangu nusu ya pili muongo wa sita karni iliopita,yaani tangu masiku ya Eisenhower na kabla kuja Kennedy, hakuja Kennedy isipokuwa alikimbilia kutimiza hatua ya kukurubiana baina ya Marekani na Urusi,haukupita mwaka na baadhi ya mwaka alipochukuwa utawala mpaka kukawa na mkusanyiko wa Viena mwezi wa sita 1961 M baina yake na Khrushchev .Yakapita makubaliano jumla juu ya maswala jumla ya kimataifa inayowezekana kuwa na tofauti baina yao,kwahiyo ikajiondoa Marekani mwisho kutoka fikra muhimu aliokuwa nayo kwa muda unaokurubia nusu karne,nayo nifikra kuumaliza ukoministi na kuindowa kutoka ramani ya ulimwengu.Ikaanza kujikurubisha na muungano wa kisovieti katika kile kilichoitwa mkataba wa amani,ikaendele hivyo kwa muda unaozidi miongo miwili hadi alipokuja Reagan kutawala Marekani miaka ya themanini,iliporudi kuhuisha kazi ya kumaliza muungano wa kisovieti upya.

Hivi ndivo yalivyowafikiana maslahi ya viongozi wa kambi mbili ilikubakia kuwa watekelezaji wa kimataifa na

kuzuia kutokezea wasiokuwawao.Yaonesha kwamba pia wamewafikiana juu ya siasa ya kumuunga Mchina na kumtoa  Muingereza kutoka koloni zake na kung'oa nguvu zake kutoka mashariki ya Katina ya mbali na kuzuiya Ujerumani kurudi kuwa serikali ya kinuklia.Kisha wakawafikiana juu ya makubaliano ya amani baina yao au kile kilichoitwa mkataba na kadhalika kutorudia nguvu ya kijeshi katika kutatua matatizo baina yao.Wakawafikiana juu ya kugawanya ulimwengu baina yao na kupanga maeneo ya nguvu zao huku ukiwepo msaada mmoja kwa mwengine katika maeneo yao na kwa lugha nyengine walikuwa washirika wawili wanachanganyikana kuwa nguvu moja ya kilimwengu.Kwa makubaliano haya yote hubadilisha hali ya ulimwengu msimamo wa kimataifa.

Amma msimamo wa kimataifa hakika ulimwengu haukuchukulia kambi mbili mbele yao kuwa watazozana kisiasa,kiuchumi na kuenea mahusiano baina yao matatizo mengi kama ilivyokuwa hali kabla1961 M,ulimwengu ulikuwa kambi mbili kifikra.Basi fikra ya kikoministi ikabakia kwa kipindi hicho,ikiwemo katika serikali za kikoministi na fikra ya kirasilimali ikionekana katika serikali za kirasilimali.Fikra mbili haziwezi kulingana baina yao,basi ulimwengu upande huu ni kambi mbili bila shaka.Amma upande wa kimataifa zimeondoka kambi mbili,ukawa ulimwengu wote ni nguvu moja,inayoonekana Marekani na Urusi,wakawa mababe wawili peke yao ndio mwenye ndio pamoja na kutangulia Marekani kuwa katika kituo cha serikali ya kwanza.

Juu ya hayo basi hakika kambi mbili ya kimashariki na ya kimagharibi zimeondoka na hazikubakia kambi za

kimataifa ulimwenguni.Hakika msimamo wa kimataifa umebadilika kimizizi,ukarudi ulivyokuwa kabla vita vya kwanza vya ulimwengu,yaani zimekuwa serikali kivyao kila serikali yenda mbio kuchukuwa ngawira,kudhoofisha serikali nyengine na kukawa na maingiliano baina yaserikali na serikali sio baina ya kambi na kambi.Tofauti baina ya hali katika kipindi cha makubaliano baada mkutano wa Viena na hali kabla vita vya dunia vya kwanza,kwamba msimamo wa kimataifa ndio uliotawala serikali mbili kubwa na kubadilisha serikali zilizobakia kuepukana na shari ya serikali mbili na kwamba ipatikane baina yao mkusanyiko itakaoleta nguvu itakayosimama mbele ya serikali mbili,tofauti na hali kabla vita vya kwanza vya dunia vya kwanza.Zilikuwa serikali kubwa zakurubiana kinguvu,hata kama serikali ya kwanza inanguvu zaidi ya zote,kukurubiana huku kwaweza kupelekea katika upungufu wa mizani ya nguvu na mvutano wa ngawira uliopelekea katika kuwasha moto wa vita dunia vya kwanza.

Amma kipindi cha makubaliano,hakika nguvu ya serikali mbili zilizoungana zilikuwa zimezidi sana za nguvu za serikali yoyote katika serikali za kilimwengu. Kwahiyo havikuto vita vya kilimwengu vikubwa kwa maana inayojulikanwa toka mwanzo bali hapakuwepo na shaka inayopelekea kuungana serikali nyengine katika mgawanyiko unaopelekea katika vita vya kilimwengu.Vile vile hali baina ya hali ya msimamo wa kimataifa katika kipindi cha makubaliano na baina ya hali yake kabla ya vita vya pili vya dunia.Hakika kabla ya vita vya dunia vya pili zilikuwa serikali zilizotengana,hata kama muundo wa miungano,lakini kwa hali yoyote zilikuwa nguvu zilizokurubiana mara ya kwanza kisha

ikafikia kukosa usawa,ikapata nguvi Ujerumani,Utaliano,Japanna haikupata nguvu Uingereza na Ufaransa.Ikawa Marekani katika kujitenga kwake,ikapelekea kukosekana huku kwa usawa katika msukumo wa  Utaliano,Ujerumani na Japan kila moja kivyake kuchukuwa nchi kwa njia ya kivita.Likapelekea hilo kwa kufatilizia kwake katika maingiliano makali yaliyoleta vita vya ulimwengu vya pili,kinyume na hali katika kipindi cha makubaliano.Hakika msimamo wa kimataifa ulikuwa ukionekana kwa wababe wawili wakubwa na makubaliano baina yao nayo ni hali isiyo ruhusiwa kutokezea mvutano wa kimataifa utakaopelekea katika vita vya kilimwenu,bali yaruhusiwa peke yake mvutano baina ya baadhi ya serikali na serikali mbili au baina ya baadhi ya serikali kwa nyengine.Lakini mfani wa mvutano huu hata ukitokezea vita vya wenyewe kwa wenye,hakika nguvu za serikali mbili kuu zilikuwa msimamizi wa kuzima vita hivi wapendapo.

Isipokuwa siasa ya makubaliano ilioanza na makubaliano ya 1961 M baina ya Marekani na muungano wa kisovieti yaani mvutano baina ya urasilimali na ukoministi lakini kulikuwa na visingizio na sababu,ikawa pande zote mbili vimewaangamiza vita baridi na kujiandaa kwa kitu kisichojulikana kutokezea au kutotokezea zikaelekea katika makubaliano baina yao na kugawanya ulimwengu. Kwa ajili ya kupata faragha kila mmja na kupanga mambo yake ya kindani.Kwa kumalizika vita vya Vietnan ukaanza mkataba kukosa umuhimu wake.Ilitolewa Ufaransa kutoka koloni zake ikarudia Ulaya kuitilia nguvu.Amma Uingereza hakika ilihisi udhaifu wake ikaanga kujijenga na Ulaya ili kuokoa kinachowezekana kuokolewa,ikawa muunga wa kisovieti iko na nguvu ya

kijeshi na mikakati mikubwa.Ikahakikisha kuzidi katika upande wa vita vya kumaliza, ikaweza kupanuka kuwepo kwake katika maeneo ya mbali na maeneo muhimu,ikawa ina nguvu ya kilimwengu kwa namna ya kuathiri.

madai,ikapatikana humo,kwa athari ya upinzani wake wa ukoloni wa ulaya ,ikielemea katika fadhila za daraja ya juu na kuikuza.Isipokuwa raia wa Marekani wamejiunga na urasilimali kama ulimwengu uliobakia wa naswara wakawa wanavutiwa na sababu mbili:Sababu ya kukinai na kuepushwa na machafu na sababu ya manufaa na ukoloni.Ikawa Uingereza yapatiliza sababu ya kwanza ikiitumia ili iwe nguvu yake katika vita na uchumi,ilipokuwa sababu ya kwanza ndio inayo ianayotawala.Ilipokuja vita vya ulimwengu vya pili na kuonja raia wa Marekani chakula cha ukoloni katika mafuta ya Ghuba mpaka ikamzidia sababu ya pili nayo ni sababu ya manufaa na ukoloni,ukampeleka mfumo wa kirasilimali.Akatoka katika upweke wa kukoloni mataifa,akaunyenyekea ulimwengu kuudhiti na nguvu zake na hatorudia upweke wake mara ya pili ila kwa nguvu,kwakuwa mfumo wa kirasilimali umemtawala na ndio iliokuwa unaopeleka maisha yake,ikawa manufaa peke yake ndio kinachotawala nyenendo zake,kuongezea na kiburi na kujiona vilivyo jaa katika maisha yake.

Marekani ilikuwa imetawaliwa na serikali za Ulaya haswa Uingereza,ikawa imegawanyika katika serikali kadhaa,basi ikapunguza kwa mara ya kwanza kukinyagwa na ukoloni wa Uingereza kisha ikaingia katika vita vikali vya kujikomboa vilivyopelekea kuifukuza Uingereza kutoka biladi yake.Zikakubaliana serikali hizi kuleta muungano baina yao,kuunda serikali moja kati yao, likakamilika hilo kwake kisha ikashika serikali nyengine mara kwa hiari na mara nyengine kwa nguvu ya kijeshi na kuyafanya ni majimbo katika serikali,mpaka ikakamilika muundo wake kwa sura ilivyo leo ikawa sasa na majimbo hamsini na moja,imeinukia

serikali na nguvu ikawa katika mpambano ni serikali yenye nguvu,ilioweza kuhami mabara mawili ya Marekani kutoka na usaliti wa srikali za Ulaya,ikawa ni ulimwengu mwengine,nao ndio unaojulikana kama ulimwengu mpya,umejengwa juu raia wachangamfu,uliopatikana katika biladi yake utajiri mkubwa.Imesimamisha Marekani nidhamu ya kiutawala wake,hatakama ni katika nidhamu za kidemokrasia,lakini ni nidhamu iliowekwa kupitia fikra ya kindani na ujuzi wa kielemu wa maana utawala,pamoja na kuwa ni utawala wa kibinadamu,
inayotawaliwa na watu katika binadamu,wala hakudhania utawala mfano wake dhana ya limantiki,bali alijua ujuzi wa kihakika wa kielimu,hilo lajulikana vizuri kwa namna ya kunasibisha kiongozi wa jamhuri,katika uwezo mpana iliopewa, katika,jukumu lake serikalini na kupanga jukumu lakinikatika sehemu zilizobakia za serikali,katika nguvu moja inayoonekana.Yasimama juu yake pamoja na kuwa nidhamu ya muungano,katika masafa yake makubwa yaliyopawa raia katika kumchaguwa kwao raisi wa serikali na katika kuchaguwa nguzo zake.Likawa hili lina nguvu kubwa kwa serikali,katika kukuza nguvu hizi kwa haraka sana.Ilikuwa kabla vita vya pili vya ulimwengu imetoka katika upweke wake na kushiriki katika katika kupeleka ulimwengu,bali ikajaribu kuwa peke yake katika idara hii,kisha ikashiriana naye adui wake Urusi ya kisovieti tangu mwaka wa 1961 M. katika idara ya ulimwengu ikazidi tama ya serikali kubwa zilizo bakia.Ilipoona kwamba imetoa malengo kutokana na makubaliano,ushirikiano na Urusi (muungano wa kisovieti) na kwamba ushirikiano huu umeleta baadhi ya

upande wa hasara,zikawa serikali za Ulaya zajaribu kumuepuka,kuanzisha mahusiano na Urusi (muungano wa kisovieti) na kwamba muungano wa kisovieti imekuwa yatekeleza majaribio la kishujaa,hata kama haukufaulu kwa kuingia katika mkusanyiko wa siasa za kimaifa.Ili kwa hilo ajichukulie kuwa ni mbabe wa kimataifa kando na siasa ya kimarekani,ilipoona Marekani hilo iliamua kurudia kupanda na Urusi (muungano wa kisovieti),kuingia katika mashindano ya silha mpya,kilichoidhinisha vita baridi vipya,ikaingia na Urusi (muungano wa kisovieti) na kambi ya kimashariki vita vya kihadhara kifikra na kiuchumi,akamfunga na mikataba,kilichopelekea kuporomoka muungano wa kisovieti mwisho wa mambo,ikaiwacha Marekani kuwa niserikali ya kwanza na mbabe mwenye athari sana katika siasa ya kimataifa.

Kuna vyama viwili vikuu navyo: Chama cha kidemokrasia na chama cha kijamhuri,wala mtu hawezi kupata tofauti kubwa baina mipangilio ya vyama viwili ilioandikwa,mpaka kwenye siasa inayofatwa.Vyama hivi viwili vyakurubia kufata njia moja wala haikurubii kutokezea mabadiliko katika kuzunguka hukmu baina vyama viwili sawa iwe ni katika siasa ya kindani au siasa ya nje,yakitokezea mabadiliko basi itakuwa imelazimu madiliko ya dhurufu ,wala si tofauti ya vyama viwili.

Chama cha demokrasia ndio chama kikongwe nacho ni chama raia,chamiliki kiwango kikubwa cha raia.Kwahiyo mara nyingi congress huwa upande wake. Amma chama cha jamhuri ni chama kilichobuniwa kutoka chama cha demokrasia,nacho ni chama cha matajiri na wenye mali nyingi,wengi katika manachama wake ni watu wenye mali nyingi,ni watu wenye mashirika na viwanda na kina

idadi kubwa ya wasomi.Wala haimaanisha kwachumwa watu wengi wala kuchukuwa watu jumla upande wake.Lau si tume ya uchaguzi wa uraisi kuisaidia haingefaulu kuchukuwa uraisi kabisa,hakika hichi ni cha cha watu wachache wala si chama cha wengi.

Marekani kama serikali nyengine zilizobakia za kirasilimali yatawaliwa na watu wa mashirika ya uvumbuzi na wenye kazi,nao ndio wenye athari katika siasa yake.Isipokuwa kwa kuangalia kwamba kila mmoja afurahi kikweli kwa haki ya raia na aweza kuathiri katika utawala,sawa iwe ni upande wa uchaguzi,au upande wa kuhesabiwa,hakika hakika hudhihirisha katika utawala wake kwamba ni utawala wa raia wote zaidi ya serikali zilizobakia za kirasilimali.kwa kuangalia utajiri wake ulio unaotiririka usio kauka,kwa kuangalia wingi wa wanaume wasomi wenye thakafa na mufakirina,kuangalia katika hali (uhuru) na hali ya uchangamfu unaoidhibiti,hakika nguvu zake ni nguvu za kihakika sio nguvu za dhahiri na kwamba ikiwa sio taifa la kale kuweko na maana ya watu binafsi na makundi katika maeneo tofauti,lakini uraia na uzalendo unawaunganisha kwa kweli katika fungamano lenye nguvu.Hata mgeni anayeishi miaka michache kisha achukuwe uraia na awe na haki ya uzalendo,awe na pupa na serikali,raia na maslahi yake zaidi ya pupa na taifa lake la mwanzo.Hili limetokana uwezo inaosherekea biladi kwa watu wake na katika mahusiano baina watu.

Amma siasa zake za nje,nazo ni siasa za matajiri na watu wenye mashirika ya uvumbuzi,yaani ni siasa za kikoloni tupu,hazina nafasi ya thamani ya juu,pamoja na kile wanachodhihirisha wanasiasa wake katika upungufu yakurubia kuwa mpumbavu mara nyengine,hakika wana

undani wa kufikiria kwa namna ambayo yazidi wanasiasa wengi ulimwenguni,wanafurahiya kwa uwezo mkubwa kwa wepesi wa kuleta mabadiliko,sampuli ya mbinu na kutatuwa matatizo.Huenda msukumo wa kikoloni katika upande wa thakafa ya juu,una athari katika uchangamfu wao wa kisiasa,nao wanaangalia ulimwengu uliobakia kuwa shamba lao,katika serikali zilizokuwa kubwa kuwa hazistahiki uwezo wanaoufurahikia na kwamba sasa ni ajiuzulu,kupumzika na kuridhia nay ale walioko nayo ulimwengu uliobakia katika kunyenyekea kwa udhibiti wa wenye nguvu.

Marekani leo yamiliki kiwanda kikubwa cha silaha za kinuklia za ya wanavyomiliki serikali nyengine za nuklia zilizo kusanyika mara nyingi.Utowaji wa kijeshi wa Marekani ukilinganisha na serikali kubwa nyengine hudhihirika wakati kuzidi Marekani kwa serikali hizo,katika mwaka wa 2002 M ulikuwa utowaji wa kijeshi wa serikali kubwa za kimagharibi kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Uingereza | Dolari bilioni 35 |
| Ufaransa | Dolari bilioni 32 |
| Ujerumani | Dolari bilioni 23 |
| Jumla | Dolari bilioni 90 |

Amma Marekani peke yake imetowa dolari bilioni 350,haya pamoja na tafauti ya sampuliya silaha na kauli ya baadhi ya wasomi kwamba Marekani imeizidi Ulaya katika kwa makumi ya miaka katika kutangulia kwa teknolojia.Yaidhibiti umoja wa mataifa na mashirika yanayotokana nayo,imeshika fungu kubwa katika benki ya kimataifa na shirika la fedha duniani kwahiyo basi imeshika nguvu za kisiasa pana kinachotekelezwa benki ya dunia na shirika la fedha kwa serikali za ulimwenguni.Vile vile ikapanuka Marekani kwa

kuimarika bishara yake kwa njia ya siasa ya utanda wazi uliomuandalia shirika la biashara ya kimataifa,ikawa ataifanya kuwa ni njia katika njia ya zake,za kuingilia katika masoko ya kimaeneo kwa hoja ya ushuru mmoja wa forodha,ikatekeleza hilo kwa kuikomboa biashara, kwa hukmu kwamba amiliki uweza mkubwa wa kiuchumi na kwa hukmu kwa mbele yake kuna idadi kubwa ya mashirika ya jinsi tofauti au yanayovuka bahari,hakika amefaidika na bima inayotolewa na shirika la biashara la kimataifa kwa Marekani katika kufungua masoka yaliyokuwa kama yaliofungwa au usugu wa kuunganisha katika uchumi wa kilimwengu ulioko wazi anaosimamia Marekani.

Uwezo huu mkubwa wa kijeshi,kisiasa na liuchumi wa Marekani umeifanya kuingilia katika jumla ya serikali zilizopo katika ulimwengu wetu leo na kuifanya ni sehemu ya siasa ya maeneo kwa serikali zote ulimwenguni.Zajaribu kutekeleza siasa ya kuhukumu serikali jumla bila ya kubagua,hakuna tofauti baina ya serikali zilizoendelea na zilizoko nyuma.Pamoja na kuhindwa kwake mara nyengine katika kuhukumu huku,isipokuwa haiwachi mahali anapopahukumi.

Basi Marekani ina mchangio katika matatizo yote yaliopo ulimwenguni,ndio inayowasha moto mkali katika maeneo yaliowashwa moto,akaingiza utunzi mpya serikalini mfano wa istilahi ya serikali za mkondo wa shari na istilahi ya serikali zinazochunga ugaidi au yanayo fanana na hayo katika utunzi ambao haiku salimika na madhara yake mpaka serikali ambazo ni washirika au serikali zinazo fatana na hazo,bali iliwajibisha ulimwengu imma uwe pamoja naye au uwe na ugaidi,amma kutokuwa na wao au kutokuwa na ugaidi haiwezekani.

Hakika imeleta matatizo na kuleta mivutano,hisha baada ya hayo huendesha mivutano hii,kuzitafutia suluhisho,ikifanya yote kwakuzingatiwa kuwa ni sehemu katika mikakati yake ya kuuhumu ulimwengu.
Imenyonya Marekani kwahiyo ikamjenga kijeshi na kisiasa katika vitendo vyake vya kisiasa unyonyaji mbaya,kwa namna ambayo hakujifunga nguvu zake upande wa kiuchumi na kibiashara,kama hali ilivyo katika serikali zinazofata ukoloni kikawaida,bali imeeneza nguvu zake katika Nyanja jumla za maisha ya kiraia kwa namna ambayo ilikuwa na nguvu katika upande wa kielimu,vyombo vya habari,jamii,fikra,thakafa na usalama.
Katika masomo jukumu lake limekuwa wazi katika kubadilisha mitaala kwa namna ambayo italingana na anavyo kiaidilojia.Kwahiyo tukapata serikali za kiarabu kama Saudia,Kuwait,Jordan,Misri na nyenginezo,imebobea katika kuangalia upya mitaala yake kwa hoja ya kuendelea na kulingana na zama, ikabadilisha Saudia masomo muhimu ya kidini katika vigawanyo walivyoviandika vya chuoni nacho ni kigawanyo cha ((al walaa-u wal baraa-u)) ikabadilisha Jordan, Misri,Kuwait na zikabadilisha serikali nyengine, masomo yanayohusiana na kupambana makafiri wanaovuka mipaka miongoni mwa mayahudi na manasara kupigana nao na yanayofanana na hayo katika fikra za kiislamu anazozichukia Marekani.
Katika vyombo vya habari Marekani wametowa mamia ya mamilioni ya dolari kwa ajili ya kuathiri vyombo vya habari katika jumla ya waarabu na waislamu,ikaanzisha ((Radio sawa)) na stasheni ya roninga ya ((Uhuru)) ili

kueneza sumu zake ndani ya kila nyumba katika biladi za kiarabu.

Katika upande wa kijamii Marekani ikasisitiza juu ya mwanamke,kwa kumueka mbali na thamani ya kiislamu,kuvizia mali,kutia shinikizo katika serikali kwa kuweka makongamano ya mwanamke,akaweka shinikizo kwa kumtia mwanamke serikalini na bungeni,ikaenea fikra ya uhuru wa mwanamke upya kwa sura mpya na fikra mpya.

Katika upande wa fikra na thakafa imekusanya Marekani vituo vya fikra, demokrasia,vyama vingi,ikabuni mashirika ya haki za wanadamu,kwa namna ambayo vikawa vituo na mashirika haya yaeneza fikra za uhuru kwa ufahamu wa kimagharibi,kwa njia ya kimarekani,ikategemeza mashirika haya na vituo hivi kwa filamu za *Hollywood* na uzalishaji wa fani za kiteknologia zilizoendelea,zinazo dhibiti kueneza vipindi vingi vya roninga za kiarabu na zisizokuwa za kiarabu.

Amma upande wa usalama ilichofanya Marekani kufungamanisha vitengo vya kijasusi katika serikali za kiarabu na serikali zilizopo katika ulimwengu wa kiislamu na vitengo vyake vya kijasusi na haswa kitengo cha CIA na FBI,mpaka tumekuwa twaona ziara za majasusi wa Marekani katika miji ya biladi za kiislamu wakiwa na uhuru kamili,chini ya ulinzi wa kanuni kama hali ilivyo Sudan,Yemen,Kenya,Tanzania,Libya,Pakistan na serikali nyenginezo.Kumekusanya kufunga huku kwa kijasusi kusalimisha wanaotakikana kwa Marekani,ikaruhusu kuweko vikosi vya Marekani haswa kwa kazi maaluma ya anachokiita Marekani kuwa ni magaidi.

Hivi ndivyo zilivyokuwa neema za Marekani hunyosha viungo vyake maishani katika mujtama za biladi za kiislamu na katika mujtama za biladi zisizokuwa za kiislamu,ukaenea humo ufisadi kama apendavyo.Nayo ni kama afanyavo Mahariki ya kati,Afrika na Kusini mwa Asia,mpaka Latin Marekani ilipomuangusha kiongozi wa Haiti aliechaguliwa Aristide na kumhamisha nje,yenda mbio sasa kumuangusha Chavez raisi wa Venezuela kutoka utawala.Kwahiyo ikawa Marekani yamakinika katika kuzikomboa serikali dhaifu kwa sababu ya kunyenyekea watawala wake na kujidhalilisha kwake.
Lakini kudhibiti huku kwa Marekani hakutodumu mda mrefu,yaelekea kuondoka,juu ya kuonekanwa Marekani kila pembe ya ardhi na juu ya kuwa kusaidiana watawala na tawala na kuwepo huku,isipokuwa kuzidi chuki ya mataifa haswa ya kiislamu kati yake dhidi ya Marekani na kukuwa kwa chuki ya wengi wakiwemo wamarekani kwa sababu ya kujiona kwao na kibri chao na kupendelea kwa Mayahudi.Kwa sababu ukoloni wao na utumwa wao kwa wengine,twasema: Hakika kuzidi huku kwa chuki na kukuwa kwa chuki kutaleta mpambano na mvutano dhidi ya kuwepo kwa Marekani kila mahali sawa iwe ndani ya bara lake au nje yake.Huongezewa juu ya hao kile kilichoswibu serikali kubwa nyengine katika dhiki na pigo la maslahi yao kwa sababu ya kijinaki Marekani na kunyakuwa manufaa peke yake na kujaribu kwake kudhibiti koloni,pia kujaribu kwake ukiritimba wa kimarekani katika kusimamia mambo ya kimataifa.
Hakika kuwepo kwa serikali inayo tabani mfumo wa kirasilimaliuliosimama juu ya ukoloni na kunyonya damu za wengine,kusimama serikali hii mbele ya ulimwengu pasi na kupata nguvu sawa nyengine inayopambana nayo

katika kuupeleka ulimwengu,kinachofanya ulimwengu kuwa katika mateso yakuendelea, matatizo yanayofuatana na kufuatana misiba.Kinachoshuhudiwa kwa kuhisiwa katika uharibifu na kuharibu Marekani ulimwengu na kuzusha matatizo yanayofatana kwasisitiza hilo.

Hayataondoka mateso ya ulimwengo na ubaya wake yanayotokana na serikali za kirasilimali na haswa Marekani,hayataondoka mateso haya isipokuwa kwa kusimamisha serikali ya khilafa itakayo tabikisha mfumo wa haki,uislamu mtukufu alioteremsha Allah kwa mtume wake (s.a.w) rahma ulimwenguni,hapo ndipo utakapofichua uadilifu wa uislamu uovu wa urasilimali na fikra yake ya kimada na njia yake ya kikoloni.Vile vile itamaliza nguvu ya uislamu ilio bora dhulma za Marekani na kiburi chake,kuilazima kujiondoa kwake,ulimwengu wake mpya kibakia na ulimwengu mpya kisha ienee kheri kote ulimwenguni,kupumua ulimwengu na matatizo baada ya kukumbana kwa mda mrefu na shida na mateso.

**5-Amma taifa la Uingereza,**hakika viwanda vya samaki na majahazi vimemzidia tangu kuinukia kwake,kisha kukapatikana kwake ubaharia na biashara ikapatikana kawaida ya kutafuta manufaa na kuyatumia na kawaida ya mfanyi biashara.Kwa kuangalia udogo wa biladi yake ikawa ni lazima kutaka msada kutoka kwa wengine,jambo la wavuvi wanaosaidiana baharini,ni kidogo kutoka peke yao. Kisha ukaja mfumo wa kirasilimali wakauingia na kukita kimanufaa.Kwahiyo utapata maisha ya uingereza kisiasa tangu ilipopatikana hadi sasa imesimama juu ya kutegemea wengine,kuandaa ladha kila anapotaka kushika kitu sawa iwe ni biladi kuikoloni au serikali atake msada kwake.Basi ikasimama

siasa yake yote juu ya mikataba,makundi,kushirikiana katika ukoloni na kwa ajili hiyo katika karni ya kumi na tisa zikashirikiana serikali nyengine katika ukoloni na kuwacha mkono wake ili kukoloni baadhi ya biladi ili ziwe upande wake kutetea maslahi yake. Kwahiyo ikaitia Ufaransa Mashariki ya kati baada ya vita vya mwanzo vya dunia,ili iwe upande wake inapopatikana hatari katika maeneo,na kuiweka mbele yake mpaka ikasemwa:Hakika Uingereza hupigana mpaka mwanajeshi wa mwisho wa kifaransa.

Hivi ndivyo tabia ya mvuvi wa samaki zilipatikana kwake tabia za kutaka msaada ili kufikia maslahi yake.

Kisha kuna tabia nyengine aliojulika nayo Uingereza,bali ni katika tabia muhimu,nayo ni kushikana yakale na kutozi kuibadilisha au kuindeleza isipokuwa polepole na itakapokuwa hawezi kuepukana na mabadiliko,basi taifa Uingereza ni taifa la kihifadhi kikweli.Nayo tangu zamani hadi sasa yadhibitiwa na jamii kongwe,matajiri na wenye rasilimali kubwa,juu ya madai yakuwa yaenda kidemokrasia na kwamba ni taifa la kidemokrasia,lakini kwa kuangalia kwa makini yabainika kwamba sio hivyo na ni taifa lisilo na athari yoyote katika kuleta viongozi,bali anayenasibisha kiongozi ni jamii tukufu na wenye ukiritimba na si raia,wala hakuna tofauti katika hilo baina ya zama zilizopita na zama zilizopo, hakika bado mpaka sasa kama ilivyokuwa zamani ikihukumiana mwishowe na jamii na warasilimali.Ilikuwa tangu zamani hupambana na kila harakati ya kitaifa inayoinukia Uingereza mpambano muovu,kuimaliza kwa mbinu ya jinsi yake. Mapinduzi ya Cromwell inayojifakhiri nayo Uengereza sio mapenduzi ya raia bali ni mapenduzi ya jamii tukufu juu ya mapenduzi ya kiraia.Imetekeleza

mapenduziya kiraia wakati huo ikitaka kumuondowa kiongozi wa jamii tukufu ya kirasimali,yakakurubia mapenduzi haya kufaulu,ikakurubia kuwa na jamii tukufu ikamtuma Cromwell kutekeleza mapinduzi akidai baadhi ya haki,wakamzunguka wengi yakapikana baadhi ya madai,akayamaliza mapenduzi ya kiraia na kuimaliza kutoka msingi wake.Kinachotawala Uingereza tangu miongo ya miaka ni chama kihafidhina *(Conservative)* na hakikuwa chama wafanyikazi isipokuwa ni chombo kinacho letwa inapolazimu haja ya Uingereza,au pindi kutakapokuwa na mambo yatakayoshinda chama cha kihifadhina kuyatatuwa,basi huitwa chama cha wafanyi kazi kimsahilishie kutatua.Yaonesha kwamba viongozi wa chama cha wafanyi kazi mwishowe walijuwa uhakika huu wakajaribu kukabiliana nayo,ikawa mzunguko wa vyama viwili kwa utawala uko karibu na kubadilishana zamu baina ya kihifadhina na wafanya kazi,kikiwemo chama cha wafanyi kazi kuwa ni chombo mkononi mwa kihifadhina.Kwahivyo twapata kwamba Tony Blair kiongozi wa chama cha wafanya kazi sasa waziri mkuu wa Uingereza amebadilisha tabia ya chama na kukurubia sana siasa za chama cha kihafidhina,ikadhihirika katika sura ya siasa kwa njia isiotafautina na sura ya vigogo vya chama cha kihifadhini,mpaka ikafamfanya Margaret Thatcher aliyekuwa kiongozi wa chama cha kihafidhina, kuwa ni kielelezo chake katika siasa ya ndani ya nje.Kikawa chama cha wafanyi kazi pia hakitafautiani sana na chama cha kihafidhina,vikawa vyama hivi viwili Uingereza ni mifano miwili ya chama cha jamhuri na chama cha demokrasia Marekani.

Chama chenyewe cha wafanyi kazi kitakapo pata watu wanaodiriki yaliyo na katika kutawaliwa na jamii tukufu

ya kurasilimali humo,hakika watu hawa watawekwa katika dhurufu zitakazo waeka mbali na kuathiri katika chama hatimaye kuathiri kisiasa.Mwanachama wa wafanya kazi Bevan katika thalathini hadi miaka ya sitini George Brown katika miaka ya sitini,ni mfano bora katika kutawala chama cha kihafidhina mpaka chama cha wafanya kazi,juu ya kutengwa wale wanaotaka kiwango cha kudhibiti nguvu ya utawala katika utawala.Chama cha kihifadhina chenyewe hakichaguwi uongozi wake kabisa,bali huchaguwa kiongozi alietangulia,kama ilivyo tokea na Macmillan alipomchaguwa Lord Hume na Margaret Thatcher alipomchaguwa John Major.Hata kama amemchaguwa Heath na Major kabisa lakini ni uchagusi wa kisura huwa amechaguliwa kwa mara ya kwanza kisha ukapita uchaguzi wa sura.Kufikia hapa hakika nidhamu ya kiutawala Uingereza,hata ikiitwa ya kidemocrasia,lakini uhakika wake ni kuchaguliwa na kuchaguliwa kwa tabaka maalumu na anayechaguwa ni jamii tukufu ya kirasilimali na wenye ukiritimba.

Kwa kuangalia Uingereza ni kisiwa katikati mwa bahari,hakitoshelezi kisiwa chake wakazi wake kwa maisha yao.Kwa hiyo kumekuwa kutoka kwao kisiwani ili kutafuta maisha ni jambo lisilo kimbilika.Isipokuwa hata hata wakitoka kwa ajili ya biashara,hakika huwa wametoka kwa ajili ya kukoloni sio kwa biashara wametoka kunyonya damu za raia na kunyakuwa mali zao sio kutaka kubadilishana mali,hilo ni kwakuwa hawakuwa mara ya kwanza na mali ya kubadilishana nayo basi wakatoka kutaba mali.Hii ndio iliokuwa hali yao tangu kutoka kwao kisiwani,walipojiunga na mfumo wa kirasilimali na manufaa ni sehemu isioepukana nao,unaokubaliana mfumo huu na tabia yao,basi

ikamakinika upande wa kikoloni ikwa ni serikali ya kikoloni daraja ya kwanza.Kisha walipokuwa kiidadi ni wachache,wala hawawezi kusimama mbele ya nguvu iliyowazidi walijiokowa kwa kudhalilisha raia wengine na serikali nyengine kumsaidia,wakaweka misaada hii kwa niundo ya vyama mfano wa miungano,makongamano na mikataba.Kwahiyo upande wa kivyama ni sehenu isiojitenga katika siasa yao.Nao hata kama katika werevu ni watu wa kawaida kama raia waliobakia lakini wanatumia werevu wao kwa kiwango cha juu,kwahiyo wakadhihika katika kufahamu kwao kazi,kufahamu kwao siasa na katika kutatuwa matatizo wakapatikana na akili ya kutatuwa matatizo kwa namna ya wazi.Kwa kuangalia haja yao kubwa ya kupanuka wakaweka viwanda vyao kwa msingi wa kiwanda cha kivita,kilichopelekea kujenga serikali kikweli wakifurahia ile nguvu ya kivita,ala za kivita,wakifurahia ile nguvu ya kiviwanda,mpaka ujuzi wao wa kindani katika siasa,utawala na wanachofurahia katika ujanja unaosifika mara nyingi kuwa ni uovu.

Amma siasa yao ya nje hakika hii yasimama juu msingi wa kikoloni,lakini hudhihirika mambo mawili:Kwanza kuhifadhika kwa usawa wa kimataifa,pili kuhifadhika kuweko kwao katika siasa ya kimataifa namna itakavyo wakalifi thamani.Kwahivyo katika vita kimsalaba walishiriki kwa sura ya wazi,katika muungano mtukufu wakawa ni yenye kujitokeza katika serikali kubwa,alipo tokea Napoleon na ukombozi walikuwa katika upeo wa vikosi vyake vilivyomvunja na kumrudisha mfaransa alipotoka.Ilipo harakishika Ujerumani katika masiku ya Bismarck ilishiriki Uingereza katika kongamano la Berlin,ikawa katika malengo yake in ule ukali wa nguvu za Ujerumani,ilipohisi kwamba kuna kukuwa

kusikokuwa kwa kawaida katika nguvu za Ujerumani,akamtangazia vita,akampiga katika vita vya kilimwengu mara mbili,akajaribu kuuvuta ulimwengu wote kuwa katika vita vya kilimwengu ili kubadilisha ramani ya ulimwengu na kwa ajili ya kudhoofisha wababe wawili wakati ule,waliokuwa wakitawala ulimwengu wakati ule,wakati wa kipindi cha makubaliano.Ilipotengwa na siasa ya kimataifa mkataba wa wababe wawili ikawa kama iliyokosa muundo wake ikawa yenda kiubaguzi huku ikijaribu kuwa na mshikamano kwa ajili ya kurudi kuwepo kimataifa na kushiriki katika siasa ya kimataifa.Nayo yategemea kuweka mikataba na serikali, kutafuta watu na kuathiri nao wala haijali kulisha mtesi chakula kikubwa katika njia ya maelewano,naye hajuwai katika siasa rafiki wala adui,bali yajuwa maslahi wala haijuwi jengine na kinachoitwa maadili ya kiamatifa hukichulia kuwa ni chombo cha kuhadaa wala haiamini kuwepo kwake.Kwa urongo hata kama atadhihirisha ili kupatikana uaminifu nao,lakini ataufanya ni silaha yay a kuathiri katika siasa yake.Akawa Churchill waziri mkuu wa Uingereza katika mkutano wake na Roosevelt na Stalin kufanya utafiti wa jambo la vita hali ya baadaye ya Ujerumani,ikawa katika yale aliowaambia kwa upeo wazi ni: "Hakika katika vita vyenye thamani hadi ni kwamba ni lazima kuhifadhika urongo kwa pupa kamili " hii yaonekana kuwa kiwango chochote kinachozingatiwa kuwa ni urongo wa kimsingi katika siasa ya Uingereza.

Hii ndio hali ya Uingereza na hali ya siasa yake.Muamala wake lazima uwe juu ya msingi wa kuwa ni serikali ya kikoloni,juu ya msingi wakuwa yanyonya raia wake wala haikuweza miaka na matukio kubadilisha njia yake hii na

kwamba ilipangia mapenduzi ya raia walioyatekeleza mpaka hawakuwacha mapenduzi kufaulu.Kwahiyo kupambana na ukoloni wake hukutokei isipokuwa kwa kujuwa njia zake,kwa makabiliana ya wazi yalioambatana na uhodari unaoonekana kuwa ni ujinga,wa mbinu zilizofichika.Nguvu zake katika biladi zake zimemakinika katika kauli ya mshairi:"na nitibuni kwa yaliokuwa maradhi" na nguvu zake nje amemakinika katika kumdhalilisha mwengine,mpaka wale wanaopambana nao. Wala hakuna njia ya kumshinda isipokuwa kwa kumuondoa kutoka silaha zake za siasa yake ya jadi na makabiliano ya kipeke yake bila wakumnusuru au mshirika.

**7-Amma taifa la kifaransa:**Ni taifa lililojenga serikali yake tukufu kati kati ya Ulaya,lajifahiri juu ya serikali nyengine za Ulaya kwamba taifa la Ufaransa ndilo lililokuja na fikra za juu kama uhuru,uadilifu,uswa na maarufu kwa ndilo lililo towa watu wakipekee katika siasa na fikra,nalo kwa namna yoyote ni serikali ya kikoloni,yatafautuana na nyenginezo kwa kuathirika na fikra za uhuru,kwa kusifika kuwa ni sifa ya kibinafsi kwake,iliyobadilika katika umbile miongoni mwa maumbile,bali tabia katika tabia zao.

Taifa la Ufaransa tangu lilipofanya uhuru kuwa ndio fikra yake iliendelea kugawanyika,ikawa karibu kuwa mkusanyiko wa watu wake badala ya kuwa umma au taifa au kundi.Kwahiyo zikakosekana serikali zenye nguvu,ikakosekana kuitawala serikali yenye nguvu,kwa ajili hiyo ikawa rahisi kwa Uingereza kuitumia Ufaransa mara kwa mara.Kwahiyo hakika Ufaransa baada ya kuondoka Napoleon hadi zama za de Gaulle,nayo yafuata Uingereza.Hiyo ni sababu ya kumakinika fikra ya

uhuru,mpaka walipotoka ili kuikoloni Marekani,Urusi na Afrika,hakika ilitowa Uingereza ili ipate nguvu,hata ikidhihirika kwamba msongamano baina serikali mbili ndio kinachoelea juu juu ya tarikhi ya ukoloni ya biladi mbili.

Juu ya hayo hakika mtu hawezi kuhukumu taifa la Ufaransa kwa sifa moja inayozidi sifa ya uhuru.Kwakuwa uhuru wa fikra ulileta wanafalsafa,washairi, mufakirina na wengineo.Uhuru wa kisiasa ulileta karama,utukufu na uaminifu wa nafsi,ukaleta kundi kubwa la watu wa kipeke yao.Uhuru wa kibinafsi ukafanya Paris kuwa maeneo ya uchafu,uovu kwa kikimbilia na matamanio na ladha.Uhuru huu ndio ulioleta mwanya wa kuingia wageni humo haswa Uingereza.Kwahiyo huchukuliwa uhuru kwa maana yake kamili ndio msingi wa balaa Ufaransa.

Wala hawezi mtu kusema kwamba Ufaransa kuna vyama kadha na kwamba chama fulani ni kadha na chama fulani ni kadha,hakika ni vigumu bali anayeomba radhi kwa raia,hili ni jambo lake,kwamba kupatikane vyama kwa maana ya chama,bali hupatikana mkusanyiko wa watu wanaojiita vyama.Kufikia hapa ni vigumu kupatikana utawala utawala wa nguvu au utawala uliomakinika, kwa hakika kila mfaransa ajitawala mwenyewe na kilamfaransa atumai kuwa mtawa,kufikia hapa hawezi mtu kusema kwamba siasa ya kindani ya Ufaransa ni kadha na siasa ya kifaransa nje ni kadha.Basi siasa ya kindani itakuwa kulingana na hali ya watawala,kulingana na ufahamu wao wa uhuru na siasa ya nje yenda kulingana na uwezo wa Ufaransa wa kushinda wengine ili kuwatawala na kunyosha nguvu zake kwake.Huzingatiwa Ufaransa kuwa ni serikali ya

kikoloni. Kwakuwa ilijiunga na mfumo wa kirasilimali.Basi manufaa ni ya kimsingi katika maisha ya kifaransa.Kwahiyo ndio ikawa na pupa ya ukoloni na kuwa na pupa ya kubakia koloni hizo.

Kama ni lazima kupawa fikra juu siasa ya Ufaransa ya nje,hakika yaonekanwa siasa yake imejengwa juu ya msingi wa kujipatia nguvu za nje sawa iwe ni kwa koloni,nguvu za kithakafa au nguvu za kiuchumi.Matendo yake ya kisiasa dhidiya serikali kubwa hakika yapata kuuza watu wake,kushiriki katika utukufu,udhibiti nayo haijui kuzuka kisiasa,bali zaidi hutumia makabiliano mara nyingi.Kwahiyo ni rahisi kugunduwa mvutano baina yake na Marekani katika masiku haya,wakati ambapo yasumbuwa kuigunduwa na nyengineo haswa Uingereza.Kwahiyo njia inayofuata katika kukabili matendo yake ni kutolaumu kubwa wake,kutomakinika kuchukuwa uongozi,kutoizingatia kuwa ni serikali kubwa isipokuwa kwa kiwango wanachokikubali serikali kubwa katika siasa ya kimataifa.

**7-Amma taifa la Urusi:**Ni taifa lenye uchangamfu,lina uchangamfu na nguvu, lakini wana wepesi na usahali na hata kama wamejiunga na mfumo wa kirasilimali kwanza,kisha ukoministi pili,kisha ikarudia mfumo wa kirasilimali,isipokuwa ilibakia kuwa nyuma ya Ulaya,wala haikufika daraja ya mataifa ya Ulaya yakawa kwa Urusi ni kizuizi cha upungufu mbele ya watu wa Ulaya,kikaathiri kizuizi hichi nyenendo zao vibaya.

Taifa la Urusi ni taifa linalo pigana,shujaa katika biladi yake,linapotoka biladi yake hukosa sifa zake,kwahiyo hutarajiwa kukosa udhibiti wake katika serikali za mashariki ya Ulaya tangu kipindi kirefu,hivi ndivyo ilivyokosa kihakika baada ya kukosa kwake muungano

wa kisovieti.Uhakika wa tarekh yahakikisha kwamba halikushinda nje ya biladi yake  katika matukio yote ya kitarekh,tatizo la Chechnya biladi ndogo lathibitisha hivyo.Wakati ambapo ilikuwa ikshinda maadui zake wakati alipokuwa akivamia ndani ya biladi yake na katika ushundi wake mashuhuri ilipokuwa ikivamia ndani ya biladi yake ni yaliotokea na Napoleon na Hitler.
Nidhamu ya kiutawala ya Urusi wakati wa makaisari sio ile ya wakati wa ukoministi na sio ile ya wakati wa sasa,isipokuwa katika hali zote za ugandamizi, alikuwa kaisari akitegemeza kwa sura haswa ubepari wa ardhi,wakawa wakubwa wa kubinafsisha ardhi na kwa njia ya mkataba na matajiri wakubwa wanaodhibiti biladi kudhibiti kwa mabwana,wakawa wanaunga mkono  siasa ya kikaisari ya kindani na nja kikamilifu,wakawa hawa wote wakiwanyanyasa raia vibaya, kilichopelekea kuporomoka kwa biladi na kurudi nyuma raia.
Ilikuwa Urusi kabla ya vita vya kwanza vya dunia imerudi nyuma kuliko Ulaya ikinyonya kutoka baadhi ya serikaliza Ulaya.Vile viwanda vya kimsingi Urusi vilikuwa katika mikono ya Ufaransa,Uingereza na Ubelgiji.Basi ikawa mitambo muhimu ya kuchimba madini iko katika mikono ya wafaransa,ikawa kiwanda cha makaa katika bondo Donbass kiko katika mikono ya wageni,ikawa karibu ya nusu ya visima vya petroli viko katika mikono ya Uingereza na Ufaransa,kikawa kiwango kikubwa katika faida ya viwanda cha Urusi huenda katika benki za kigeni,haswa benki za Uingereza na Ufaransa,zikawa biladi mpata mwaka wa 1914 M zimerudi nyuma katika nidhamu ya kiutawala,kiuchumi,kithakafa na kielimu pamoja na hayo ikawa Urusi ni serikali kubwa na yazingatiwa kimataifa

kuwa ni serikali kubwa na ikawa ina athiri katika siasa ya kimataifa.Kiliposhika chama kikoministi uongozi,haikubadilika hali ya uongozi isipoluwa katika mbinu. Wakasimamia wakoministi uongozi wa biladi kwa chuma na moto,kuuwa na umwagaji wa damu,mateso na ugaidi,wakamakinisha utawala wao na makovu ya raia.Wakaweza kulazimisha serikali ya kwanza kuwacha fikra ya kuipiga,wakaingia katika mikataba nayo hadi ikawa mshirika wake au kama mshirika,kwahiyo ikawa Urusi (muungano wa kisovieti) ni mshirika wa serikali ya kwanza katika kupeleka ulimwengu,bali hakika ulimwengu wote watawaliwa na wababe wawili Urusi (muungano wa kisovieti) na Marekani.Amma siasa ya Urusi ya kikoministi ilikuwa imesimama juu ya fikra.Basi fikra yake ni kueneza ukoministi na njia yake ya uharibifu,kuvunja na kubomoa,kuleta mgongano nayo hujaribu kila mara anaporuhusiwa kuingia ukomonisti katika baadhi ya serikali,kama inavyojaribu kudhibiti serikali ambazo nidhamu ya kiutawa kwao ni nidhamu ya kikoministi.

Amma baada ya kuporomoka ukoministi limepatikani taifa la Urusi lenyewe na viongozi wake kuwa na haja ya utambulisho upya unaotafautiana na Urusi ya kikaisari,mabadiliko ya muda wa kikoministi,basi wakarudia urasilimali,ikawa yajilinda kutokana na joto kwa motoufakiri ukazidi,ikatingishika sura ya Urusi na kutetemeka kituo chake ulimwenguni.

Imekuwa nidhamu ya kiutawala Urusi ni ya kirasilimali,ikawa yafanana naya wakati wa kaisari,pamoja na kuhifadhika baadhi ya alama zake kwa muda ule wa ukoministi,ikarudi tabaka ya kirasilimali na mapinduzi makubwa,wakawa na athari yao katika

utawala kikamilifu kama ilivyokuwa hali katika zama za kaisari, lakini mara hii badala ya makaisari ikawa Urusi yatawaliwa na majasusi wa kisovieti waliotangulia KGB na wana sias waiotangulia,waliobadilisha ngozi yao wakawa warasilimali kulingana na (uvumbuzi) mpya.
Amma siasa yake ya nje imekuwa ni mwenye kumakinika kuwa na majukumu peke yake,pasi na kuwepo na mtizamo wa kilimwengu katika siasa ya nje.Kwahiyo ikadhoofika kuwepo kwake katika eneo la kilimwengu ikawa atafuta peke yake kuwa na jukumu lolote na asiwe nyuma mwishoni katika siasa ya kimataifa.Hali hii ya kukosa utambulisho wa fikra ya kiitikadi mbele ya taifa la Urusi na hali ya kufilisika kisiasa kwa kiwango cha watawala na raia wa kirusi,huipa fursa ya kusimama mbele ya siasa za kirusi kwa kupatikana mahusiano ya jibiashara na Urusi kumakinika waislamu kuingia Urusi,kumakinika Urusi kuuona uislamu kuwa uko hai katika mahusiano ya watu,kuwa kupambana na majaribio ya Urusi katika kuathiri siasa ya kimataifa kwa kutoipa fursa ya hilo na kufunga nayo mahusiano upande wa kibiashara na kukadiriana katika nyanja zilizobakia kama serikali nyengine za kirasilimali.Kwakuwa siasa yake ya nje imejengwa juu ya kupora na ukoloni,hata kama haya hayadhihiri isipokuwa katika serikali jirani.
Hakika mataifa manne ya mwisho:Taifa la Marekani,Uingereza,Ufaransa na Urusi ni mataifa ya serikali zinazo tambulika kwa sasa kuwa ni serikali kubwa zenye tamaa ya kutawala katika siasa ya kimataifa maeneo tofauti ulimwenguni,kuyazozania pamoja na tofauti walionayo ya nguvu na udhaifu.Kwa kufatilia athari zake za siasa ya kimataifa karni hii ya ishirini na

moja milady, twaweza kujumlisha kiufupi siasa ya serikali hizi nne kama ifuatavyo:

**Amma Marekani:**Zimekuwa nguvu zake kwa njia ya haraka haraka tangu kuanguka serikali ya muungano wa kisovieti kighafla ikawa serikali kuu yenye nguvu za kuathiri ulimwengu,haswa na kwamba pengo ililoliwacha muungano wa kisovieti haikumakinika serikali yoyote kubwa kulijaza,mpaka ikawa Marekani ndio serikali kubwa pasi na mvutano,haikumakinika mpaka sasa serikali yoyote katika serikali kubwa zilizopokuinula hadi daraja ya pili inayo ishughulisha muungano wa kisovieti.Hali hii mpya katika hali za kimataifa,iliomakinisha Marekani katika kuwazidi wengine,iliwapelekea wanasiasa wa kimarekani kupendelea kutukuka na kujinaki katika kuamiliana na wengine na huenda waziri wa mambo ya nje wa Marekanizama za Clinton Bi Madeleine Albright akielezea kuhusu hali hii katika maneno yake akisema: "Hakika Marekani ni (umma-dharura)nayo ndio yenye majukumu ya kilimwengu,iko tayari kufanya kila kitu,wakati wowote itakao na wajuwe wote kwamba sisi twafanya tutakavyo na twabadilisha tutakavyo wala havisimami njiani mwetu vizuizi.kwakuwa ulimwengu mzima ni wetu,ulimwengu wa wamerikani".

Huku kujinaki na kujigamba katika siasa ya kimarekani kulisababisha mpaka watu wa Ulaya waliokuwa washirika wake kuwa hawatoweza kujikuza kwake ulimwenguni,wala matamko hayo kwa sauti ya juu ya Marekani ya kujitukuza. Kwahiyo wakamrudi wakati wa magazeti yao iliokuwa ikieleza kisumbuka kwao,likasema gazeti la kifaransa(Le Monde diplomatique) kurudi tamko Albright: "Hakika kudhibiti kwa Marekani hakufai kuwa

kiwango mambacho hakina budi,hakika ni juu ya Marekani kufahamu kutoka sasa na kuendelea kwamba haitokuwa kwa uweza wake kulazimisha kanuni zake kwa mabara matano kulingana na maslahi yake peke yake,kama ambavyo haitokuwa (askari wa ulimwengu) katika maeneo ya mivutano na matatizo milele".

Kwahiyo basi hakika Marekani hutoka katika siasa yake katika mtizamo wake kwamba yeye ndiye mmliki wa ulimwengu huu na mwenye haki noa na watu wake!.Yatangaza mchana wazi kwamba yeye ndiye kiongozi wa ulimwengu kama alivyosema Bush wakati wa ziara yake ya kuichanguzi wa majimbo ya Marekani katika mwezi wa nane mwaka wa 2004 M.Hutangaza vile vile miradi ya ulimwengu (ulimwengu mpya),(mashariki ya kati mpya),(mashariki ya kati kubwa)…hadi mwisho.Isipokuwa kiburi hichi na kujinaki huku kwa Marekani matokeo yake yatakuwa mabaya kwao,bali hakika matarajio ya hayo yamedhihiri. Basi hii Marekani imezama ndani ya matope ya Afghanistan na Iraq,akavunjiwa heshima yake,juu ya vitendo vyake vya kihalifu vinavyovuma bila mpango kwa raia,aliyoyafanya katika vitendo vya fedheha vya kinyama katika majela,isipokuwa pamoja na hayo imekuwa hutoa mizonga ya majeshi yake hadi kwake Marekani baada ya kuuwawa kwao Afganistani na Iraqi.Wamekuwa raia wa eneo wamejaa chuki,kwa uhalifu wao muovu uliowafika mtu,mti,jiwe,bali njia ya taalim,vyombo ya habari na fikra…

Vile vile hakika Ulaya,Urusi,Afrika yamewaumiza aliyoyafanya Marekani katika kunyakuwa mali yao na uadui wa kuendelea katika biladi na waja na kujaribu Marekani kudhibiti katika maeneo ya kilimwengu.

Namna hii hakika kinachobaisha siasa ya Marekani ni upande wa:Kibri,kujiona, fani za uhalifu na kuuangalia ulimwengu kuwa ni shamba lake.Upande mwengine: Ni chuki kubwa na hasira nyingi kwaokutoka kwa mataifa yote ya ulimwengu, katika maadui zao na katika wale waliokuwa ni marafiki zao pia.Haya yote yaashiria mwisho wa kuumiza kwa Marekani na kuanguka kwa uovu wake kama walivyoanguka wababe wote ulimwenguni.

**Amma Uingereza :**Hakika hii yaweka mguu wake Ulaya na mguu Marekani,ikizozana naye muongozo,mizozano ya Ulaya upande mwengine na *Anglo-Saxon* upande mwengine nayo huhifadhi usawa baina pande mbili.

Umekuwa usawa huu ni msingi wa mahusiano kwa wote Marekani na Ulaya,ikichangia kamba mbili na ikifaidika kutoka pande mbili,ikipata nguvu kwa Ulaya na Marekani wakati huo huo,basi haiwezi kuwacha Marekani wala kuweza kujitenga na Ulaya,lakini maslahi yake zaidi yalemea upande wa Ulaya.Kwahiyo twaipata yajikurubisha nayo zaidi kwa masiku na kuingia kwake katika muungano wa Ulaya ni dalili ya hayo.Imechangia Uingereza mwishowe kwa kuweka kiini cha jeshi la Ulaya mbali na muungano wa NATO,akafanya hayo kwa kusaidiana na Ufaransa na Ujerumani juu ya Marekani kukataa vikali juu ya hayo,hii ndio siasa ya Uingereza huko Ulaya nah ii ndio pembe inayotoka matendo yake ya kisiasa huko Ulaya.

**Amma Ufaransa :**Hili ni kinyume na Uingereza,kwakuwa husimamisha siasa yake juu msingi wa kiulaya mtupu,wala haitilii umuhimu wowote kwa Marekani, nayo yajaribu kutilia nguvu muungano wa Ulaya na yajaribu kuidhibiti ili iwe nguvu ya siasa ya Ulaya

imeungana,kando kabisa na Marekani na iwe kwa sababu ya wenza yalingana na nguvu ya Marekani,katika pande zote za siasa,uchumi, kijeshi,thakafa wala haijifungi na uchumi peke yake au kwa kusaidiana namna ya kisiasa.
Ufaransa katika kujikurubisha na Ujerumani hufanya kuwa ni jambo la kimsingi katika kuifikia siasa hii,kwa namna kwa namna ambayo imekuwa yachukuliwa muungano wa Ufaransa na Ujerumani ndio msingi wa siasa hii ya ushirikiano wa kiulaya.
Hii ndio siasa ya Ufaransa ya kiulaya,nayo halika ni siasa ya kivyake yenye changemoto za wazi,iliofanya Ufaransa na Ujerumani ndio moyo wa nguvu za Ulaya na dainamo inayoiharakisha.
**Amma Urusi:**Siasa yao sasa upande wa Ulaya yabainika katika mambo mawili:
**Kwanza:**Kuingia katika jukwa la serikali za Ulaya,kushirikiana nazo katika kutafuta mambo ya Ulaya tamko la usawa,ikafaulu kwa hili,kwa namna ambayo alimakinika kuingia katika kikao cha Ulaya,katika muungano wa nchi saba zenye uwezo mkubwa wa kiviwanda duniani lakini haikufaulu kuingia katika muungano wa Ulaya au kugombea ili kuingia humo.
**Pili:**Kujaribu kuhifadhi mahusiano tofauti na serikali zilizokuwa zamani ni sehemu ya muungano wa kisovieti,na serikali zilizokuwa zikizunguka katika mzunguko wake,kwa namna ambapo mahusiano ni usimamizi wa kudumu, ikaanguka kwa jambo hili kuanguka kubaya,ikakosa udhibiti wake kabisa wa serikali zote za Ulaya Mashariki nazo ni:Bulgaria,Romania,Czech,Slovakia,Poland, Hangary na serikali za Yugoslavia zilizotawanyika,ikaanza kukosa sehemu ya udhibiti wake

Georgia,Azerbaijan,Armania,Ukrania,Belarus,Moldovo na jamhuri za Urusi ya Kati za kiislamu,haikubakia kwake ubwana kamili isipokuwa Kazakhastan,kama ilivyokosa kabla udhibiti wake wote katika serikali tatu za Baltic nazo ni:Lithuania, Estonia na Latvia mapema.

Kwa ufupi wa siasa ya Ulaya Ulaya kwa Urusi ni kwamba haikumakinika kustahiki Ulaya kwa kiwango alichokipanga na kukikimbilia na huenda ikawa kile ambacho hakikummakinisha kwa hiloni kuwa serikali ya Eurasian yaani Ulaya ya Asia,haiwezi kudai kuwa ni ya Ulaya kamili,kisha haiwezi kukosa kujuwa upeo wake wa Asia mpana au kubainika mahusiano yake na maslahi yake makubwa na wawasiokuwa wa Ulaya,basi yashuhulika kupanga upeo wake muhimu mpana, nayo kwa hilo ababaika hawezi kumakinika katika jambo la Ulaya peke yake.

Kwahiyo tutakuwa tumeshajua mataifa ya serikali kubwa (Marekani,Uingereza, Ufaransa na Urusi) na pia (umma ya kiislamu) iliokaribu kurudi serikali yake kubwa khilafa rashida pamoja na taifa la Ujerumani linalotarajiwa kurudi kwake kama serikali kubwa hata ikikawiya.Kisha tumetaja Japan kwa athari yake kubwa ya kiuchumi.

Itadhihirika kuathirika na athari ya mataifa haya katika siasa ya kimataifa wakati wa kuweka wazi maswala ya ulimwengu mkubwa.

**1-Kadhia ya Ulaya**

Kadhia ya Ulaya ni kadhia ya ulimwengu wa mwanzo tangu karni nyingi,nayo ni kadhia yahusiana na serikali kubwa,usawa baina ya serikali hizi,yahusiana na kudhibiti ulimwengu kikoloni na upeo wake kijeshi,kiuchumi,kisiasa,kithakafa,nayo ni katika kadhia

za kitambo na ya hatari sana kwa kile kinachoitwa amani ya dunia.

Amma kule kuwa ni kadhia ya kitambo,hakika hii ndio ilioleta kile kinachoitwa jamii ya kimataifa au muungano wa kimataifa ulimwenguni,ambayo kwa ajili yake kumepatikana kile kinachoitwa kanuni ya kimataifa.Basi kwa ajili ya kusimama Ulaya mbele ya uislamu ikapatikana jamii ya kimataifa kutoka serikali za kinasara za Ulaya.Kwa ajili ya pigo la Napolean na kuzuia kupanuka kwa Ufaransa ikapatikana kile kinachoitwa Muungano Mtukufu.Kisha katika kuzuia Ujerumani kuchukuwa mafuta ya mashariki ya kati na kiwango cha nguvu zake,kukawa na vita vya kwanza vya dunia.Kisha kwa ajili ya kupambana na Ujerumani na kuizuia kutokana na kutofata usawa wa nguvu huko Ulaya zikawafikiana serikali nne kubwa:Uingereza,Ufaransa,Marekani na mungano wa kisovieti kuitenga Ujerumani na kuizuia kurudi kuwa serikali kubwa ya pili.Kuzuia kuungana Ulaya na kuzuia kupata nguvu Ujerumani,zikawa hila za kisiasa zilizozuiya kubuniwa muungano wa Ulaya miaka kadhaa,kisha zikazuia kuungana Ujerumani makumi ya miaka.Yamepatikana matendo kutoka kwa wababe wawili kwa lengo hili kabla makubaliano na baada yake,ikawa kwa Ufaransa iko mwanzo wa mkondo katika hilo,lakini ikabadilisha baadaye,ikawa yenda mbio kutilia nguvu Ulaya kupitia Ujerumani,ikawa kwa Uingereza ina mchangio kwa hilo,hata bidii ya kuunganisha Ulaya.Zaidi ya hayo hakika kadhia ya Ulaya na yanayohusiana na hayo ni katika kadhia za kitambo.

Amma kule kuwa kadhia ndio kadhia hatari kwa kile kinachotwa amani ya ulimwengu,basi hakika hilo

hutokezea katika nyenendo na tabia za wote katika Ufaransa,Uingereza,katika nyenendo za muungano wa kisovieti na Marekani kabla kuwafikiana baina yao.Katika tabia za wababe wawili Marekani na muungano wa kisovieti baada ya kuwafikiana baina yao na pia baada ya kumalizika kipindi cha makubaliano baina yao mpaka baada ya kuporomoka kwa muungano wa kisovieti na kambi ya kimashariki ikavunja mkataba wa Warsaw.Amma Ufaransa,Uingereza na Marekani kabla kukubaliana wababe wawili walikuwa wakiwakilisha kambi ya kimagharibi.Ikawa kadhia ya Ulaya ikiwakilisha kuondoa vita vya pili vya dunia,ikawa yaonekana baina ya kambi mbili katika kutafuta hali ya baadaye ya magharibi mwa Ulaya na hali ya baadaye ya Ujerumani.Basi kambi ya magharibi ilikuwa ikiona kuunganisha ili kusimama mbele ya muungano wa kisovieti,ikawa Marekani yakusudia kwa namna haswa katika utumaji wa jeshi la kijerumani,kupata jeshi la Ujerumani lenye nguvu ili kusimama mbele ya muungano wa kisovieti na kupatikana usawa mpya baina ujerumani,Ufaransa na Uingereza.Amma muungano wa kisovieti ilikuwa ikiwakilisha kambi ya kimashariki,ikawa yaona hatari kwake kwamba yatoka kwa Ulaya na haswa Ujerumani.Kwahiyo ikawa yasimama mbele ya kuunganisha Ujerumani,mbele ya kuunganisha Ulaya,dhidi ya jeshi la Ulaya,dhidi ya kurudisha kujihami kwa Ujerumani,ikaweza kwa vita baridi,kwa matendo ya kisiasa na shughuli za kidiplomasia kufaulu.Ikakataza Ulaya makumi ya miaka kutokana na kutangulia hatua moja katika kadhia yake.

Amma baada ya wababe wawili na kwa makubaliano yaliotimu baina ya Khrushchev na Kennedy,hakika hali

imebadilika,zilipoungana rai ya Marekani na muungano wa kisovieti mbele ya kadhia ya Ujerumani,wakawafikiana katika rai moja mbele ya kadhia ya Ulaya.Limedhihi hilo mara baada ya kukutana kwao,akampa John Kennedy,raisi wa Marekani wakati huo kiwazi akisema: "Hakika uonga wa muungano wa kisovieti kutokana na kupigwa na Ulaya vita vya kijeshi kuna anayo yadhihirisha.KwakuwaUrusi imepigwa na Ulaya mara mbili katika tarekh.mara ya kwanza iliipiga Ufaransa wakati wa Napoleon na mara ya pili ikaipiga Ujerumani wakati wa Hitler.Kwahiyo ni lazima kupatikana kile kitakachodhamini kutokuweko hatari kwa muungano wa kisovietikutoka Ulaya, kama mfano kuondoa silaha za Ulaya ya kati".Tamko hili laonesha dalili ya wazi bila ya shaka kwamba rai ya muungano wa kisovieti na Marekani mbele ya kadhia ya Ulaya na kadhia ya Ujerumani kwa sura haswa imekuwa ni rai moja. Ilipomalizika makubaliano haikubadilika rai ya Marekani Ulaya katika dharura ya kudhibiti na kupiga matarajio yake yakujikomboa,kushiriki katika kuchora siasa ya kimataifa na kuizuia isirudi katika maeneo ya mamlaka yake zamani,kuondoa mamlaka yake kutoka kusini mashariki mwa Asia na maeneo ya ghuba, kunyenyekea kwake ili kubakia chini ya dhila ya Marekani katika cnini ya NATO, kusimama mbele ya jaribio la Ulaya ili kuanzisha nguvu ya kijeshi haswa kwake. Kwahiyo pindi Ulaya ilipojua kwamba mawazo ya vita baada ya mkataba yameondoka,ikataka kurudisha uzima wake na kumakinisha uchumi wake,ilianza kuwa na matarajio ya kushirikiana na wababe wawili katika kuchora siasa za kitaifa na kujenga siasa zake na Marekani juuya msingi wa ushirikiano na usawa wala sio msingi wa uraia.Kama

ilivyoanza kufanya kazi kurudi katika maeneo yake ya ukoloni ya zamani,haswa Uingereza na Ufaransa kilichofanya Marekani kuchunga shughuli za Ulaya kwa makini.Kama ilivyokuwa Marekani baadaya kuporomoka kambi ya mashariki na kuvunjika NATO,ikakimbilia kuchukuwa nafasi iliotokezea katika serikali za Ulaya Mashariki kwa kuanzisha mahusiano nao.Hilo ni kwa kukata njia ya kuungana Ulaya haswa Ujerumani ili kupanua mashariki.Pia ikawacha Marekani,ikapinga na bado yapinga,kuanzisha kikosi cha kijeshi cha Ulaya kando na NATO.Amma Urusi iliorithi muungano wa kisovieti hii haifichi uoga wake mbele ya kupanuka kwa muungano wa Ulaya Mashariki ikafanya bidii kufikia katika usalama.Lakini kwa sababu ya msimamo wa kimataifa uliotokana na kuporomoka kwa muungano wa kisovieti,kambi ya kimashariki na kuhisi kwake udhaifu mbele ya Marekani,hakuwa na budi ya kujiunga na serikali za Ulaya kwa ajili ya kujikurubisha katika faili kwa jambo la Ulaya Mashariki. Kama inavyofanya bidii kujiunga na baadhi ya serikali za Ulaya Mashariki ili iwe itaathiri katika siasa ya kilimwengu,kilichompelekea kupunguza msimamo mikali mbele ya muungano wa Ulaya na serikali zake,kinyume na hali ilivyo mara tu baada ya vita vya pili vya dunia,wakati wa kipindi cha makubaliano na mara tu baada ya haapo kidogo.

Amma Ufaransa hakika baada ya kuja de Gaulle katika utawala na mpaka alipozuru de Gaulle Marekani na kukutana na Nixon mwezi wa tatu 1969 M, ikawa Ufaransa yafanya kazi kuunganisha Ulaya na kuifanya ni nguvu ya tatu itakayosimama baina ya kambi mbili.Kwahiyo ikawa yafanya kazi kuitia nguvu Ujerumani kwa kiwango ambacho haitakuwa ni hatari

kwa Ufaransa na kuwepo muungano wa *confederal* baina ya serikali za Ulaya pamoja na dhamana ya ubwana wa Ufaransa na kufanya bidii kiasi cha Uweza wake kuitenga Uingereza kutoka Ulaya.Kwa kuitakidi kwamba siasa yake ni ya kuigiza tangu mapema mwa tarekh kuwa ni kizuizi cha njia zote za kuungana Ulaya.Lakini baada ya kujitenga de Gaulle mwaka wa 1969 M na kufa kwake baadayake kwa mwaka,alikutana na raisi wa Ufaransa Pompidou na waziri mkuu wa Uingereza mwaka wa 1971 M katika mazungumzo marefu makali alipowafiki mwishoni Pompidou uwanachama wa Uingereza.

Bado Ufaransa na Ujerumani haswa wakiendeleza siasa ya Ulaya ya nje wakishikiana,zaidi ni kwamba Ujerumani yajua upeo wa upinzani kama bguvu ya Ujerumani,basi hujaribu kushikana na Ufaransa kudhihiri kana nguvu ya mzunguko wa umoja wa Ulaya,ikitaka sana kufikia malengo yale haswa kwa hilo kama kupanua mashariki.Zikafaulu serikali mbili wakati wa vita vya Iraq mwaka wa 2003 M kwa kudhihiri na msimamo wa kipeke yake wa kupinga vita hivi, kinachoweza kumuandalia hali ili kufanya Ufaransa na Ujerumani ni kituo cha kuvutia cha siasa za nje za Ulaya za ushirika.Hazikuwa mbio za serikali mbili kwa ajili ya kuleta katiba iliowekwa mpya,muundo wa ushirika wa nguzo za kijeshi wa Ulaya kando na NATO,isipokuwa ni kwa ajili ya kuifanya Ulaya ni nguvu ya kilimwengu inayoathiri katika siasa ya kilimwengu.

Amma Uingereza,hakika iko katika kipindi cha makubalianoikawa yajaribu kuimarisha mahusiano yake na Ujerumani na kufahamu njama za Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) dhidi ya kuendelea kwa Ujerumani na dhidi ya kupata kwake nguvu.Kisha baada

ya hapo ikaamua kujiunga na soko la Ulaya la ushirika,wakati wa mkao mrefu wa pamoja baina ya Pompidou na Edward Heath mwaka wa 1971 M,hilo juu ya upinzani mkali wa kindani Uingereza.Ikajaribu Uingereza kupata nguvu na Ulaya katika kukabiliana na kabla ya kuporomoka muungano wa kisoveitina baada yake,lakini haikuwa na msimamo wa maadi wa wazimbele ya Marekani,hilo larudia dharura ya kituoni,basi Ulaya ilikuwa bado iko mwanzo wa njia ili iwe nguvu ya ulimwengu na njia yake iliozungukwa na hatari na yawezakuwa asifikie katika malengo aliokuwa akiyatumaini,haswa vile ambavyo Marekani iko macho na malengo ya Ufaransa na Ujerumani,yenda mbio daima nayo ndio yenye nguvu zaidi katika uwanja wa kimataifa,mpaka isimamishe mipango ya Ufaransa na Ujerumani na iko na uweza wa kufanya hayo kila inapopata nafasi.Siasa ya Uingereza leo imesimama juu ya kuweka mguu Ulaya na mwengine Marekani ikiotea manufaa itakapo yapata mahali popote.

Huu ndio ukweli wa watu unaotafautiana baina ya serikali za Ulaya,haswa zile kubwa kati yake,zinazo onekana kuwa ni kikwazo mbele ya kuijenga Ulaya iliounganishwa yenye nguvu inayiathiri pamoja katika siasa ya kimataifa. Kinachothibisha hayo ni kile tulichokijua wakati wa kuandaa kitabu hichi kwamba muungano wa Ulaya,iliojengwa na serikalia ishirini na tano,ukavunjika mkutano wao uliofanyika Dablin,tarehe 18/6/2004 M na hawakuwafikiana kumchaguwa kiongozi wa muungano,wakauahirisha hadi wakati uliokuja.Pamoja na hayo juu ya sababu ya watu na manufaa ya kirasilimali wanayojiunga nayo serikali za muungano,nazo ni sababu mbili ambazo ni kikwazo kwa

umoja wa Ulaya wa kihakika,isipokuwa muungano wa Ulaya umekuwa ukionesha nguvu ya kiuchumi kubwa inayoshindana na Marekani,ikawa yuro yashindana na dola katika kiwango cha ununuzi wa kimataifa.Kama ambavyo kuathiri kisiasa ni kwa kimataifa pamoja na kutafautiana maslahi na pamoja na kupenya Marekani katika serikali za muungano kwa njia ya mahusiano yake mazito na baadhi ya serikali,haswa serikali za Ulaya Mashariki zilizoungana karibuni 1/5/2004 M isipokuwa muungano umekuwa waleta dhiki yenye kwa kiwango fulani katika mipango ya kiuchumi ya Marekani.

Kwa ufupi twaweza kusema kwamba lau ungekuwa muungano wa Uingereza umeshikamana ungeweza kuvutana na Marekani kwa nguvu za kimataifa kichumi,kisiasa na kwa kiwango fulani kijeshi.Lakini ni muungano chakavu uliodhoofika sana katika nguvu zake.Hii ndio tabia ya muungano,muungano wowote,hakika hukosa nguvu zake zinazopatikana katika ule umoja.

Muungano wa Ulaya ni mbabe wa uchumi anaougopa Marekani na hufanya bidii zake zote kuipuza,kwakuwa ni mshindani wake wa kihakika katika upande wa kiuchumi.Imenukulu AFP tarehe 19/4/2003 M "Hakika Marekani yategemea kwa kiwango cha mbali uzalishaji wa umoja wa Ulaya ili kuziba upungufu wake mkubwa katika hisabu zinazopita zilizozidi dolari bilioni (500)mwaka wa 2000 M kulingana na Fred Bergsten msimamizi wa kituo cha uchumi wa kimataifa,nacho ni kituo cha masomo haswa huko Woshington".Ikatimu saini ya serikali kumi huko Athens tarehe 16/4/2003 M ya kujiunga na serikali kumi na tano zilizotangulia katika muungano wa Ulaya,baada ya takriban mwaka (mwanzo

wa mwezi wa tano 2004 M) kinachofanya Ulaya eneo kubwa la kibiashara duniani linalounganisha watu milioni 450.

Amma katika upande wa kisiasa na upande wa kijeshi,hakika muungano wa Ulaya ni dhaifu ukilinganisha na Marekani.Marekani imefaulu katika kuidhoofisha kwa sababu miongoni mwazo ni:

**A**-Kubakia katika muungano wa NATO uliokuwa ukichukuliwa kumalizika tangu kumalizika kwa kwa mkataba wa Warsaw chini ya uongozi wa muungano wa kisovieti uliovunjika.Lakini Marekani ikanusuru kuendelea kwa muungano wa NATO kwa hoja ya kuhami serikali za Ulaya kutokana na Urusi na nyenginezo ikilazimu.Kwahiyo yakabakia mamlaka ya kijeshi ya Marekani juu ya Ulaya. Akasema mkuu wa tume ya Ulaya tarehe19/4/2003 M (AFP): "Hakika muungano wa Ulaya lazima ifanye sauti yake isikike ndani ya muungano wa NATO.wakati utakapokuwa muungano uliosimama juu ya misingi miwili wa Ulaya na Marekani" akaengezea: "Hiyo itakuwa muungano wa NATO wa kihakika badala ya muungano tuliouandaa na anaouitikiya Marekani peke yake" na akasema: "Haiwezi Ulaya kusalimisha majukumukwa ya hazina na kumuachia mkoba wa amani Marekani".

**B-**Matokeo ya siasa ya Uingereza isiotaka kuyeyuka kwa muungano wa Ulayaikawa ni serikali kama Luxembourg.Kwahiyo huweka mguu wake kwa umoja wa Ulaya na mwengime Marekani,yakutane maslahi yake na maslahi ya Marekani katika nukta ya kudhoofisha muungano wa kisovieti:Uingereza ili kubakia ndio nenye nguvu Ulaya na Marekani il isishindane nayo Ulaya kama nguvu imekuwa moja.

**C-**Serikali kumi zilizotia saini tarehe 16/4/2004 Mya kujiunga na muungano wa Ulaya mwanzoni mwa mwaka wa 2004 M zaidi ni maeneo ambayo Marekani ana mamlaka nayo au kama alivyosema Prodi tarehe 19/4/2004: "baadhi ya serikali za muungano wa Ulaya mpya ziko na mahusiano ya nguvu na Marekani katika yale yanayohusiana na usalama".

**D-**Kuzidi mamlaka ya Marekani katika visima huipa mamlaka ya ziada katika serikali za muungano wa Ulaya zinazo hitaji mafuta.Pia kuzidi mamlaka ya Marekani kwa viongozi wa ulimwengu wa tatu humfanya ajipendelea katika mikataba ya kibiashara zanye faida na kunyakuwa utajiri wa ulimwengu huu, inachokataza serikali za Ulaya chumo hili.

Kwahiyo twasema kwamba hakika mizani ya nguvu za Ulaya hazikushikana na yakurubia kukosekana nguvu moja ya Ulaya,bali ni serikali zenye nguvu Ulaya zikiongozwa na Ufaransa zinazofanya kazi kupatikana muundo wa serikali nyengine za Ulaya pamoja,ili ipatikane nguvu ya Ulaya na Uingereza upande mwengine ambao haimuhusu kupatikana muundo wa Ulaya wenye nguvu,bali Uingereza ndio yenye athari kubwa.

Hivi ndivo ilivyo maingiliano ya kadhia ya Ulaya na mahusiano yake ya kitaifa yaioko baina yao au baina yake na Marekani au baina yake na kadhia moto moto nyengine,bado maingiliano haya hufanya Ulaya iliobakia iwe katika umuhimu wa kimataifa.Tafauti ya usawa uliopo,kugongana na maslahi na mahusiano huifanya kuwa ni kadhia ya hatari kwa kile kinachoitwa amani ya ulimwengu,sawa iwe ni kumakinika kwake au kutetemeka kwake.

Kwahiyo hakika kuathiri kwa kadhia ya Ulaya katika kadhia tano nyengine na maingiliano yake kati yake haiwezekani kusahaulika,juu ya hapo basi hapana budi kuangalia kadhia ya Ulaya kwa mtizamo unaowafikiana na hali ilivyo na hatari zake tangu ilipokuwa Ulaya ni serikali zinazo zozana,hadi ilipokuwa ni soko la kiuchumi la ushirika kisha kuungana kwa Ulaya kunakoleta uzito maalumu ulimwenguni na litabainika hilo kwa uwazi tutakapo eleza kadhia nyengine na mahusiano yake na Ulaya.

**2- Kadhia ya Mashariki ya Kati**

Hakika ni kadhia inayohusiana na uislamu,hatari zake kwa Magharibi,katika maene ya kimikakati na kutawala kwake mawasiliano ya Ulaya,Afrika,Asia, muundo wa kiyahudi na kuwa ni msitari wa mbele katika kutetea maslahi ya kimagharibi,ukoloni na manufaa yake ya kimada haswa mafuta.Basi kadhia yahusiana na uislamu,maeneoya kimikakati,serikali ya kiyahudi,ukoloni na mafuta.Hapana shaka kwamba kadhia iko katika upeo wa umuhimu,sio kwa wa eneo na waislamu peke yake lakini ni kwa ulimwengu mzima.

Amma uislamu ulikuwa na bado waonekana ni hatari kubwa Marekani na Magharibi.Eneo la Mashariki ya Kati huzingatiwa kuwa ni maeneo ya kutokea kikawaida ya kwa ulinganizi wa kiislamu ulimwenguni.Kwahivyo halikuwa ni jambo geni kwamba Marekani imeufanya uislamu kuwa ni adui mkubwa na wa kipeke yake baada ya juanguka ukoministi,ikawa ugaidi ndio alama yake,kuvuka mikapa kidini na siasa kali kuficha kampeni yake dhidi ya uislamu na waislamu maeneo haya nayo yafanya bidii kwa kila alichopawa katika nguvu ilikuweka mbali haraki za kiislamu za kisiasa na

utawala,hiyo ni katika mbinu za kutishia, kushika,kuadhibu na kuzidhibiti kile kinachofanya serikaliza vibaraka zinazomfuata katika maeneo yao.Ametangaza Bush vita vipya vya kimsalaba dhidi ya waislamu kwa sura ya wazi,akasema John Ashcroft waziri wa uadilifu wa Marekani: "Wazi hakika ugaidi wawezekana katika uislamu kwa dhati yake,sio tu peke yake baadhi ya wanaojiunga nao",na akasema kwamba Allah ahimiza ugaidi katika Quran kwa kiasi za wakati wake.

Amma maeneo muhimu ya Mashariki ya kati na kutawala kwake mawasiliano, umuhimu wake huja katika eneo la makutano ya mabara ya zamani matau:Afrika, Ulaya na Asia na kutawala kwake katika mapito membamba, Basphorous,Adan, Hormoz,Swez Canal,bahari Nyeupe ya kati,bahari Nyeusi,bahari Nyekundu, Ghuba na kuongezea na kuwa ni makutano ya njia za mali ghafi na bidhaa baina ya mabara matau.Umekuwa umuhimu wake kimikakati huleta hali ngumu baina ya kambi mbili Magharibi na Usovieti kabla ya makubaliano.Hiyo ni kwamba Mashariki ya Kati ni kama ukanda wa Magharibi katika maeneo ya kambi iliopigwa dhidi muungano wa kisovieti iliotangulia,ikawa ukanda huu ni msitari wa utetezi wa mwanzo wa Magharibi katika kuilekea muungano wa kisovieti kutoka Mashariki ya Kati na Afrika.Kwahiyo zikabuniwa Mashariki ya kati kambi za kijeshi,zikiwemo kambi za kinuklia,yakapika majaribio kadha kuunganisha serikali zake na mikataba ya kijeshi na vikabuniwa viwanja vya ndege vingi na njia pana zinazoitwa *autostrada,*zikawa na umuhimu wa kimikakati.Amma baada ya makubaliano ya wababe wawili mwaka wa 1961 M,haukuchukulia umuhimu huu

wa kijeshi.Kwahiyo ikapuza jambo la mkataba wa kijeshi,zikaondolewa kambi za kinuklia wakawa wababe wawili ni nyayo katika kuondowa kambi za Uingereza, zikafaulu katika kuondoa kambi ya Adan,Libya,Seuz Mashariki wakafanya bidii kuondoa kambi zake Cyprus.Kwahiyo haikuchukuliwa kuwa Mashariki ya kati ina umuhimu kimikakati wakati huo.Isipokuwa baada ya kumalizika vita baridi na kuondoka muungano wa kisovieti,ukarudi umuhimu wa Mashariki ya Kati wa kimikakati,haswa kulingana na Marekani mbele ya Urusi na Ulaya.Kwahiyo ikarudia Marekani katika kuwepo na kambi za kijeshi Ghuba,ikanyakuwa Afghanistani na Iraq,ikatangaza Pakistani na Kuwait baada ya Bahrain kama mshirika wa kimikakati.

Kisha ikamchukulia kuwa ni mwenye kuchelewesha msitari wa mbele katika kutetea usalama wa umoja wa mataifa na kuandalia mradi aliouita “Mradi wa Mashariki ya kati mkubwa” kisha akaubadilisha hadi “Mradi wa Mashariki ya Kati na Afrika Kazkazini”.Ikamtanguliza katika mkutano wa serikali nane zenye uwezo mkubwa wa kiviwanda uliofanyika mwezi wa sita 2004 M katika maeneo ya  Sea Island.

Juu ya yote haya twaweza kusema maeneo muhimu ya Mashariki ya Kati yalioenea kutoka magharibi mwa bahari ya Atlantic Magharibi hadi Iran na Iraq mashariki mwa Ghuba,kutoka kazkazini mwa Uturuki hadi jangwa kubwa la Afrika Kusini yaani yajumuisha serikali za kiarabu jumla kuongezeka na Uturuki na Iran,haya ni maeneo muhimu yaliofanywa ni kibla cha wakoloni na panapokusudiwa na wenye tama,kwa ule umuhimu mkubwa katika usafiri na mawasiliano,si katika kipindi

hichi peke yake,lakini tangu vita vya kimsalaba mpaka leo hii.
Amma kulingana na muundo wa kiyahudi uliopandwa Paletina,ikawa ni kituo cka swala la Mashariki ya Kati kilichokuwa ni sababu ya kukosekana utulivu,si kwa Mashariki ya Kati peke yake,bali ulimwengu mzima.Hilo ni kwa kutambua wamagharibi wenyewe waliokiri kwamba 90% katika matatizo ya ulimwengu wa kiislamu yasiyomlaza mmagharibi,hakika yarudia tatizo la kuwepo serikali ya kiyahudi Palestina yaani kati kati ya ulimwengu wa kiislamu.
Amma umuhimu wake kikoloni,hakika hili ndilo lilioisababishia balaa, ikaiondowa na sifa yake kuwa nia serikali kubwa na nguvu ya kilimwengu ikaibadilisha kuwa koloni ya kimagharibi linalo zozana serikali za kimagharibi ukoloni na kueneza nguvu zao.Basi mafuta yaliyopo humo yanayozidi nusu ya mafuta ya ulimwengu na mali ghafi iliopo humo Jordan,Iraq,suria,Uturuki,Iran na nyenginezo huleta utajiri mkubwa ulioko sawa na mara kumi utajiri wa Ulaya kuchanganya na wa Marekani.Kwahiyo serikali zashindania kuikoloni na zavutana kwa ajili yake.Mpaka vita vya Marekani ni kwa kuidhibiti ni mfano ulioko wazi.
Basi kuchanganyika misingi hii mitatu katika kadhia moja nayo ni:Uislamu,petrol,maeneo muhimi kimikakati na (Israeli),ni mdhamini wa kubadilisha kadhia hii kuwa kadhia hatarina inayo tatiza sana kwa kiwango ambacho imekuwa ni katikati ya fundo na tatizo la matatizo,nalo ni fundo zaidi ya kufunguliwa na serikali kubwa na kuliko wanavyo lifahamu.Kwahivyo basin i kadhia sugu iliozidi ugumu,isioyoweza nguvu kubwa kutatuwa,nayo

haitotatuka isipokuwa itakaposimama serikali ya kiislamu (khilafa).
Mashariki yakati ilikuwa chini ya utawala na mamlaka ya uislamu na serikali ya kiislamu hadi katikati ya karni ya kumi na nane.Tangu kongamano la Berlin yaani tangu mwishoni mwa karni ya kumi na nane,zilianza serikali kuu za Ulaya zikaanza kuipiga vita,zikaipiga vita zote Ufaransa,Uingereza na Utaliano. Vikaendelea vita hadi walipoiangusha serikali ya kiislamu kwa kuiangusha serikali ya kiothumani kwa kuindosha khilafa,ikaingia Mashariki ya Kati chini ya ukoloni Uingereza,chini ya udhibiti wake na mamlaka yake ikaenea mamlaka yake katika serikali jumla zake mpaka serikali zisizokuwa za kikoloni kama Uturuki na Afghanistan.Haikuwa Ufaransa isipokuwa sehemu ndogo iliofungika katika sehemu ya kazkazini mwa biladi za Shamu zinazoitwa Suria na mwambao wake ulioko kusini magharibi unaoitwa Lebanon.Ikabakia hali hivyo hivyo mpaka mwisho wa vita vya pili vya dunia,wakamfukuza mfaransa nan a kubadilika ukoloni wa Uingereza kwa mbinu nyengine mpya,kwa kumakinisha kugawanya kwake na kuipa jina la serikali kila sehemu.Kwahiyo vikamalizika vita vya pili vya dunia na ikawa Mashariki ya Kati yote yachukuliwa ni koloni ya Magharibi au sahihi zaidi ni koloni ya Uingereza.Kwahiyo ikawa yachukuliwa kuwa ni ulimwengu ulioko huru na sehemu katika kambi ya kimagharibi na hapakuwepo na kambi ya kimashariki.Zimemsaidia Uingereza sababu mbili kujipwekesha na ukoloni wa Mashariki ya Kati sababu mbili:

**Kwanza:**Kudhoofika Ufaransa kisiasa,kiuchumi na kimataifa,haikuweza kufatana na Uingereza na kuzozana nayo katika kukoloni Mashariki ya Kati.
**Pili:**Ni kuendelea Marekani baada ya vita vya kwanza vya dunia na siasa ya kujitenga.Kwahiyo akawa peke yake Uingereza katika kukoloni Mashari ya Kati tangu karni ya kumi na tisa hadi mwisho wa karni ya ishirini.Lakini baada ya mwaka wa 1950 M hali ikatafautiana na kubadilika kimsingi,ikadhihirika mivutano ya kikoloni baina ya Uingereza na Marekani,kukatokezea kilichoshuhudiwa katika vita na mapinduzi,ujanja na njama,ukaendelea mvutano kuzidi kwa kipindi fulani na kupunguwa katika chengine mpaka iliweza Marekani kuchukuwa uongozi Mashariki ya kati.Ikafikia Uingereza katika udhaifu hadi ikawa haiwezi kupambana na Marekani kiwazi,lakini ikabakia na mshikamano wake kiasi cha uweza wake kuhifadhi koloni zake,akafanya hima ya kuwepo katika maeneo hata kama ni sehemu na hilo ni kwa kushiriki na Marekani katika miradi yake kama ilivyofanyika katika kuinyakuwa Iraq.
Juu ya hayo twaweza kusema kwamba hakika mvutano wa Mashariki ya Kati baada ya vita vya pili vya dunia ulikuwa umemakinika kiathari baina ya Marekani na Uingereza kama ifuatavyo:
Iliendelea siasa ya Marekani na Uingereza katika kadhia ya mashariki ya Kati baada ya vita vya pili vya dunia wakifuata njia ya kushirikiana,zikawa serikali mbili zachanganyika na kukumbushana katika siasa yao,kuunganisha mipango na mbinu baina yao,ikaendelea Uingereza kuruhusu Marekani kuwania baadhi ya manufaa haswa mafuta ya Bara Arabu,ikaendelea kushikana naye mara nyengine lakini lakini ikawa

husimama mbele yake mara nyengine katika yale aliyokuwa akiyaona yana madhara kwa maslahi yake.

Ilipokuja kadhia ya Mayahudi Palestina,ikawa rai ya Marekani mbele ya serikali ya kiyahudi Palestina,hiyo ni kwa ajili ya kuifanya sababu ya kukoloni maeneo hayo na haikuwa uingereza imekata jambo lake katika kubuni serikali ya kiyahudi,ikawa ina shaka baina ya kuwa Palestina ni nchi inayo tawaliwa na Mayahudi au ni serikali ya kiyahudi.Ikawa yataka kuiunganisha na koloni zake nyengine za biladi za kiarabu.Kwahiyo haikukata jambo,ikarudisha kadhia kwa baraza Umoja wa Mataifa,ilipopitisha baraza la Umoja wa Mataifa kwa shindikizo la Marekani kuanzisha serikali ya kiyahudi,ikanyamaza Uingereza na kuwacha zama zikipitisha:Je,laweza eneo kuwacha serikali ya kiyahudi baina ya waislamu,amma mwili huu wa waislamu utaitema?.Ikawa siasa yake mbele ya serikali ya kiyahudi ni kungojea yatakavyo amua masiku?.

Amma Marekani hakika alianza kuhimiza mipango ya kumakinisha Israel na kumaliza kinachozuia kuimakinisha.ikawa Uingereza iko kinyume kwa hilo lakini kwa njia ya kisiri,kukapatikana mvutano mkali baina ya Uingereza na Marekani kuhusu kuwepo kwa serikali ya kiyahudi.

Kwa upande huo ikajaribu Marekani kunyosha bomba la petrol kupitia Jordan,Syria na Lebanon katika bahari Nyekundu ya kati,ikasimama Uingereza njiani kwake,ikawa nayo ikiwa ya kale katika eneo,inayoweza kuathiri viongozi jumla wa eneo.Kwa kuwa ni wawakilishi wake.Ikaona Marekani kuwa njia moja ya mageuzi ya hali ya eneo ni kutekeleza siasa alioitekeleza Marekani Kusini nayo ni kupata viongozi wa wana jeshi

na kuleta mapenduzi,yakatekelezwa mapinduzi ya kwanza ya kijeshi alioyatekaleza Husni al-Za'im wa Syria.Akampa Marekani fadhila kwa kurefusha bomba la petrol,akarefusha bomba na kumaliza tatizo hili.Lakini Uingereza ikahisi kwamba Marekani yataka kukoloni eneo lile na kulichukuwa kutoka kwake,ikaanza kupambana na Marekani vikali,lakini kwa mbinu za kisiasa,hila na kwa njia ya wenyeji.

Baada ya mapenduzi ya Husni al-Za'im na baada ya kuzidi mpambano wa Uingereza kwa miradi yote ya Marekani,ulibadilika mvutano wa kisiri uliokuwepo baina ya serikali mbili hadi kuwa mvutano unaokaribia kwa wazi,wakaona wawakilishi wa Marekani wa kidiplomasia huko Mashariki ya Kati ikitishia maslahi ya Marekani kijeshi na kiuchumi eneo lile,wakaona kubakia siasa ya Marekani upande hadi upande pamoja na Uingereza maana yake ni kubakia Marekana,kama ilivyokuwa kabla ya vita vya pili vya dunia,kuwa ni chombo kinachotumiwa na Uingereza,anayetosheka kwa kumpa chakula kidogo ili kumtuliza katika eneo,kumtetea na kumkataza heri zote za eneo na kubakia eneo lote kuwa chini ya mamlaka ya Uingereza peke yake.Wakaona hayo wana deplomasia wa kimarekani wanaotegemewa mbele ya mkusanyiko wa waarabu, akahakikisha kuwa ni lazima kufanya baadhi ya mabadiliko ya kimsingi katika kuielekea siasa ya Washington na kuirekebisha marekekbisho mapya,kwa namna ambayo atafanya kusaidiana baina wa wakaazi wa biladi ndio msingi wa maendeleo siasa hii na kuikamilisha,lakini waliona wenyewe wakati ule kwamaba kundi kubwa wako mashakani kuengezea na kusimama na wakati wanapomfichia wailamu katika chuki na karaha.Kwahiyo

wakaona kwamba ni lazima kutatuwa matatizo haya kabla ya kufikiria kisawa sawa na kabla kuanza kubadilisha eneo badala ya kuwa ni kambi ya Uingereza hadi kuwa ni kambi ya Marekani,kwahiyo wakaitisha kongamano miongoni mwao kutafuta maudhui hii.Mwezi wa kumi na moja 1950 M wakaweka kongamano la kwanza Istanbul na kusimamia kongamano bwana George Maggie muwakilishi katika wizara ya nje ya Marekani katika mambo ya Masharika na Kati na Afrika Kazkazini,likaendelea kongamano hili kwa muda wa siku tano mfululizo wakafatilia kongamano hili la kisiri watu wanachama wakubwa wa kisiasa,kimikakati na kiuchumi wa eneo hili,ikamakinika rai yao kwamba hakuna njia ya kubakia siasa ya Marekani kufungamana na siasa ya Uingereza,wakitaka kihakika kubadilisha Mashariki ya Kati kuwa ni kambi ya Marekani na kufanya kusaidiana na watu wa biladi kuwa ni mbinu katika mbinu za kubadilisha eneo hilina kufanya yale yaliofika Syria katika kukataa Shukri al-Quwatli raisi wa jamhuri kuyapa ubora mabomba ya petrol akaanza hilo kupitia njia ya mapenduzi alioyatekeleza Husni al-Za'im,walioifanya hiyo kuwa ni dalili ya kushikika ya kusihi rai yao,hasa kuwa Uingereza ilirudi mwaka uleule wa 1949 M,wakatekeleza mapenduzi aliyoyafanya El Hannawy na kumuondoa Husni al-Za'im ikarudi Syria kwa Uingereza.Ikawa hii pia yawasaidia katika rai yao,kwamba ni lazima kutenganisha siasa ya Marekani na siasa ya Uingereza itakapotaka kufanya kazi katika eneo.Hizingatiwa kongamano hili kuwa ni chombo muhimu cha kulekeza diplomasia ya Marekani katika ardhi ya waarabu, yakawekwa mapendekezo kw azote nyuba nyekundu,wizara ya nje,wizara ya ulinzi na jeshi la

wanamaji na kuingia katika mapendekezo haya mkutasari muhimu unaofupishwa kama ifuatavyo:
Yamethibitisha majaribio ya vita vya pili vya mwisho kwamba eneo la Mashariki ya Kati kuwa ni kambi ya kimsingi inayokusanya jumla ya vipengee muhimu vya kuingia kwenye vita dhidi ya muungano wa kisovieti na kwamba kufikiria kuvamia visima vya mafuta vya Urusi huko Caucasus na kuzuia chombo cha kupiga vita vya kisovieti katika mapato yake ya juu ya mafuta,sio katika mipango mikubwa ya kufaulu kwake kupitia njia ya kusaidiana kijeshi na Uturuki peke yake,bali hakika hayo yalazimu kupatikana kambi za anga zilizopangana Syria, Lebanon na Palestina ili ibadilike Iraq na Misri kuwa ni hazina kubwa iliosalimika kutuma watu,silaha nan a garama katika mradi wowote wa uvamizi unaolenga kuzingira na kuzuiya visima vya mafuma vya mafuta vya Soviet,Baku Caucasus na kiujumla.
Kama zilivyo kampeni za kijeshi juu ya Ugiriki,Sicily na Utaliano kwa muda wa kipindi kirefu kutoka mwaka wa 1941 M hadi mwaka wa 1944 M ikawa wazi kwa namna isioyo hitaji mjadala wala utafiti,umuhimu wa Mashariki ya Kati katika utowaji na usambazaji wa mfano wa sampuli ya vitendo vya kivita vikali,vilivyo dhamini ushindi wa vita vya vikosi vilivyounguna na kuzingira majeshi ya maadui ngome ya Ulaya.
Kisha ikamalizika kwaujumla na maoni yalioyeyushwa na makubaliano wa waliokuwa katika kongamano wote kwa sura ya mapendekezo yafuatayo:
**Kwanza:**Kujitenga na siasa za Uingereza katika jumla ya yanayokusanya kadhia zinazohusiana baina yake na baina ya ulimwengu wa kiarabu.

**Pili:**Kufanya uungaji wa mapendekezo ya waarabu ya kikaumiyya ndio msingi wa Marekani wa siasa Mashariki ya Kati.

**Tatu:**Kusaidia Misri matakwa yaokutoka kwa Uingereza na kuhimiza kukuwa kwa mfano wa harakati hizi Iraq.

**Nne:**Kuzuia kuendelea kwa ushindi wa kidiplomasia na uchumi wa Israel na kuhimiza shirika la Umoja wa Mataifa kutekeleza mradi wa kugawanywa Palestina serikali mbili ya kiarabu na kiyahudi na kutekeleza maamuzu ya baraza la usalama la kimataifa katika yanayohusiana na kusawazisha swala wakimbizi wa kiarabu, kwa msingi wa kuwarudisha katika miji yao na kubadilishana na wale wasio kuwa na haja ya kurudi.

Husemwa kwamba waliwapa Misri mapendekezo haswa,kwakuwa walihusia dharura ya Marekani kuchukuwa Misri kutoka kwa Uingereza na kuitoa Uingereza humo na kusimamisha serikali yenye nguvu itakayo itakayosimamia uongozi wa eneo lote,kwa yaliothubutu katika tarekh kwamba Misri ndio mlango wa eneo la Mashariki ya Kati.

Yamepelekwa maoni haya katika kitengo cha kiongozi cha Umoja wa Mataifa,kikawa chama cha demokrasia ndicho kinacho simamia utawala Marekani na chama cha demokrasia kinachopendelea kawaida kuipaka mafuta Uingereza.Ikawa Truman ndie raisi wa Marekani na Truman alieingia kwenye utawala kwa kuhimizwa na sababu mbili:Kwanza mamlaka ya kiyahudi pili mamlaka ya Uingereza katika baadhi ya waadilifu wa Marekani,akajifunga Truman na majukumu kadhaa mbele ya Uingereza pia mbele ya Mayahudi. Kwahiyo hayakuchukuliwa maamuzi haya umuhimu uliokuwa

wana diplomasia wanatarajia,hata kama walifikia umuhimu wake katika zama za Eisenhower.
Namna mambo yatakavyokuwa,hakika siasa ya Marekani imechangamka Mashariki ya Kati baada ya kongamano la wana diplomasia waliotajwa,ikasimama Marekani kujaribu vikali kupatikana suluhu baina ya serikali za kiarabu na Israeli na kuitowa Uingereza kutoka Jordan na Iraq,kwakuwa imetengana diplomasia ya Marekani na mfalme Abdulaziz akamuachia katika kufunga ahadi naye ufupisho wake ni kwamba awache mfalme Abdulaziz Uingereza na awe na Marekani na kwamba Marekani amuwache ajuinge na Iraq na Hijaz,aanzishe serikalikutoka Jordan,Iraq,Hijaz aiunganishe na Syria na Lebanon kinyume na kufanya sulhu na Israeli.Hakika Marekani itawapa mikopo na misaada ya lazima ili kukuza serikali hii mpya kiuchumi,akakubali mfalme Abdallah hayo,kisha akaanza kazi kufikia mradi huu.Akenda Iraq,huko akakutana na Abdalla na Nuri al-Said na kuanza maudhui,akawataka wende pamoja,haikuwa kwao ila kushikana na balozi wa Uingereza huko Baghdad na kumuonyesha miradi ya mfalme Abdallah, akamkataza muingereza kwenda nao.Kwahiyo hawakukubali alioyasema wala kuyakataa wakawacha mambo yakipita,akarudi Jordan akatumtumia Riadh Al Sulh waende pamoja ili amsaidie mradi ule,akakubali Riadh Al Sulh hilo na wazi ni kwamba alikuwa amegeuka na wamerekani,akakimbilia muingereza kumuuwa Riadh Al Sulh huko Amman,akiwa njiani kuelekea uwanja wandege akirudi Beirut,kisha baada ya wiki moja akauwawa mfalme Abdallah al Qudsi msikiti wa al Aqswa,matokeo ya njama iliyogunduliwa alioipanaga Cloob kumuuwa, akamtahadharisha balozi

wa Marekani kiwazi zile njama na safari kabla ya siku moja kabla ya kuuwawa kwake kwahiyo ukafa mradi huu.Mwaka ule ule wa 1952 M ukatokea uchaguzi wa uraisi Marekani,kikatokea chama cha jumhuri na uraisi wa Eisenhower,akashika uongozi mwanzo wa mwaka wa 1953 M,kwa kushika utawala ukazidi utawala baina ya Uingereza na Marekani.Kwakuwa Eienhower ajulikana kwa kutanguliza maslahi ya Marekani ya juu katika pande zake mbili kijeshi na kimataifa kuliko ugandamizaji wa kiyahudi na Uingereza. Kwahiyo ikawa mvutano baina ya serikali mbili Marekani na Uingereza una sura kali,ikawa katika alama zake muhimu ni Marekani kuchukuwa Misri kutoka kwa Uingereza, kisha mwisho kutolewa kutoka homu.Ikawa Marekani kabla ya hayo imeteleza mapinduzi Syria akaja na kibaraka wake Adib Shishaklykatika utawala. Kwahiyo ikawa Misri na Syria ziko na Marekani.Tangu zama hizo biladi za kiarabu zote zimekuwa ni uwanja mpana wa mvutano wa Uingereza,akatekeleza matendo kadhaa yanayomfanya kama mpira unaotoka katika mkono wa Marekani hadi mkono wa Uingereza na kutoka mkono wa Uingereza hadi mkono wa Marekani, hivi ndivyo ilivyo.Yakadhihika haya katika matendo kadhaa yaliojumlisha Misri, Syria,Jordan,Iraq,Saudia na Yemen,ikwa zaidi ni Syria kwa sifa yakuwa ni mtu wa kati wa mkataba,yaathiri bildi zote za kiarabu kwa sura jumla.Kwahiyo yakatokea Syria matendo kadhaa ya kisiasa,ikawa ya muhimu ni kuzidi mapinduzi,basi ikawa kwa kuuwawa Husni al-Za'im ikadhihirika chuki ya Uingereza kwake na kumalizika utawala wake.Mpaka ikawa Uinereza yafanya kazi kuimakinisha utawala Syria kwa msingi wa demokrasia,kufanya kazi ili kuiunganisha na Iraq kama

hatuwa ya kupatikana hilaliya rutuba.Kihakika yakatokea mapenduzi Syria, ikawekwa katiba ya biladi,ikadhibiti chama cha raia na chama cha kizalendo katika utawala na kutangaza katika mpangilio wao kuungana na Iraq.Imejaribu Marekani kuzuia juhudi za Uingereza,lakini hakuweza kupata fursa hadi alipokuja Adib Shishakly katika utawalaakamdhibiti kwanza nyuma ya pazia,kisha akamdhibiti kiwazi,akajiweka mwenyewe kuwa raisi wa jamhuri,ikaingia Syria katika mkono wa Marekani ikaendelea kuwa katika mkono wake hadi Mei 1954 M,waliposimama vibaraka wa Uingereza kwa usaidizi wa Iraq kumpenduwa Shishakly ikarudi Syria katika mkono wa Uingereza na kurudi utawala wa bunge. Wakati huu ikaanza Uingereza kudhihirisha muungano wa Baghdad kuwa wazi. Hadi ilipokuja mwaka wa 1955 M lilpoingia eneo hatuwa kali katika mvutano wa Uingereza na Marekani kwa sura kali.Basi ikaanza Marekani kupitia njia ya Misri akachangia mchangio wa kujikomboa,umoja,ujamaa na akaanza Abdinasir kuingilia Marekani kimvutano mkali na Uingereza.Akatekeleza amri ya Marekani kwa kununua bishara ya silaha kubwa kutoka kambi ya kikoministi,akawafunulia wananchi kwamba amekuja kuipiga Israeli na kuivunja.Yakawa hayo ni madai makubwa kwa raia wa kiarabu wote,akatabani uzalendo wa kiarabu,akatangaza kwamba Misri ni ya kiarabu,akalisajili hilo katika katiba ya katiba ya serikali ya Misri,akawa ananadi uadilifu wa kijamii na umoja.Yakapelekea matendo yake hayo kukusanya raia wa kiarabu na akawa ni bwana katika mabwana wa biladi za kiarabu.Ikasaidia katika hilo mbinu walioifata Marekani katika kuipiga Uingereza, kuleta mkanganyiko

baina ya watu wa biladi,hakika juu ya uadui uliomakinika wakati baina ya Marekani na Urusi (muungano wa kisovieti) imefafanya mbinu za kuvutia Urusi (muungano wa kisovieti) katika maeneo,kuifanya ni sababu ya kimataifa dhidi ya Uingereza.Pamoja na Marekani kupiga ukoministi ilmkinaisha Jamal Abdinasir kiongozi wa Misri na ukoministi na kumlingania,basi ikawa Misri kununua silaha kutoka kambi ya kikoministi ni sababu ilioingiza Urusi (muungano wa kisovieti) katika eneo,ikawa ulinganizi wa Abdinasir wa uzalendo ni sababu ya kisiasa katika kuhuisha uzalendo wa kiarabu baada ya kuwa umekufa au kukurubia kufa.Ikawa tabani ya kikominsti ilioendelea kutokana na uadilfu wa kijamii ndio sababu inayoathiri katika kuenea kwa mrengo wa kushoto ikaifanya jeuri katika rai jumla katika eneo.Kisha ikawa tabani ya Misri ikivamia muungano wa kigeni haswa muungano wa Baghdad ina athari kubwa katika kuondo shaka ujira wa Abdinasir kwa Marekani,haswa alivyokuwa akihujumu ukoloni wa Marekani.Kwahiyo haikubakia shaka hata kidogo kwa raia wa kiarabu wote kwamba Jama Abdinasir kuwa ndiye mkombozi mkubwa aliemtuma Allah kwa umma hii kuikomboa kutokana na ukoloni.Kwahiyo wakajifunga watu wote naye isipokuwa kundi moja lililokuwa likijaribu kumfichuwa na kumhujumu,lakini hilo halikuathiri kidogo wala sana akaendelea kudhibiti kikamilifu.Kihakika kudhibiti huku ndivyo walivyokuwa vibaraka wa Uingereza huko Jordan na Iraq kwa sifa yakuwa ni viongozi,katika kituo kinachotetemesha,wakawa vibaraka wa Uingereza huko Syria na Lebanon katika hali mbaya kiraia.Kwahiyo yakapatikana makazi mazuri kwa Marekani kwakuwa yafanya kazi kuiondoa Uingereza bila kuzinduka eneo

kwamba kinatimu katika matendo ni kuingiza mamlaka ya Marekani katika eneo lamahali pa Uingereza.Ikawa ni juu yake kudiriki kwamba ni wajibu kufanya kazi kusafisha ukoloni wa serikali mbili:Marekani na Uingereza siokubadilisha moja kwa nyengine.

Wakati huu yakatokea Syria maendeleo ya kindani,aliokuwa ameyapata Abdinasir kutoka kwa jumla ya raia juu yake katika kutetea maendeleo haya,basi hakika chama cha ba'thi kiliungana na chama cha waarabu cha kikomisti, ukapatikana muungano huu wa chama na ba'ath kuwepo katika jeshi. Kisha hakika vyama viwilivikaenua alama ya(umoja,uhuru na ukoministi),vikawa vina athari serikalini,vikashirikiana kihakika,vikapata kutoka kwa Abdinasir na anacho kinacholingania kuwa nifursa kwao ya kuwafanya raia wawaangalia,wende na umoja ,na ukoministi wanaotaka kufata kiwazi.Kwahiyo imekuwa Syria ikitawaliwa na tawala zilizodhibitiwa na chama cha ba'ath ili kuepukana na shari yake,kuogopea yaliyokuwa wakidhania ya kupatikana uraia baina ya watu. Kwahiyo ikawa Syria na Uingereza kihakika,lakini ikidhibiwa na fikra mbili ya umoja na ukoministi nay ale walioko nayo katika kuathira rai jumla.Kisha akasimama Abdinasir kutaifisha Suez Canal,ikatokea uadui wa tatu kwa Misri, akafikia Abdinasir katika uraia wake upande wa mbinguni.Kwahiyo hawakuwa wajasiri vibaraka wa Uingereza kudhihirisha ukumbini,wakatulia mpaka hawakukurubia kuhisiwa na yoyote.

Katika mwezi wa nane 1957 M wakakusanyika idadi ya maofisaa na kutajiana yanayohusiana na utawala huko Syria mwendo wao na Magharibi,katika kuchumka mamlaka ya kimagharibi humo,basi wakaamua

kunyakuwa mamlaka ili iendele utawala,yaani raisi jamhuri na mawaziri katika vituo vyao,wakapambana nao,yaani maofisaa kwa kusimamia mambo na kusimamia mambo ya utawala. Wakatekeleza kitendo cha kutenganisha Syria na ukoloni wa Magharibi,ikawa Syria kabla ya kutenganishwa kwake na ukoloni huu wa Magharibi na Uingereza kihakika,lakini kilicho wazikwake ni kuwa yachukuliwa kuwa imefungwa na Marekani.Kwakuwa fikra zilizo tawala ni fikra anazolingania Abdinasir:uhuru, ukoministi na umoja na chamacha ba'ath chenye neno la kwanza katika rai jumla chadhihirisha kama kwamba ni rafiki wa Abdinasir au mshirika wake.Kwahiyo ikachukuliwa kuitenganisha kwake na Maharibi kwaelekezewa Marekani,hata kama kihakika kwaelekezewa Uingereza zaidi kuliko wamarekani.Juu ya haya hakika Uingereza walikubali kutenganishwa huku kwa kunyamaza wala kutikisika. Amma Marekani walishikwa na wazimu,ikaanza kutumia ubaguzi wazikwa kupiga maofisaa na kurudisha katika uhatari wa Magharibi.Kukapita majaribio kadha kwa ajili ya hilo,yote akawa ni yenye kushindwa.Baadaya kushindwa Marekani kutatuwa matatizo,akatangulia Abdinasir kutatuwa, akamtuma Mahmud Riadh, akawa huyu afanya kazi kupatikana muungano baina ya Misri na Syria ikachuwa hapo misri utawala huko Syria,kwahiyo ikachuwa Marekani uongozi,ikawa yafanya kazi kuifukuza Uingereza kutoka Iraq na Lebanon,ilipokuja mwaka wa 958 M,ikaja mapenduzi ya Lebanon kisha mapenduzi ya Iraq,ikawa Syria,Iraq, Lebanon na Misri iko mkononi mwa Marekani,wala haikubakia kwa UIngereza isipokuwa Jordan.Akawa Abdinasir hukutana naye Jordan,ikawa iko karibi kujisafisha kutoka eneo

lote,isipokuwa Uingereza haikuvunjika moyo,ikawa yaanza kufanya kazi katika kambi yake Jordan.Ilipokuja mwaka wa 1961 M ikawa ina nguvu ikafanya kazi Syria,zikakusanyika nguvu jumla za kisiasa,chama cha wananchi,chama cha kizalendo na chama cha Ba'ath au (chama cha ba'ath na uarabu wa kikoministi)vikakusanyika vyote dhidi ya Abdinasir na dhidi ya umoja, ukatokea mgawanyiko wa Syria na Misri,wakarudi vibaraka wa Uingereza kudhibiti utawala.Isipokuwa Marekani ilimkubali Abdulkarim Qasim katika utawala Iraq baada ya kuwacha koloni yake na kuwa na wakoministi,ikapatikana Iraq serikali ya kimarekani anayoitawala chama cha ba'ath,ikawa yafanya kazi kubadilisha wanachama Syria na Jordan kwa kuziunganisha na Iraq.Ikaogopa Uingereza hilo,wakasimama vibaraka wake Damaskas kupendua kimakusudi, wakafanya chama cha ba'ath ni pazia ya utawala.Isipokuwa mwaka wa 1971 M baada ya kwenda Hafidh Asad Misri na kuingia katika umoja wa wanne akarudi kutoka Misri hadi Syria kwa uso ambao hakwenda nao,ilikinaishwa huko kwa aweza kuwa raisi wa jamhuri ya kiarabu ya Syria juu yakuwa ni Alawiyya Nasiriyya.Ikaonekana wazi wakati huo kwamba Marekani ilikuwa nyuma ya hilo,kwamba itamtegemeza madamu yuko pamoja naye.kama ilivyo Misri itafanya kundi lake huko kumuunga mkono na kwamba Misri na alioko nyuma yake Marekani,watafanya kazi kuondowa kizuizi cha kumnasibisha kuwa raisi wa jumhurikwakuwa na Alawiyyu na watu Syria hawakubali kutawalwa na Alawiyya bali muislamu.Hivi ndivyo alivyo muandalia Marekani mambo,kumrahisishia mazito baada ya kukubali kwenda pamoja.Ukaanza mwendo wa

kutekeleza hayo. Basi akaanza taratibu ili awe raisi wa jamhuri,akaanza kuzuru kazkazinikisha akatekeleza mawasiliano ya wananchi.Alipoona kwa wananchi wanakwenda na kiongozi na kwamba hakuna upinzani wa wazi kwake,akakimbilia kutekeleza hilo kivitendo,ukatimu uchaguzi wa Hafidh Asad wa uraisi wa jamhuri ya kiarabu ya Syria na kutawalishwa siku ya 12/3/1971 M siku ya uamuzi,kisha akawa Hafidh Asad raisi wa jamhuri ya Syria,ikaingia Syria katika makucha ya Marekani upya,nayo bado mpaka leo.

Huu ni mfanokutoka mvutano wa Uingereza na Marekani huko Syria nalo ni dhihirisho wa wazi la mvutano.Amma serikali zilizobakia za kiarabu,hakika Jordan ni kivuli chini ya udhibiti wa Uingereza.Kwakuwa wananchi thuluthi mbili za wapalestina wengi wao wanaishi kwa kitambulisho chaUmoja wa Mataifa,maisha ya watu wake wanaofanya kazi nje ya Jordan,thuluthi yake ni mabeduiwa mashariki mwa Jordan wengi wakiishi miongoni mwao katika maisha ya watu wao katika jeshi.Kwahiyo haikupata Marekani katika wananchi wa Jordan hali nzuri alivyoipata Syria,haikutokea Jordan kitendo chochote cha kisiasa kinacho dhihirisha mvutano wa kimataifa,isipokuwa maandamano yaliotokea dhidi ya mkataba wa Baghdad,jaribio la mapenduzi yaliotetwa na mfalme Hussein mwaka wa 1957 M,alioleta kuwafukuza baadhi ya vibaraka wa Abdinasir kutoka biladi. Kufikia hapa haichukuliwi Jordan kwamaba kwamaba imetokea matendo ya kisiasa makali yanayohusiana na mvutano,hata kama katika sehemu kubwa zinazo pita mivutano baina ya Marekani na Uingereza kwa yale aliopo katika utajiri unaobabaisha chini ya ardhina juu ya maji.

Amma Iraq,hakika juu yakuwa Abdul Salam Arif aliehalifu watu wa ba'ath katika utawala,alikuwa akifata nyayo za Abdinasir,isipokuwa vibaraka wa Uingereza katika wana siasa na maofisaa wa jeshi wamepata mbele yao fursa muhimu ya kuchangamka,kwa juhudi kidogo wakadhibiti jeshi,juu ya matukio ya kiuchumi,ikarudi Iraq kwa Uingereza.Juu ya kuwa Marekani iliirudia Iraq katika zama za Abdurrahman Arif,isipokuwa waingereza katika watu wa ba'ath na wengineo walidhibiti utawala mwaka wa 1968 M,yakaendelea mamlaka ya Uingereza huko Iraq mpaka 9/4/2003 M ilipoanguka Baghdad,kuanguka nidhamu ya Saddam Hussein na utawala wa ba'ath Iraq,ilipoingia Iraq chini ya uvamizi wa Marekani.

Amma Misri,hakika tangu alipochukuwa utawala Abdinasir ikawa ni kambi kubwa ya kimarekani na bado mpaka sasa ni kambi ya kimarekani muhimu,wala haikutokezea amali zozote za kisiasa muhimu zinzoingia katika mvutano isipokuwa yaliotokea baada ya kufariki Abdinsir kwa mda mchache,zilipotimu sehemu ingewezekana kurudisha Misri kwa Uingereza:

**Kwanza:** Ulisimamautawala dhaifu usioweza kujihifadhi,licha ya kuziba nafasi alioiwacha Abdinasir.

**Pili:** Ulipatikana Misri uchangamfu katika jeshi na wananchi wakitangaza vita nayo ikitangaza kumfukuza mrusi (muungano wa kisovieti) na kutangaza kujikomboa kikamilifu.

**Tatu:** Mawasiliano baina ya Uingereza na Misri yalioanza kwa ziara ya Douglas Home waziri wa nje wa Uingereza ya Misri kwa hoja ya kuzuru jeneza la Abdinasir,zikafatia ziara kadha kutoka Uingereza kupitia Libya,kisha ikawa rasmi si kwa ziara ya Muhammad Hassanein Heikal peke yake bali kwa barua rasmi, kutaka kiwazi kutoka Misri

kujenga mahusiano baina yake na Uingereza,ikawa kurudi Misri kwa Uingereza kuwa ni swala la zama peke yake na swala la juhudi kulingana na kituo cha mabwana chenye wasiwasi mwanzo wa utawala wake.Lakini Marekani akaweza kumakinika mabwana katika utawala juu ya hayo,ikabuni chama mwaka wa 1973 M,kuandaa amani na Israel akafanya katika mabwana kuwa mashujaa ikammakinisha kuchukuwa usimamizi wa mambo, kwahiyo ukafichika mvutano wa kimataifandani ya misri na kuendelea kambi ya Marekani kubwa na muhimu mpaka sasa.

Amma serikali za kazkazini Afrika hakika Moroko iliingia chini ya udhibiti wawakati wa kujikomboa kwake wakati wa Muhammad V na Aljeria ikawa ya Marekani kwa fadhila ya Ahmed bin Bella.Lakini hayo hayakudumu mda mrefu,hakika Muhammad V alikuwa amefariki na kusimamia utawala mtoto wake Hassan akawa na Uingereza.Amma bin Bella hakika aliandaa mapinduzi dhidi yake kipitia njia ya mfalme Hassan,kupitia Muhammad Khidar,wakawavutia Thwahir Zubeir na Abu Madin,wakatekeleza mapinduzi yaliomuangusha Muhammad bin Bella,ikatolewa Marekani kutoka Aljeria na kuwa Uingereza ndio yenye mamlaka humo.Amma Libya na Tunisia hakika Marekanihaikuweza kuingia kwa yoyote wala kutekeleza amali yoyote ya kisiasa kwa yoyote,bali yalibakia mamlaka ya Uingereza yaendele humo.Kwahiyo hawakushiriana katika mvutano Marekani na Uingereza.Amma Yemen na serikali za ghuba isipokuwa Saudia za nyenyekea mamlaka ya Uingereza wala hakuna mvutano kwa maana inayojulikana isipokuwa Yemen,ambapo mamlaka ya Uingereza humo yapambana na usumbufu kutoka kwa

Marekani mkakamavu unaovuta.Amma Saudia imeweza Marekani kuvutia baadhi ya watu wa jamii ya wafalmewaliobakia kwa Uingereza watu wake ni jamii ya wafalme pia.Wazunguka mvutano wa Uinereza na Marekani humo kupitia watu wa jamii,kwa kutokea Fahdi bin Abdulaziz kwa mfano,imekuwa Saudia yenda katika mzunguko wa Marekani,lau ingebadilika halikwa kuja muingereza mmoja katika utawala kama Abdallah msimamizi matarajiwa,basi itarudi Hijaz na Najdi katika mamlaka ya Uingereza,hivi ndivyo yalivyo,hata kama Marekani baada ya ulipuaji wa 11/9/2001 M ilibadilisha kudhibitisha mamlaka yake Saudia pasi na kuogopa kuhangaika watu wa jamii, kwa kupatikana mabadiliko katika mfano uliozoeleka.Itaonyesha kwamba chini ya usomi wa amanayepalaka siasa Washington,kama zinavyo nukuluwa habari.

Ukaendelea mvutano wa Marekani na Uingereza kuzidi katika biladi za kiarabu katika miaka ya hamsini na sitini karni iliopita,likaendelea swala la Palestina ndio msingi wa mvutano huu,kwakuwa Uingereza mwaka wa 1964 M wakafikia katika kukinai na eneo kwamba halipatikani maandalilzi ya kukubali kuvunjika serikali ya kigeni kindani na kwamba jariio la kusimamisha ya kiyahudi Palestina ndio jaribio lililo shindwa.Kwahiyo ni bora kusimamia serikali ya elmani kwa mfano serikali ya Lebanon,hilo kwa kurudi kuhuisha mradi wa karatasi nyeupe alioiweka Ungereza mwaka wa 1939 M,akaifanya msingi wa utatuzi wa swala, wakawaambia wakubwa wa kiyahudi,wakakinai na fikra hii,akatekeleza Habib Bourguiba kiongozi wa Tunisia ziara ya Misri,Jordan,Lebanon,Kuwaeit,Saudi na kuweka mradi wa Uingereza uliotajwa kwa viongozi wa kiarabu na

baadhi yaw a palestina, akachukuwa makubaliano jumla mradi ule,ikaanza Uingereza kujaribu kutekeleza. Lakini Marekani kupitia kibaraka wakeAbdinasir akaweza kuuangusha mradi huu kwa kuupinga vikali.
Kwa haya yote yabainika kwamba kadhia ya Mashariki ya Kati upande wa kimataifa,ilkuwa ni lazima ilikuwa ni lazima iwe kadhia ya mvutano baina ya wetu wa eneo na baina ya serikali za kikoloni,kama ilivyotokea na Marekani yenyewe ilipoutowa ukoloni,akabuni serikali ya muungano wa majimbo na kama ilivyotekea na China baada ya vita vya pili vya dunia ilipofukuza ukoloni wa Japan na mamlaka ya kigeni,ikasimamisha serikali ya kikoministi ilioko na daraja ulimwenguni.Kama ilivyo kawaida katika kila biladi iliokoloniwa,iliopewa uwezo wa kimataifa na uweza wa kimaeneo kujikomboa kutokana na mamlaka ya kigeni, kujibunia serikali ilio na kiwango cha kimataifa,lakini kimasikitiko,haikuwa hali hii ndio hali ya kadhia ya Mashriki ya Kati bali ilikuwa ni kadhia ya kimataifa ni mvutano mkali baina ya Marekani na Uingereza wa kukoloni eneo na kulipora.Ili kupatikana vikwazo vipya vinavyo vika vikali vinvyo wazuia watu wa eneo wasifikiria kwa kufikiria kujikombo peke yake.Ukaendelea mvutano baina ya Marekani nan a Uingereza lakini kwa mkazo mwepesikatika miaka ya sabini na thamanini ya karni iliopita.
